# Nipashe

Jumatatu Juni 17, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579946

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Sugu ampongeza Mwakyembe, atoa tahadhari uchaguzi wa 2020

UKURASA 4




UKURASA 13

## SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Ubakaji watoto watisha

**Waziri** Ummy asema matukio yanayoongoza ni ubakaji, ulawiti pamoja na mimba za utotoni...*Endelea uk. 2*

### YALIYOMO

UKURASA WA 3

**UTAFITI WAFICHUA SIRI UZAZI MPANGO, MAAMBUKIZI VVU**

UTAFITI uliofanywa na muunganiko wa magwiji wa utafiti Duniani kuangalia endapo kuna uhusiano wa kupata Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa mwanamke anayetumia njia za uzazi wa mpango (ECHO) ...

UKURASA WA 2

**LUGOLA APOKEA RIPOTI WAFUNGWA KUTOROKA**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amepokea ripoti mbili za uchunguzi ikiwamo ya kifo chenye utata cha Isululu Kabote (85), mkazi wa Kijiji cha Buhungukila ...



Katibu Tawala Msaidizi wa Mipango na Uratibu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Yokobety Malisa, akisoma moja ya mabango ya wanafunzi jana, kabla ya kuhutubia katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwenye viwanja wa Shule ya Msingi Makuburi wilayani Kinondoni, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## SERIKALI YAJITOSA NYUMBA 4,000 DAR

UK 3

# Zitto Kabwe ataka bei elekezi taulo za kike

UK. 2

**MICHEZO** MAYANGA MBIONI KUJIUNGA NA KMC UK.31

MAONI, KATUNI UK.6

## Ripoti kifo cha Kabote, kutoroka kwa wafungwa zatua kwa Lugola

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amepokea ripoti mbili za uchunguzi ikiwamo ya kifo chenye utata cha Isululu Kabote (85), mkazi wa Kijiji cha Buhungukila, Kata ya Bugarama, Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu.

Kabote alidaiwa kuuawa akiwa mikononi mwa polisi Mei 17, mwaka huu, saa 8:00 usiku. Pia Lugola alipokea ripoti ya uchunguzi wa tukio la kutoroka mahabusu 17, Mei 21, mwaka huu, mkoani Geita.

Mahabusi hao walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita wakikabiliwa na mashtaka mbalimbali na kuwekwa kwenye ukumbi wa jengo jipya la mahakama wakisubiri kusomewa kesi zao.

Ripoti ya uchunguzi wa kifo cha marehemu Kabote iliwasilishwa na Lalph Meela (Mwenyekiti), kutoka Dawati la Malalamiko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Wajumbe ni Daktari Bingwa wa Mifupa kutoka Hospitali ya Rufani ya Dodoma, Ibenze Ernest, Kefa Kaswamila kutoka Dawati la Malalamiko Kitengo cha Upelelezi Wizara ya Mambo ya Ndani na Mzee Mzee kutoka Ofisi ya Ofisa Usalama, Mkoa wa Simiyu.

Kamati hiyo ilifanya uchunguzi huo kuanzia Juni 4 hadi 10, mwaka huu na ripoti ya uchunguzi wa tukio la kutoroka wafungwa ilikabidhiwa na Mwenyekiti wake, Alex Mfungo.

Baada ya kupokea ripoti hizo, Lugola alisema ameridhishwa na matokeo ya uchunguzi huo na wajumbe wa kamati zote walipata fursa ya kuzichambua na kutoa mapendekezo.

Viongozi wengine waliokuwapo wakati Lugola akipokea ripoti hizo ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Meja Jenerali, Jacob Kingu na Naibu Katibu Mkuu, Ramadhani Kailima.

Kamati ya uchunguzi wa kifo cha Kabote iliundwa baada ya wananchi wa kijiji hicho kudai kabla ya kukumbwa na mauti, alikamatwa na polisi, kupigwa akidaiwa hajatoa mchango wa maendeleo Sh. 50,000 madai ambayo Jeshi la Polisi liliyakanusha.

Mwili wa marehemu Kabote ulikaa siku 20 katika chumba cha kuhifadhia maiti kwa ajili ya uchunguzi wa kidaktari.

## SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Ubakaji watoto watisha

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Tanzania ikiungana na mataifa mengine barani Afrika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, takwimu zinaonyesha matukio ya ubakaji kwa watoto yanashika kasi nchini.

Takwimu zilizotolewa hivi karibuni na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), zinaonyesha kuwa katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo kwa mwaka 2018 watoto 2,365 walibakwa, idadi ambayo ni sawa na watoto 394 kwa siku.

Aidha, ripoti ya hali ya uhalifu kwa mwaka 2017 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya

Takwimu (NBS), inaonyesha katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2017, matukio ya uhalifu dhidi ya watoto yalikuwa 13,457.

Kadhalika, kwa mwaka 2016 matukio hayo yalikuwa 10,551, na kwamba kati ya hayo, matukio ya ubakaji yalikuwa 2,984.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (Unicef), inaonyesha kuwa wabakaji wengi ni ndugu wa karibu ambao wanaishi ndani ya familia.

Kutokana na hali hiyo Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), kimeiomba serikali na wadau wengine wa masuala ya haki za watoto kuendelea kupaza sauti zao ili kuhakikisha ukatili huo unapungua na ikiwezekana kumalizika kabisa.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tamwa, Rose Reuben, ilisema kuwa matukio ya ubakaji wa watoto ni tishio kwa usalama wao, ukuaji wao kwa ujumla na maendeleo endelevu ya taifa.

"Mtoto ni taifa la kesho, endapo atafanyiwa ukatili leo, je, kesho taifa hili litaongozwa na nani? Tamwa tunasisitiza hatua kali za kisheria na mabadiliko mengine ya kisera ili kumlinda mtoto dhidi ya ukatili," alisema Rose.

Aliwasihi wazazi, walezi kulipa uzito mkubwa suala la ulinzi kwa mtoto ili kuepusha ubakaji.

"Kupinga unyanyasaji, ubakaji na ulawiti wa watoto ni jukumu la jamii nzima na wakati umefika sasa kila mmoja kwenye nafasi yake awalinde watoto kwa kuripoti vitendo vya unyanyasaji vilivyofichika kwenye jamii yetu," alisisitiza.

Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika hufanyika kila Juni 16, na kaulimbiu ya mwaka huu ni: "Mtoto ni msingi wa taifa endelevu, tumtunze, tumlinde na kumwendeleza."

Kwa upande wa Tanzania Visiwani, vitendo hivyo vimedaiwa kuongezeka licha ya Tanzania kuwa ni nchi iliyosaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda yenye lengo la kuwalinda watoto dhidi ya udhalilishaji.

Akizungumza na waandishi wa habari

INAENDELEA UK. 8



Wafagiaji wa barabara wakiwa kazini, eneo la Tataba Segerea, jijini Dar es Salaam juzi. Baadhi yao hufanya kazi hiyo bila kuwa na vifaa vinavyozuia vumbi puani, kuvaa viatu maalum pamoja na kuweka alama zinazowatambulisha kuwa wako kazini, hivyo kuwapo uwezekano wa kupata ajali. **PICHA: SABATO KASIKA**


**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na muda ni kuanzia saa nne asubuhi. Mnada huo utaendeshwa na Madalali tajwa hapo chini kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZANIA LTD.**

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| Daniel Thomas Maiko | Kiwanja | Mivumoni- Madale | 30/6/2019 | Raisa Co. Ltd |
| Abdallah Nassoro Salmin | Shamba Ekari 3 | Ngeta - Mlandizi | 29/6/2019 | Tavir A/Mart |
| Mbegu Kangamka Ahmed | Nyumba | Pugu – mtaa wa Bombani | 22/6/2019 | Emashi A/Mart |
| Alfred Asajile Kandonga | Kiwanja - Kimepimwa | Kahama Street - Kahama | 28/6/2019 | Josina Co. Ltd |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki zitakuwa juu ya Mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na;-**
**Emashi A/Mart: 0655208575;**
**Champion Auctioneer: 0654200448/0756761328**
**Tavir A/Mart: 0717 495311; Josina Co. Ltd: 0713/0768/203040**

**TUJIJENGE TANZANIA LTD**
**MOB: 0718276859/0718068335 (HQ).**

215278002


## Zitto ataka bei elekezi ya taulo za kike

**Na Enock Charles**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT -Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema serikali imeweka kodi katili kwa wanawake kwa kurejesha kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa taulo za kike na mawigi na kuwa serikali ilipaswa kukaa na wafanyabiashara na kuweka bei elekezi ya taulo hizo badala ya kurejesha kodi katika vifaa hivyo.

Zitto ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini kupitia chama hicho, ameifananisha hatua hiyo na kutoza kodi ya hedhi.

"Serikali ilipaswa kukaa na wafanyabiashara wa pads (taulo za kike) kuweka bei elekezi kwa sababu bei zinazowekwa kwa retail (rejareja), ni bei kubwa sana kutoka asilimia 30 hadi asilimia 40," alisema Zitto.

Akizungumza na vyombo vya habari jana katika ofisi za makao makuu ya ACT-Wazalendo kuzungumzia bajeti ya mwaka 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Alhamisi na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, Zitto ambaye kitaaluma ni mchumi, alisema kuongeza kodi ya taulo za kike ni sawa na kuwaadhibu zaidi ya wanawake milioni 12 nchini ambao huingia katika siku zao kila mwezi.

Kiongozi huyo alisema serikali ilipaswa kufanyia utafiti biashara ya vifaa hivyo na kuangalia mfumo mzima wa usambazaji kabla ya kuja na mapendekezo ya kuongeza kodi kwa kuwa kufanya hivyo, bei ya taulo hizo inaweza kuongezeka zaidi.

"Inawezekana kabisa zikauzwa mpaka kwa ya Sh. 1,000 iwapo serikali itatazama mfumo mzima wa usambazaji," Zitto alisema.

Ameishauri serikali kutenga eneo maalum (Special Economic Zone) kwa ajili ya viwanda vya uzalishaji wa taulo za kike mkoani Simiyu hasa kwa kuzingatia kuwa mkoa huo huzalisha pamba kwa wingi ambazo ndio hutumika katika kutengenezea hizo.

Akizungumzia Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2019/20, amesema bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni bajeti ya vitu zaidi kuliko watu kwa kuwa miradi ya maendeleo inayowagusa wananchi wa kawaida imetengewa fedha kidogo na fedha nyingi kuelekezwa kwenye miradi ya vitu.

"Ni bajeti ya vitu, asilimia 55.7 ya bajeti yote ya maendeleo ni ya vitu... watu unawapata kwenye elimu, maji , afya, kilimo, uvuvi na mifugo," alisema Zitto na

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Serikali yaingilia kati fidia nyumba 4,000 Dar

**Na Mwandishi Maalum**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ameagiza kupitiwa upya mkataba wa mauziano ya nyumba kati ya Kampuni ya PMM 2001 Ltd na wamiliki wa nyumba 4,000 wakazi wa Vingunguti jijini Dar es Salaam.

Uamuzi huo unafuatiwa kutozingatiwa kwa masharti ya mkataba ulioingiwa awali ambao umeonekana kuwa na mapungufu mengi ya kisheria, hivyo kusababisha kampuni ya PMM 2001 Ltd kushindwa kuwalipa wamiliki wa nyumba katika eneo la Vingunguti kwa takriban miezi tisa kama walivyokubaliana jambo lililozua taharuki kwa wamiliki wa nyumba hizo.

Mabula alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kukutana na pande zote mbili za kamati inayosimamia makubaliano ya uuzaji nyumba 4000 katika mitaa minne ya Vingunguti ambayo ni Mnyamani, Mtambani, Mtakuja na Faru, kampuni ya PMM 2001 Ltd na Mbunge wa Segerea, Bona Kamoli, katika ofisi za wizara jijini Dodoma.

Alisema, baada ya kupitia mkataba wa mauziano ya nyumba katika eneo la Vingunguti kati ya Kampuni ya PMM 2001 Ltd na wamiliki wa nyumba katika eneo la Vingunguti wamebaini mkataba kutofuata taratibu za kisheria na kubainisha kuwa wamiliki ambao hawajalipwa fedha yoyote hawabanwi na mkataba huo na wanaweza kuzifanyia shughuli yoyote nyumba zao.

Alisema, kwa zile nyumba 80 ambazo kampuni ya PMM 2001 Ltd ilizinunua kwa wamiliki katika eneo hilo, wizara yake itatuma timu maalum kufuatilia iwapo kampuni hiyo imefuata taratibu zote za mauziano ikiwamo kutoa kodi ya serikali na kuongeza kwa kuitaka kuhakikisha inakamilisha taratibu za kumilikishwa nyumba hizo.

Kuhusu suala la wamiliki wa nyumba 17 ambao kampuni hiyo imewalipa Sh. milioni 35 kwa kila mmoja kama fedha za awali, Mabulai aliagiza hatua za kisheria zifuate kwa kuwa mkataba wa mauziano hauonyeshi kiasi kilichobaki baada ya kutolewa cha awali sambamba na muda wa ukamilishaji malipo jambo lililosababisha wamiliki kufuatilia kwa muda mrefu bila mafanikio.

Kwa mujibu wa Mabula, ilichokifanya kampuni ya PMM 2001 Ltd kwa wamiliki ni udanganyifu unaoweza kutoa mwanya mkubwa

INAENDELEA UK. 8

## Utafiti wafichua siri uzazi mpango, maambukizi VVU

**Na Elizabeth Zaya**

UTAFITI uliofanywa na muunganiko wa magwiji wa utafiti duniani kuangalia endapo kuna uhusiano wa kupata Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa mwanamke anayetumia njia za uzazi wa mpango (ECHO), umebaini kwamba hakuna uhusiano wa kupata maambukizi hayo kwa kutumia njia hizo za uzazi wa mpango.

Utafiti huo wa kubaini uhusiano wa maambukizi hayo ya VVU na matumizi ya njia za uzazi wa mpango umechukua muda wa miaka minne kukamilika kuanzia mwaka 2015 hadi Desemba 2018 na kutolewa rasmi Juni 14 mwaka huu na ulifanywa kwa kuangalia maambukizi hayo kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Kenya, Eswatin na Afrika Kusini.

Akizungumza katika semina ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam iliyoandaliwa na Inter News mwishoni mwa wiki kwa ajili ya kuwajengea uwezo juu ya utafiti huo na masuala mengine ya afya, Mhamasishaji Jamii wa VVU na Afya ya Uzazi, Dk. Lilian Mwakyosi, alisema utafiti huo ulihusisha njia za uzazi wa mpango

INAENDELEA UK. 8




MAHOJIANO MAALUM

# Sugu ampongeza Mwakyembe, atoa tahadhari uchaguzi wa 2020

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (pichani) (Chadema), amempongeza Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya sanaa na burudani mwaka huu.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma hivi karibuni, makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema sekta hiyo imeongoza sekta zote kwa kasi ya ukuaji kiuchumi mwaka huu.

Dk. Mpango alisema sekta hiyo mwaka huu imekua kwa asilimia 13.7 ikifuatwa na sekta za ujenzi asilimia 12.9, uchukuzi na uhifadhi wa mizigo asilimia 11.8 na habari na mawasiliano asilimia 9.1.

Katika mahojiano maalum na Nipashe bungeni jijini Dodoma wiki iliyopita, Sugu alisema kuwa pamoja na kwamba yeye ni mbunge wa upinzani, anampongeza Dk. Mwakyembe kwa mafanikio hayo, akieleza kuwa yametokana na waziri huyo kufanyia kazi ushauri wa wabunge.

Mbali na kumpongeza mtaalamu huyo wa sheria, Sugu pia alizungumzia hukumu ya kutumikia kifungo cha miezi sita gerezani aliyopewa hivi karibuni kisha kuachiwa kwa msamaha wa Rais John Magufuli. Katika mahojiano hayo, Sugu ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alizungumzia hali ya kisiasa nchini, husan upinzani mkali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) unaomkabili katika kuwania tena ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini.

**Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mbunge huyo:**

**SWALI:** Sekta ya sanaa na burudani imeongoza kwa kasi ya ukuaji kiuchumi mwaka huu. Wewe ni msanii na ni waziri kivuli katika wizara inayosimamia sekta hii, mafanikio hayo yamechochewa na kipi hasa?

**SUGU:** Kwa kweli ni mafanikio 'positive' (chanya) na kitu ambacho tumekuwa tukikipigania miaka mingi. Ni kwamba juhudi zilikuwapo na hayo yanayoitwa mapato yalikuwapo. Shida yetu si kwamba mapato hayakuwapo, shida yetu ilikuwa kwamba hayakuwa na udhibiti na ufuatiliaji.

Kwa hiyo, mapato yalikuwa hayawafikii walengwa ambao ni wasanii, lakini pia serikali ilikuwa haifikiwi na mapato haya kwa maana ya kodi.



Na ndiyo maana tukawa tunasisitiza sanaa irasmishwe kwa sababu ikishakuwa rasmi, inakuwa rahisi kwa serikali kuifuatilia, na ukishaifuatilia, utaisimamia vizuri na ukiisimamia utapata kilicho cha kwako na walengwa watapata kilicho cha kwao.

Kwa hiyo, mafanikio hayo si kwamba yametokea kwa bahati mbaya, yametokana na kazi ambayo tumekuwa tukiifanya humu bungeni.

Nipeleke tu 'credits' (pongezi) kwa Mheshimiwa Waziri (Dk. Mwakyembe) kwa sasa kwa kuwa pamoja na kutokusema, lakini amekuwa akichukua ushauri wetu.

**SWALI:** Unafikiri mafanikio haya ni ya msanii mmoja mmoja?

**SUGU:** Hapana! Ni 'collective' (kwa ujumla). Hata unaposema kilimo kimefanikiwa, haimaanishi kwamba wakulima wote wako sawasawa.

Sasa tunajua kama wasanii eneo letu lina mapato kiasi gani. Ni kazi yetu sisi kama wasanii mmoja mmoja kupigana kupata kipande katika zile 'revenues' (mapato) zote.

**SWALI:** Kwa hali ilivyo kisiasa nchini, matumaini ni makubwa kiasi gani kwamba utarejea bungeni baada ya uchaguzi mkuu wa mwakani?

**SUGU:** ... (kicheko) Nikuhakikishie tu kwamba Sugu atakuwapo bungeni baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2020. Hapa katikati yetu na mwaka 2020 wa uchaguzi, kuna Mungu tu, hakuna binadamu atakayezuia. Na hilo tumeshalisema wazi - suala la ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini si Sugu kuwa mbunge. Suala lililopo Mbeya ni kura za Mbeya zinachangia vipi katika kura za kitaifa ii kuing'oa serikali ya CCM. Hiyo ndiyo hoja ya wanaMbeya, kwamba kura zao zinatoa mchango gani katika kuing'oa CCM madarakani 2020 na si suala la mbunge. Suala la Mbunge wa Mbeya Mjini tulishalimaliza tangu mwaka 2010. Kilichotokea mwaka 2015, ndicho kitakachotokea mwaka 2020 na ndiyo maana nasema, kati yetu na uchaguzi wa mwaka 2020, hatuna binadamu wala mtu yeyote mbali kuna Mungu tu! Ni suala la kuomba uzima.

**SWALI:** Kifungo cha miezi sita dhidi yako, kimekupa funzo gani?

**SUGU:** Nilichojifunza ni kwamba sasa Tanzania imeanza kuzalisha wafungwa wa kisiasa. Mimi nilifungwa kisiasa. Ukiniuliza nimepata funzo gani kama unavyoniuliza leo, ukweli kutoka moyoni mwangu, ooh kumbe Tanzania sasa imeanza kuzalisha wafungwa wa kisiasa.

SWALI: Changamoto kubwa inayolikabali Jimbo la Mbeya kwa sasa ni ipi na hatua zipi zimechukuliwa kuitatua?

**SUGU:** Changamoto kubwa Mbeya Mjini kwa sasa ni baadhi ya viongozi wa CCM kutaka kuleta siasa uchwara kwenye masuala ya maendeleo tunayoyafanya pale chini ya mbunge ambaye ni wa Chadema na halmashauri ambayo pia iko chini ya Meya wa Chadema.

CCM wamekuwa wanafanya vitu ambavyo unaweza kuviita vya ovyo sana, ili kuvuruga mafanikio ya halmashauri iliyo chini ya Chadema na hata pengine kutaka ionekane kwamba mbunge hajafanya kitu chochote, lakini wananchi wa Mbeya si wajinga.

Pale kuna wasomi, wameelimika, wana ufahamu na wanamfuatilia mbunge wao na wanajua kila kinachoendelea.

Kwa hiyo, tatizo la Mbeya Mjini ni siasa uchwara zinazoletwa kila siku. Lakini pia watendaji kama RC (Mkuu wa Mkoa), DC (Mkuu wa Wilaya) ambao wanaacha kutekeleza majukumu yao ya msingi, 'focus' yao inakuwa jinsi ya kumwangusha Sugu.

Mimi siangalii mtu mmoja mmoja, nakiangalia Chama Cha Mapinduzi kwa sababu hata mwaka 2015, kuelekea Uchaguzi Mkuu tulikuwa na kelele hizi hizi kuhusu dada yangu Mary Mwanjelwa. Mwanjelwa... Mwanjelwa... kelele zilipigwa kama sasa anavyotajwa Dk. Tulia (Ackson).

Lakini mwisho wake, sikugombea na Mwanjelwa, chama kilipitisha mtu mwingine kabisa tofauti. Kwa hiyo, nyinyi mnaozungumza pengine hamjui siasa za Mbeya na siasa za CCM wenyewe kule Mbeya.

Ziko tofauti sana. Pengine mnayemtaja kwenye mitandao na magazeti yetu, huenda asiwe yeye kwenye uchaguzi. Ndiyo maana mimi nasema mbele yangu siangalii mtu yeyote, mimi nakisubiri Chama Cha Mapinduzi.

**SWALI:** Ni miaka mingi Sugu hajatoa wimbo mpya. Umeamua kuachana na muziki?

**SUGU:** Sijatoka kwenye muziki, kutokutoa wimbo hakuna maana kwamba nimetoka. Daktari asipotibu wagonjwa kwa siku mbili, tatu, haina maana kwamba ameacha udaktari.

Kwenye muziki bado tumo, lakini sasa hivi kutokana na 'situation', wewe ni mwanahabari unafahamu tumeshatoa mwongozo wa namna muziki wetu uwe.

Kwa sababu sasa tunaona ni vigumu kubaki, kuendelea kuwa 'professional artist', unaangalia sasa ni namna gani utaenenda.

**SWALI:** Ukiamka asubuhi na kujiangalia kwenye kioo, unaona nini mbele yako?

**SUGU:** Eeh... ninaiona 'future' yangu binafsi nikijaribu kuioanisha na 'future; ya taifa letu itakuwaje!

Na ninapovioanisha hivyo, ndiyo maana naacha kuwa 'selfish' (mbinafsi) katika mambo ya kitaifa, nayazungumza na kutoa mchango wangu na si tu kuangalia mimi kama mimi nimevaa suti nzuri, niko vizuri, basi niache kusema mambo ya msingi ya taifa.



## HABARI KITAIFA

# Biashara saruji kwenda DRC, Burundi kushika kasi

**Na Mary Geofrey,** KALAMBO

BIASHARA ya saruji kwenda nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Burundi, inatarajiwa kushika kasi na kukuza uchumi wa Taifa, baada ya upanuzi wa gati la kisasa kukamilika, katika Bandari ya Kasanga wilayani Kalambo mkoani Rukwa.

Kwa sasa bandari hiyo ina gati lenye urefu wa mita 20 lenye uwezo wa kupokea meli moja na mpango wa Mamlaka ya Bandari (TPA) ni kuongeza gati lenye urefu wa mita 100 na kufika mita 120 litakalowezesha kupokea meli tatu za mizigo na abiria.

Meneja wa Bandari ya Kigoma anayesimamia bandari zote za Ziwa Tanganyika, Ajuaye Msese, akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea bandari hiyo juzi, alisema bandari hiyo inategemewa kwa kusafirisha saruji kutoka Mbeya kuelekea nchi za Congo na Burundi.

> **Alisema upanuzi wa bandari hiyo utakaogharimu Sh. bilioni 4.7 utawezesha shehena kubwa ya saruji kusafirishwa kwenda nchi hizo kutoka tani 20,000 kwa mwaka hadi tani 100,000 kwa mwaka.**

Alisema upanuzi wa bandari hiyo utakaogharimu Sh. bilioni 4.7 utawezesha shehena kubwa ya saruji kusafirishwa kwenda nchi hizo kutoka tani 20,000 kwa mwaka hadi tani 100,000 kwa mwaka.

"Kuboreshwa kwa bandari hii ya kimkakati inayotegemewa na mikoa ya Katavi, Mbeya, Songwe na Rukwa utawezesha kukuza uchumi wa Taifa. Bidhaa kubwa inayosafishwa kwenda DRC na Burundi ni saruji ambayo inazalishwa na kiwanda cha Safuri cha Mbeya Cement. Hivyo tunatarajia mizigo itakayosafirishwa inaongezeka mara tano zaidi," alisema Msese.

Alisema mapato ya bandari hiyo kwa mwaka ni Sh. bilioni moja hivyo wanatarajia yataongezeka mara dufu baada ya kukamilika mradi huo.

Adha, alisema bandari hiyo ambayo ipo Kusini mwa Ziwa Tanganyika, ina ghala la kuhifadhi tani 2,000 za saruji na ghala lingine la nje lenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,000 ya makaa ya mawe.

Alisema zaidi kuwa, upanuzi wa gati hilo utaenda sambamba na ujenzi wa sakafu ngumu, ujenzi wa nyumba za wafanyakazi, ghala kubwa la kuhifadhia shehena ya mizigo na ofisi za taasisi za umma zinazofanya kazi na bandari. Adha, alisema kuelekea katika bandari hiyo kulikuwa na changamoto ya barabara ya kutoka Namanyele kuelekea Kisanga ambayo kwa sasa imeanza kujengwa na Wakala wa Barabara (Tanrods) ili kuongeza ufanisi wa bandari.

# Uhakiki mizani ya pamba waanza

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAKALA wa Vipimo (WMA) umeanza kuhakiki mizani inayotumika kupima zao la pamba kabla ya msimu kuanza ili kuwasaidia wakulima kunufaika na kilimo hicho.

Akizungumza katika ziara ya ukaguzi wa mizani hiyo mikoa ya Kanda ya Ziwa, Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa WMA, Irene John, alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa wakala huo kuhakikisha mizani inayotumika kupima zao hilo kupitia vyama vya msingi vya ushirika ni sahihi.

Alisema ukaguzi huo unaendelea katika mikoa saba ya kanda hiyo, ili kuendelea kujiridhisha kama bado mizani hiyo ni sahihi, haijachezewa wala kufanyiwa uhalifu na wajanja wachache.

"Kuelekea msimu huu wa pamba tunafanya uhakiki wa mizani yote inayokagua pamba, ufuta, kahawa na tumbaku, ingawa kwa sasa tumeanza na pamba kwa sababu msimu wake ndiyo umeanza.

"Nia yetu ni kulinda wakulima wapate thamani ya jasho lao, kwamba akipeleka kilo 100 kweli ziwe ni halisi kwenye mzani na si vinginevyo," alisema Irene.

Irene alisema katika ukaguzi huo mpaka sasa hawajapata mizani iliyochezewa isipokuwa kasoro ndogondogo za kawaida, huku akiishukuru serikali kwa kurekebisha sheria ya vipimo na kuipa nguvu WMA katika kutekeleza kazi zake.

Aidha, alisema marekebisho ya sheria Na 340 na mapitio yake ya mwaka 2016 yanatoa adhabu kwa yeyote anayechezea mizani au kuweka uchafu kwenye pamba kwa masilahi binafsi, ambapo adhabu yake ni faini kuanzia Sh. 100,000 hadi Sh. milioni 20 kwa anayekiri kosa na wale wanaofikishwa mahakamani hutozwa faini ya kati ya Sh. 300,000 hadi Sh. milioni 50, kifungo cha miaka miwili jela au adhabu zote kwa pamoja.

Alisema elimu inayotolewa kwa wakulima kuhusu mizani na vipimo sahihi kabla ya msimu kuanza, imesaidia kutoa uelewa na hivyo kupunguza uchakachuaji na kupatikana pamba iliyo safi na hivyo kukuza uzalishaji.

Mikoa ambayo mizani yake imefanyiwa ukaguzi ni Tabora (158), Kagera (26), Mara (332), Shinyanga (589), Simiyu (832), Mwanza (360), Geita (523) na Katavi (50) ambapo jumla ni wastani wa mizani 2,950.

Yetu Microfinance Bank PLC

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

## TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DECEMBER 2018

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2018.**
Kiwango kwa Tzs.'(000)'

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 TZS | Mwaka Uliopita 31-Dec-17 TZS |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 273,805 | 365,395 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 0 | 0 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 0.00 | 0.00 |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 750,768 | 1,908,880 |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | 0.00 | 0.00 |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 12,613,928 | 12,551,116 |
| 12 | Mali Nyingine | 873260.00 | 271,162 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0.00 | 0.00 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 440,883.00 | 504,465 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **14,952,644** | **15,601,018** |
| B. | **DHIMA** | | **0** |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | **0** |
| 18 | Amana za Wateja | **1,198,826** | **922,323** |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | **0.00** |
| 20 | Amana Maalumu | **1,034,089** | **2,427,458** |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | **0.00** | **0.00** |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | **0.00** | **0.00** |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | **58,156** | **152,171** |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mte | **0.00** | **0.00** |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi | **0.00** | **0.00** |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | **893,371** | **196,491** |
| 28 | Madeni | **4,000,000** | **3,650,000** |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **7,184,442** | **7,348,443** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **7,769,299** | **8,252,575** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | **6,056,497** | **6,056,497** |
| 32 | Akiba ya Mtaji | **130,555** | **191,464** |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | **803,429** | **547,466** |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | **708,029** | **1,299,984** |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | **69,693** | **157,165** |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | | **-** |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **7,768,203** | **8,252,576** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | | **0** |
| 39 | Mikopo chechefu | **872,734** | **726,128** |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | **1,326,281** | **1,056,304** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | **0.00** | **0.00** |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | **%** | **%** |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 52% | 53% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6% | 5% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **624%** | **406%** |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 84% | 80% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84% | 80% |
| vi | Ongezeko la Amana | **0%** | 0% |
| vii | Ongezeko la Mali | **-4%** | **9%** |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018.**
Kiwango kwa Tzs.'(000)'

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 TZS | Mwaka Uliopita 31-Dec-17 TZS |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 5,027,399 | 4,842,509 |
| 2 | Gharama za Riba | 404,573 | 312,785 |
| 3 | **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **4,622,826** | **4,529,724** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | 0.00 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | -79,869 | 19,995 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **834,012** | **870,156** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 617,919 | 600,925 |
| | 6.3 Gawio | | |
| | 6.4 Mapato Mengine | 216,093 | 269,231.00 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **4,408,800** | **3,607,920** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 1,934,470 | 1,689,827 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0.00 | 0 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 2,474,330 | 1,918,093 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **968,169** | **1,811,955** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 260,140 | 511,971 |
| 10 | **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **708,029** | **1,299,984** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | **0.00** | **0.00** |
| 12 | **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **708,029** | **1,299,984** |
| | | | **-** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **125** | 83 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | **59** | 107.31 |
| 15 | Idadi ya Matawi | **3** | 3 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | **31%** | 29.03% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | **60%** | 54.89% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | **95%** | 79.65% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | **37%** | 36.09% |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2018**

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa Hisa | | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya juma | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la wa mwaka 01/01/2017** | 6,056,497 | | - | - | 292,985 | 1,245,448 | 7,594,930 |
| Rekebisho : | | | | | | | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha mwaka | - | | - | - | - | - | - |
| Toa: Mapato mengine | - | | - | - | (135,820) | - | (135,820) |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | | 124,847 | | | (124,847) | - |
| Mtaji wa kisheria | | | | 66,617 | | (66,617) | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | - | - | - | 1,299,984 | 1,299,984 |
| Gawio lililolipwa | | | | | | (506,519) | (506,519) |
| **Salio kwa mwaka 31.12.2017** | 6,056,497 | | 124,847 | 66,617 | 157,165 | 1,847,449 | 8,252,575 |
| Mabadiliko ya kanuni za uhasibu la IFRS 9 | | | | | | (324,938) | (324,938) |
| **Salio la mwaka 01.01.2018** | 6,056,497 | # | 124,847 | 66,617 | 157,165 | 1,522,511 | 7,927,637 |
| Rekebisho : | - | | | | | | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha mwaka | - | | | | (50,368) | | (50,368) |
| Toa: Mapato mengine | | | | | (37,104) | - | (37,104) |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | | 5,708 | - | | (5,708) | - |
| Mtaji wa kisheria | | | | (66,617) | | 66,617 | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | | 709,126 | 709,126 |
| Toa: Gawio lililotolewa | - | | | | | (779,990) | (779,990) |
| **Salio kwa mwaka 31.12.2018** | 6,056,497 | # | 130,555 | - | 69,693 | 1,512,556 | 7,769,301 |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Taarifa za fedha zimekaguliwa na Balakrishna sreekmar & Co. na kutoa Hati safi.

***Kuthibitishwa na:***

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Ernest K. Ndimbo* | *Mwenyekiti wa Bodi* | ........................ | *13.06.2019* |
| *Altemius Millinga* | *Mkurugenzi* | ........................ | *13.06.2019* |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018**
Kiwango kwa Tzs.'(000)'

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 TZS | Mwaka Uliopitia 31-Dec-17 TZS |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **969,266** | **1,811,955** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | **-324938.00** | 0.00 |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **128,299** | 128,222 |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | **0.00** | 0.00 |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | **-** | - |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | **0** | 0 |
| | | **772,627** | **1,940,177** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | **-** | - |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | **(63,911)** | (2,298,188) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | **-602,098** | (28,957) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | **(1,116,866)** | (124,161) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | **-** | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | **714,896** | (31,723) |
| | | **(295,352)** | **(542,852)** |
| | - Kodi Iliyolipwa | **(372,171)** | (368,122) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(667,523)** | **(910,974)** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | **0.00** | 0.00 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | **(64,717)** | -143033.00 |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | **0.00** | 0.00 |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | **-** | 0.00 |
| | Mengineyo Amana za kudumu | **-** | 0.00 |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | **0.00** | 0.00 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa*** | **(64,717)** | **(143,033)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | **500,000** | (691,667) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | **(150,000)** | 1,800,000 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | **0.00** | 0.00 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | **0** | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | **(779,990)** | -373118.00 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | **(87,472)** | (135,820) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **(517,462)** | **599,395** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha | **(1,249,702)** | **(454,612)** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | **2,274,275** | 2,728,887 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **1,024,573** | **2,274,275** |

**ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2018**

AINA YA BIDHAA

1. AKAUNTI ZA AKIBA — 2. Mkopo

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | | 2. Mkopo | |
|---|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufungua akaunti | 5000/= | | Mikopo ya biashara | 3% pm |
| Ada ya mwezi | BURE | | Mikopo ya kuboresha nyumba | 1.4% pm |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | | Ada ya Mkopo | 0.01 |
| Kuuliza salio | BURE | | Bima ya mkopo | 0.015 |
| Kufunga akaunti | 5000/= | | Adhabu kuchelewa kurejesha | 2.5% per inst. Arreas |
| Gharama za kuendesha akaunti | 5000/= | | Agricultural Loan | 2.1% - 2.3% pm |
| Gharama za kuweka fedha | BURE | | Mikopo ya kulipia Bima ya afya | 2.3% pm |
| Account maintanance charge | FREE | | | |
| Account maintanance charge | FREE | | | |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, klabu sasa ni wakati wa kutafuta wadhamini

**TAYARI** tumeshuhudia timu zilizoshuka kutoka Ligi Kuu Bara hadi Ligi Daraja la Kwanza kufuatia msimu wa 2018/19 kumalizika tangu Mei 28, mwaka huu.

Katika ligi hiyo iliyojumuisha jumla ya timu 20 kwa mara ya kwanza katika historia ya Ligi Kuu Tanzania Bara, zilizoshuka ni African Lyon ya jijini Dar es Salaam na Stand United ya mkoani Shinyanga.

Aidha, kuelekea msimu mpya wa 2019/2020 unaotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu, timu zilizopanda Ligi Kuu ni Namungo FC ya Ruangwa mkoani Lindi na Polisi Tanzania ya Kilimanjaro.

Hata hivyo, msimu uliomalizika wa 2018/19, ulitawaliwa na changamoto nyingi za ndani ya uwanja zikiwamo waamuzi kuchezesha chini ya kiwango ama kinyume cha sheria 17 za soka na nyingine nyingi.

Kwa upande wa changamoto nje ya uwanja, ukiachilia mbali viporo vya Klabu ya Simba vilivyotokana na kushiriki michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika, tumeshuhudia Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), ikishindwa kuandaa ratiba rafiki kulingana na uchumi wa wanachama wake ambao ni klabu. Lakini kubwa kuliko ni bingwa wa Ligi Kuu, Simba kuishia kukabidhiwa kombe tupu pasipo zawadi yoyote, hali hiyo ikitokana na kukosekana kwa mdhamini mkuu. Hakika ilikuwa ni ligi ngumu si tu kutokana na ratiba ndefu iliyotokana na kushirikisha timu 20, bali changamoto kubwa ilikuwa ni hali ya uchumi kwa klabu shiriki.

Hivyo, wakati huu klabu zikiendelea kujiandaa kwa msimu mpya, hazina budi kujipanga ipasavyo husussan kwa upande wa kujizatiti kiuchumi kwa kutafuta wadhamini wao binafsi badala ya kuitegemea TFF kutafuta mdhamini mkuu.

Ni wazi suala la kutafuta mdhamini wa Ligi Kuu kwa TFF, limeonekana kuwa changamoto kubwa, hivyo klabu zinapaswa kuingia sokoni rasmi kutafuta wadhamini wao binafsi.

Ikumbukwe mdhaminni mkuu wa ligi hapaswi kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa klabu bali ni jukumu kwa kila klabu kujitafutia wadhamini wake mfano wa jezi na vifaa vingine vya michezo, ili kujiimarisha kiuchumi.

Nipashe tunashangaa kuona klabu zikielekeza lawama kwa TFF kufuatia shirikisho hilo kushindwa kupata mdhamini mkuu jambo ambalo zinadai limechangia hali ngumu kwao kiuchumi katika kujiendesha.

Sisi tunakiri ni aibu kwa TFF kushindwa kutoa zawadi kwa bingwa wa Ligi Kuu na kuishia kupewa kombe na medali tu, lakini si kwa klabu njaa zao kuzielekeza TFF kwa kushindwa kupata mdhamini mkuu wa ligi hiyo.

Tunatambua kote duniani klabu hujiendesha kwa kutumia vyanzo vyake binafsi vya mapato na si kwamba hutegemea wadhamini wa shirikisho husika.

Katika hili, pia TFF inapaswa kulaumiwa kwa kupunguza hamasa, msisimko na ushindani kwenye Ligi Kuu kutokana na timu kucheza pasipo kujua bingwa, mshindi wa pili hadi wa tatu ama wa mwisho anazawadiwa nini.

Lakini katika hilo pia, TFF haina budi kuimarisha kitengo chake cha masoko ili kutafuta wadhamini na kutangaza mapema bingwa hadi mburuza mkia atavuna nini kabla ya ligi kuanza.

Ni vema kutambua kuwa ligi iliyo bora haiishii tu kumzawadia bingwa ama mpaka mshindi wa tatu, bali zawadi huanzia kileleni hadi mkiani, na kwa kufanya hivyo huongeza ushindani kwa kuwa kila nafasi ya juu ina kiwango cha kupendeza cha zawadi.

Hilo likifanyika itakuwa vigumu pia kuona hata baadhi ya timu zikihofiwa kupanga matokeo kwenye mechi za mwisho kutokana na kuwania zawadi katika kila nafasi, hivyo ni wakati sasa kwa TFF na klabu kuanza kujipanga mapema kwa kutafuta wadhamini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uingereza ratiba hadharani, TFF isisubiri kabla ya wiki

Na Adam Fungamwango

**KIZURI** huigwa, hata kama kinafanywa na adui yako, au mtu ambaye humkubali. Na kwa Tanzania hatutaki ama tunazembea kujifunza kutoka kwa wenzetu wa nje walioendelea hususan katika sekta ya michezo.

Hasa kwenye nyanja za soka, tunapaswa kuangalia na kufuata mifano na mifumo ya klabu na vyama vikubwa vilivyoendelea barani Ulaya.

Nchini England msimu wa Ligi Kuu 2018/19, ulimalizika Mei mwaka huu, kama ilivyokuwa kwa Ligi Kuu nchini Tanzania. Tofauti ilikuwa ndogo tu kuwa Bongo ilimalizika mwishoni mwa mwezi huo.

Katika hali inayoonyesha kuwa jamaa hao wa England hawana masihara, tayari wameshatoa ratiba yao ya msimu ujao.

Ijumaa ya Agosti 9, mwaka huu, shughuli itaanza upya kwa Liverpool itakapokuwa nyumbani dhidi ya Norwich City.

Jumamosi ya Agosti 10, West Ham itacheza na Manchester City, AFC Bournemouth itapambana na Sheffield United, Barnley itacheza dhidi ya Southamton, Crystal Palace itaanza na Everton, Leicester City dhidi ya Wolverhampton, Watford dhidi ya Brighton, Tottenham itacheza na Aston Villa na Jumapili ya Agosti 11, Newcastle United itakumbana na Arsenal, huku Manchester United ikiiva Chelsea.

Ratiba hii imetoka mwezi mmoja na kitu kabla ya ligi yenyewe kuanza na hata kabla klabu hazijaita wachezaji wao kwa ajili ya kuanza maandalizi ya msimu mpya.

Cha kufurahisha zaidi ni kwamba wameweka mpaka saa za kuanza mechi hizo. Hili na mengine, ndiyo yanayowafanya wenzetu kuwa mbele na kufanya ligi yao ipendwe kiasi cha kufuatiliwa na watu wengi, pamoja na kupata wadhamini kibao.

Hili ni jambo la mfano wa kuigwa kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), ambalo mara nyingi limekuwa likilalamikiwa kwa kushindwa kupanga baadhi ya mipango yake sawasawa. Mara nyingi tumeshuhudia TFF ikishindwa kutoa ratiba kulingana na wakati. Wakati mwingine imekuwa ikitoa ratiba vipande vipande na mambo mengine mengi.

Kwa sasa siwalaumu sana kwa sababu viongozi wao na hata baadhi ya watendaji wakuu watakuwa bize na Afcon, lakini itakapomalizika hakutokuwa tena na hoja ya kujitetea badala yake kujifungia ndani na kutengeneza ratiba.

Tena ratiba yenyewe iwe nzuri itakayozingatia mambo mengi ikiwamo ushiriki wa timu nne kwenye mechi za kimataifa msimu ujao ili kusiwe na utitiri wa viporo, kama vile haitoshi iwe ya usawa na si timu moja kuanza mechi nne mpaka tano nyumbani au ugenini tupu.

Faida ya ratiba kutoka mapema kama kwa wenzetu ni kwamba, tayari kila mmoja anakuwa anajua anakwenda kucheza na nani. Hii inawapa makocha kutengeneza mbinu ya kwenda kumkabili mpinzani wake, kwa sababu kila mmoja anakuwa na aina ya mfumo wa timu anayokwenda kucheza nayo.

TFF si vibaya kuiga hili. Hatutaki kuona hadi timu zinaanza maandalizi ya msimu mpya hazijui ni lini ligi itaanza, achilia mbali ratiba.

Tumechoka kuona ratiba inatolewa kwa kushtukiza, yaani wiki moja au mbili kabla, na kuzifanya timu kukurupuka na kuanza safari kwa zile zinazotakiwa zikacheze mbali ya vituo vyao.

Wakati mwingine kipindi hicho baadhi ya timu zinakuwa nje ya nchi kwa ajili ya maandalizi ya msimu, zinalazimika kukatisha na kurejea haraka.

Ratiba za aina hiyo za Kibongo zinakuwa haziwapi makocha wakati muafaka wa kuwaandaa wachezaji wao kwa mfumo ambao itakwenda kucheza na timu pinzani.

Mfano, Polisi Tanzania inapangiwa na Yanga, ratiba inatoka wiki moja kabla, kocha hatoweza kuwatengeneza wachezaji kukabiliana na timu hiyo, pia Namungo ukiishtukiza kucheza na Simba wiki moja kabla, huku kocha wao akiwa bado hajaweka mfumo wa kuizuia timu hiyo ni matatizo matupu.

Ratiba ikitoka mapema na kuwa nzuri inasababisha vitu vingi kwenda kama invyotakiwa, kila mmoja akitimiza majukumu yake na hata TFF yenyewe itakwepa zile lawama inazotupiwa ambapo wakati mwingine si za kwao, lakini zingine ni za kujitakia wenyewe.

MJADALA

# Tusiwadekeze wachezaji wavivu wa Kibongo

**Na Adam Fungamwango**

AKIWA kwenye hafla ya kuichangia Klabu ya Yanga, Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema anataka msimu ujao klabu hata kama zitasajili idadi kubwa ya wachezaji wa kigeni, lakini watakaocheza uwanjani kwa wakati mmoja wawe watano tu.

Na akasisitiza kuwa hilo atalisimamia. Lengo la waziri ni nzuri tu, kwa sababu anataka wachezaji wa Kitanzania wengi wapate nafasi ya kucheza kwa ajili ya kuiwezesha timu ya taifa kupata wachezaji wazuri zaidi siku za usoni.

Hata hivyo, suala hili inabidi kuwe na uwanja mpana zaidi wa kuliangalia hili kuanzia serikalini hadi kwenye Shirikisho la Soka nchini (TFF).

Hakuna Mtanzania yeyote ambaye hataki kuwa na wachezaji wazuri wenye uwezo wa juu, lakini pia hakuna anayetaka kuona timu ya Taifa Stars inakuwa dhaifu dhidi ya mataifa mengine.

Lakini kuna vitu vingi vya kufanya Stars iwe bora na wachezaji wenye uwezo mzuri zaidi, lakini sidhani kama hili linaweza kutusaidia sana.

Kwangu mimi binafsi sioni kama kuna tatizo kubwa kwa wachezaji 10 wa kigeni kucheza kwenye kikosi kimoja wote wakiwa uwanjani.

Binafsi, sioni kama wachezaji hao wanazuia kitu chochote, ikiwamo wachezaji wa Kitanzania kutoonekana, zaidi ya kuwafanya wachezaji wa Kibongo kujituma zaidi.

Kuwawekea wachezaji wa kigeni idadi ya kucheza uwanjani ni kuzuia klabu au makocha kuchezesha wachezaji ambao wanaona wataipa timu ushindi na kumlazimisha kuchezesha wachezaji ambao huenda hawana uwezo, ili mradi tu kwa sababu ni Watanzania.

Kuna hadithi moja ya baba mmoja aliyekuwa na mtoto wake ambaye ni mvivu wa kula na kwa sababu anaishi kwa watoto wa mdogo wake nyumbani kwake alichoona yeye ni kumtengea sahani yake ili awe anakula peke yake. Ikawa ndiyo maisha yake, wenzake wanakula kivyao na yeye pepe yake kwa kuhofia wenzake watampunja kutokana na kasi yao na matonge yao makubwa.

Rafiki yake mmoja alimtembelea na alipoona ile hali na kuelezwa, alimshauri kuwa hatatui tatizo, bali anachotakiwa kufanya ni kumjumuisha na wenzake kwa muda wa wiki moja, bila ya kumpa chakula cha ziada.

Baba yule alifanya kama alivyoagizwa, na mtoto wake baada ya wiki moja alianza kuzoea na yeye kula kwa kasi na matonge makubwa baada ya siku tatu za mwanzo kushindwa kuendana na kasi ya ndugu zake na hakuwa akipewa chakula zaidi ya kulala akiwa hajashiba vizuri.

Alichokifanya alijipanga na yeye awe kama wao. Na kweli, baada ya wiki mbili akawa mahiri zaidi kwenye msosi kushinda hata baadhi ya ndugu zake.

Hata huku kwenye soka, tusiweke kanuni za kuwadekeza wachezaji wa Kitanzania ambao wengi wao hawajitumi, hawajitambui, mara kwa mara tunakutana nao kwenye klabu za pombe usiku wa manane, huku keshokutwa wakiwa wana mechi ya Ligi Kuu.

Mchezaji kama huyu ambaye hajitambui, huku kukiwa na mastaa wa kigeni ambao wao soka wanalifanya kama kazi, ukimwekea kanuni hii ya kumlinda na kuona kuwa ni lazima tu acheze hata iweje, si itakuwa balaa?

Kinachotakiwa kufanyika ni kuwaacha wenyewe wagombee namba na wageni. Sidhani kama kuna mchezaji wa Kitanzania ambaye ana uwezo wa hali juu, anaweza kuwekwa nje na kocha yeyote yule eti kwa sababu kuna mchezaji wa kigeni.

John Bocco amekuwa na kiwango kizuri na licha ya kuwa na wachezaji wa kigeni amekuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Simba. Huyu hachezi kwa hisani ya kanuni.

Shomari Kapombe amekuwa majeruhi kwa kipindi kirefu, lakini pamoja na kuja kwa wachezaji wa kigeni, kina Nicolaus Gyan na Zana Coulibaly, lakini hakuna hata mmoja aliyeweza kufikia kiwango chake. Hawa ndiyo wachezaji wanaotakiwa wacheze kwa viwango vyao na si kwa sababu tu wanatakiwa wachezaji watano uwanjani.

Kuna dhana kuwa wachezaji wetu watakosa nafasi kwenye kikosi cha Taifa Stars. Lakini ukiiangalia dhana hii unagundua kuwa tunaziangalia zaidi Klabu za Simba, Yanga na Azam FC tu basi. Hizi ndizo timu zinazosajili wachezaji 10 wa kigeni. Zingine zinasajili pungufu na zingine hazisajili kabisa.

Si lazima mchezaji wa Taifa Stars atoke Simba, Yanga au Azam FC. Kuna timu kama Mtibwa Sugar, Lipuli FC, JKT Tanzania, Coastal Union, Prisons na nyingine nyingi ambazo huwa hazisajili wachezaji wa kigeni na wachezaji wao wanacheza wao msimu mzima, hizi hazitoshi kutoa wachezaji wa timu ya taifa kama wanafanya vizuri?

Halafu cha ajabu ni kwamba pamoja na kuwa na wachezaji wa Kitanzania ambao wanapata nafasi mechi zote, lakini ni Lipuli tu ndiyo ina wachezaji timu ya taifa, zingine hazina hata mmoja.

Na hizi tunazoziangalia sana na kuona kuwa zinasajili wachezaji wengi wa kigeni wanaowabana wachezaji wa Kitanzania wasionekane, ndizo zina wachezaji wengi kwenye kikosi cha Stars.

Hapa naona tuache tu sanaa ya soka iende kama inavyotakiwa. Tuwaache wachezaji wenye uwezo wacheze iwe wa Kitanzania au wa kigeni na tusiwapangie makocha au mashabiki nini cha kwenda kuangalia. Tunaweza kufukuza mashabiki uwanjani na kuanza kulia kuwa wamepungua viwanjani.

Mashabiki wanataka vitu vilivyo bora, wanataka kuangalia wachezaji bora wanaojitambua na kujituma wawe Watanzania au kutoka nje, lakini tukiwapangia wanaweza kuacha kwenda kuangalia soka.

Inawezekana kabisa kuwa hata Tanzania kwenda Afcon mwaka huu ni kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wachezaji wa kigeni nchini ambayo imewafanya baadhi ya wachezaji wa ndani kupambana nao kwa dhati, hivyo kuboresha viwango vyao.

Nadhani kuna vitu vya kuangalia kama vile kuwa na viwanja vingi nchini, kila klabu iwe na timu za vijana U-23, U-20 na U-17. Kuhamasisha wachezaji wa Kitanzania kwenda nje ya nchi ili ifike wakati tukiita Stars basi hata klabu za Simba, Yanga na Azam tunazoziangalia sana ziwe na mchezaji mmoja mmoja, wawili au watatu tu, lakini wengine watoke nje ya nchi.

Hii ndiyo njia bora ya kuifanya Tanzania iinuke kisoka na si kuwatengenezea kanuni wachezaji wa Kitanzania wa sasa ambao baadhi yao ni wavivu hata wa mazoezi na starehe nyingi ili wawe wanacheza hata kama uwezo hawana, tunaweza kuanza kurudi tena nyuma kisoka.




Rais wa TFF, Wallace Karia

KABWELA NA FADHIL MOHAMMED





## CHALLENGING SALES POSITIONS IN LAKE OIL GROUP

LAKE OIL

## VACANCY: ZONAL MANAGERS ACROSS TANZANIA

**Job Title:** Zonal Manager

**About the position:**
Lake Group is looking for experiences Retail Sales personnel for their Fuel Division to be positioned across Tanzania.

They will be allotted Zones which would have a set number of Retail Outlets, which have to be regularly visited, Sales & Service Performances monitored and ensure Sales Targets Achieved.

Your role will involve the ability to effectively monitor stocks & Sales at Retails Outlets, and ensure that orders are generated sufficiently early to ensure no Stock-Out of Fuel at Stations.

You will be also responsible for ensuring high quality Customer Service at all Stations in addition to ensuring correct quality, quantity and various other facilities required by all types of motorists.

To develop and build customer base in his/her Zone including expanding the Retail Network and maintaining good relationships.

You will also be responsible for all Company Assets placed at all Fuel Stations in your Zone and also propose with justification for additional facilities like Storage Tanks, Dispensing Units etc for equipping the station so as to enable to achieve the Sales Targets.

**Remuneration**
Remuneration will be based on experience & market related.

**Key Responsible Areas**

**Sales:**
1. Monitor Sales at Retail Stations and support by canvassing for new customers and maintaining the existing ones.
2. Ensure no Stock outs in any Fuel Stations by indenting in time and following up with S & D for deliveries to the stations.
3. Ensure proper working of all equipment's and confirm all stations work as per TRA and other Statutory norms.
4. Ability to meet Monthly Station wise Targets consistently.

**Customer Service excellence**
1. Ensure motorists coming to our Fuel Stations are treated to excellent service and good quality & quantity Fuel.
2. Minimization & speedy resolution of any complaints

**Competencies**
Applicant should be literate/minimum computer knowledge and should have Sales Experience in Fuel or Fuel related or FMCG Products and have Field experience and ready to do extensive travelling:

1. A Graduate from any recognized University.
2. Minimum Experience of 5 years in any Retail FMCG Industry or 3 years in Fuel & Fuel related Industry.
3. Knowledge of English would be an advantage.

**Competencies**
Interested Candidates may make an Application in their own handwriting together with their CV and send it to :hr@lakeoilgroup.com

**Application can send to below Addressed**

**Lake Oil Limited**
**P.O.Box : 5055 Plot No.46,**
**Vijibweni Industrial Area, Kigamboni**
**Dar Es Salaam -Tanzania**

215278101

# Serikali yaingilia kati fidia nyumba 4,000 Dar

INATOKA UK. 3

kupoteza haki yao na kusisitiza kuwa serikali ya awamu ya tano haiko tayari kuona wananchi wanapata tabu kufuatilia haki zao na kuiagiza kampuni hiyo kuwaeleza wamiliki itawalipa lini kiasi kilichobaki ili kuondoa mkanganyiko.

Mabula alisema, atamuagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Dar es Salaam kuzungumza na wananchi wanaouza nyumba kwa kampuni hiyo, na yeye atazungumza na wakazi hao wa Vingunguti kuhusiana na sakata hilo.

Mkurugenzi wa Fedha na Utumishi wa Kampuni ya PMM 2001 LTD, Damian Kanuti, alijitetea kwa kueleza kuwa kampuni yake ilishindwa kutekeleza makubaliano ya ununuzi wa nyumba katika mitaa ya Vingunguti kutokana na kuchelewa kupata mkopo ilioutarajiwa kutoka Benki ya TIB na kubainisha kuwa lakini kampuni ilishalipa kiasi cha bilioni 1.7 ikiwa ni malipo ya nyumba 80 na fedha ya awali kwa wamiliki 17.

Mwenyekiti wa kamati ya kusimamia uuzaji nyumba 4,000 katika eneo la Vingunguti, Ramadhani Pepo, alililamikia kampuni ya PMM 2001 Ltd kwa kutoonyesha ushirikiano kwa kamati wakati wa zoezi hilo, hivyo kufikisha malalamiko kwa Mbunge Kamoli pamoja na Mabula kwa lengo la kupatiwa ufumbuzi.

Pepo alisema, kutokana na Kampuni ya PMM 2001 Ltd kushindwa kutekeleza makubaliano yaliyokuwa yatekelezwe Septemba 2018, wamechoka kufuatilia suala hilo na wanachotaka ni kulipwa fedha za awali kukamilishiwa kiasi kilichobaki.

Mbunge Kamoli ameliitaka kampuni ya PMM 2001 Ltd kueleza bayana kiasi cha fedha kilichobaki kwa wamiliki wa nyumba 17 zitakazolipwa lakini, Kanuti alishindwa kutoa jibu na kutaka kampuni yake kupewa muda wa kulifanyia kazi.

# Utafiti wafichua siri uzazi mpango, maambukizi VVU

INATOKA UK. 3

za sindano, kitanzi na kipandikizi.

Alisema utafiti huo ulifanyika baada ya kuwapo kwa wasiwasi mkubwa wa kupata VVU kwa wanawake wanaotumia njia hizo za uzazi wa mpango kwa miaka mingi.

"Kwa muda mrefu kuna watu walikuwa wanahisi na kuuliza maswali kwamba labda kuna uhusiano baina ya kutumia njia za uzazi wa mpango na kuongezeka kwa hatari ya kupata VVU, kwa hiyo ilibidi jopo la watafiti kutoka katika nchi mbalimbali duniani wafanye utafiti huo, na waliamua kufanya kwa nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa sababu maambukizi yalikuwa juu katika nchi hizo na waliangalia katika njia za uzazi wa mpango za kitanzi, sindano na kipandikizi," alisema Dk. Mwakyosi.

Aliongeza: "Na waliangalia kwa wanawake walio katika uwezekano wa kupata ujauzito kuanzia miaka 16 hadi 30." Kuhusiana na kundi la watu ambao wanaongoza kwa maambukizi mapya ya VVU, Dk. Mwakyosi alisema katika utafiti huo, imebainika kuwa wanawake ndiyo wanaongoza kwa kupata maambukizi hayo japokuwa maambukizi wanayopata hayahusiano na matumizi hayo ya matumizi ya njia za uzazi wa mpango.

"Kundi la wanawake ndiyo linapata maambukizi mapya ya VVU kuliko kundi jingine kwa sababu katika utafiti huo inaonyesha kuwa hata katika kundi la watu 100 nusu ya watu wanaofanyiwa utafiti, nusu ya hao waathirika ni wanawake ingawa maambukizi haya hayahusiani k abisa na matumizi ya njia za uzazi wa mpango," alisema Dk. Mwakyosi.

Aliongeza: "Na ndiyo maana tunashauri kwamba kuna haja ya kuendelea kubuni njia mbalimbali za kuzuia maambukizi haya na siyo kwa kutegemea kondomu pekee, hatutakiwi kupuuza na kuona maambukizi haya yakiendelea kwa wanawake."

# Zitto ataka bei elekezi ya taulo za kike

INATOKA UK. 2

kuendelea: "Kwa ujumla watu ni asilimia 17.3 yaani bajeti ya ndege ni bilioni 500 na afya bilioni 500."

**WAFANYABIASHARA**

Akizungumzia sekta binafsi, kiongozi huyo alidai serikali imekuwa hairejeshi kodi ya VAT (TAX Refund) kwa wafanyabiashara, hivyo kuwafanya wafanyabiashara kushindwa kuzimudu biashara zao, ikiwamo kushindwa kulipa madeni waliyokopeshwa na kushindwa kulipa wafanyakazi wao.

**WAFANYAKAZI**

Kuhusu wafanyakazi, Zitto alilalamikia kodi katika mishahara ya wafanyakazi akidai ni eneo ambalo lilitakiwa kuangaliwa katika bajeti kwa kupunguza kodi katika mishahara yao sambamba na kupunguza michango inayolipwa na wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi za jamii.

# Ubakaji watoto watisha

INATOKA UK. 2

kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, Mkurugenzi wa Miradi ya SOS Zanzibar, Asha Salim Ali, alisema licha ya serikali kuwa na sheria mbalimbali, sera na mipango ya kuwalinda watoto dhidi ya aina zote za udhalilishaji, bado vitendo hivyo vinaendelea kutokea ikiwamo kubakwa na kulawitiwa.

Aidha, alisema licha ya Zanzibar kutekeleza mpango wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, bado inakabiliwa na kiwango cha juu cha udhalilishaji ikiwamo utelekezwaji wa familia, ndoa za ututoni, ukatili wa kingono, na wa kimwili pamoja na watoto kubakwa na kulawitiwa.

Kwa upande wake Meneja Mradi wa Huduma za Simu kwa Mtoto Zanzibar, Fatma Ahmada, alisema lengo kuu la maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ni kuwakumbusha viongozi wa serikali na jamii kwamba maendeleo ya taifa hayawezi kupiga hatua bila ya kuwasaidia watoto katika kupata mahitaji yao muhimu.

Alisema bado kuna kundi kubwa la watoto wanaohitaji msaada ikiwamo watoto maskini na wenye mahitaji maalum.

Naye Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akiwa mjini Geita, amewataka wakuu wa mikoa ambayo haijaanzisha mabaraza ya watoto kuanzisha haraka pamoja na madawati ya ulinzi wa mtoto shuleni.

Akiwa katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, kimkoa mkoani Geita jana, alitaka kila mkoa uhakikishe unaanzisha haraka mabaraza ya watoto pamoja na madawati ya kulinda watoto shuleni, ili kuhakikisha matukio ya ukatili wa watoto yanatokomezwa kabisa.

Alisema lengo kuu la maadhiAlisema takwimu za utafiti wa afya za mwaka 2015/2016 zinaonyesha kuwapo kwa ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto hapa nchini hususani wasichana kiwango cha kitaifa, ndoa za ututoni asilimia 37, mimba za ututoni asilmia 27 na ukeketaji wasichana asilimia 10.

Aidha, alisema takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2018 zinaonyesha kuwapo kwa matukio 14,419 ya ukatili yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi nchini ikilinganishwa na matukio 13,457 kwa mwaka 2017 ambalo ni sawa na ongezeko la matukio 1,034, asilimia 7.7.

Pia ameongeza kuwa mikoa mitano inayongoza kwa matukio ya ukatili nchini ni Tanga (1,039), Mbeya (1,001), Mwanza (809), Arusha (792), Tabora (616) na kwamba matukio yanayoongoza ni ubakaji, ulawiti pamoja na kusema kuwa takwimu hizo zinaonyesha kuwa mapambano bado yapo katika kutetea haki za watoto. Naibu Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Plan International, Benatus Sambili, alisema shirika hilo linajishughulisha na utetezi wa haki za watoto ambalo linafanyakazi katika mikoa 13 nchini katika kuhakikisha ustawi na upatikanaji wa haki za msingi za watoto hasa wa kike tangu mwaka 1991 katika maeneo ya elimu, afya ya uzazi wa mama na mtoto pamoja na usafi wa mazingira, uwezeshaji vijana kiuchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel Luhumbi, amesema kuwa viongozi pamoja na jamii wana jukumu kubwa la kuhakikisha watoto wanalindwa na kusimamia haki zao na hivyo kuitaka jamii kutowatenga watoto wa kike kwa kuwa wote wana haki kupata elimu.

***Imeandaliwa na Salome Kitomari, Dar es Salaam, Rahma Suleiman, Zanzibar na Alphonce Kabilondo, Geita**

**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku

215227501



# Neema ya soko la uhakika wakulima wa mboga Tanga

**Na Dege Masoli,** TANGA

WAKULIMA wa mboga na matunda Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, wamepata fursa ya kipekee ya soko la uhakika la kuuza mazao yao kwa fedha taslimu kutoka shambani pamoja na kupata mikopo ya pembejeo, mbegu na mitaji yenye masharti nafuu.

Fursa hizo kwa wakulima zimetolewa na Kampuni ya MacLeans BeneCIBO yenye makazi yake Kigamboni jijini Dar es Salaam ambayo imefungua tawi lake wilayani Lushoto ili kuwahudumia kwa karibu wakulima wa mboga na matunda wilayani humo.

Kampuni ya MacLeans BeneCIBO inajishughulisha na kusambaza vyakula kwenye makazi ya watu, ofisini, hotelini na kwenye vyombo vya usafiri vya nchi kavu, angani na majini kwa kuzingatia ubora uliokubalika kimataifa kwa gharama nafuu, kuzingatia afya na kutunza virutubisho vya asili. Aidha, kampuni hiyo ina programu maalumu za kuwaendeleza wakulima ili waweze kufanya kilimo chenye tija.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa tawi lao jipya wilayani Lushoto katika kijiji cha Mnadani kata ya Malindi, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Nnala Mwakanyamale, alisema lengo la kumfuata mkulima shambani ni kuhakikisha kuwa anafaidika moja kwa moja na kazi yake na kumwondolea hasara alizokuwa anazipata zilizotokana na uharibifu wa mazao, gharama za usafiri, kukandamizwa na madalali na uhaba wa masoko.

Mwakanyamale alisema kampuni hiyo imekuwa inadhamini vikundi vya wakulima kupata mikopo ya kilimo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB), ambapo imewezesha wakulima kupata mkopo wa jumla ya Sh. 119 milioni kutoka benki hiyo.

Aidha, MacLeans BeneCIBO inafanya utaratibu na Taasisi za Mikopo kutoa mikopo ya kujikimu wakati wa msimu wa kilimo.

"Tayari tumeingia makubaliano na kampuni ya mikopo ya Kopafasta ambayo itawakopesha wakulima fedha, pembejeo na mbegu na sisi tutachukua jukumu la kuwadhamini na kuwalipia riba ili wao warejeshe kiasi kilekile walichokopa," Mwakanyamale aliongeza.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Lushoto, Emmanuel Vuli, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya hiyo katika uzinduzi huo, January Lugangika alisema kuwa wameipokea na wanaiunga mkono kampuni ya MacLeans BeneCIBO kwani kwa uwekezaji wao italeta mapinduzi ya kilimo cha mboga na matunda na kukipa thamani kinayostahili katika kuhuisha uchumi wa viwanda.

Aidha, aliwataka wakulima kuhakikisha wanalima kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu ili kutoa mazao yenye ubora utakaokubalika kwenye masoko ya kimataifa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Lushoto, Lucas Shemdolwa, alieleza kuwa wakulima wa vijiji vya eneo hilo walikuwa wamekata tamaa kutokana na changamoto kubwa ikiwa ni pamoja na mazao kuharibika kwa kukosa soko na matunzo pamoja na madalali walionunua kwao kwa bei kandamizi.

Aliahidi kuwa halmashauri hiyo itashirikiana na kampuni hiyo katika kuhakikisha wanatimiza lengo walilokubaliana kwa ufanisi na kuinua kipato cha wakulima.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima wa vijiji vya Wilaya ya Lushoto, Mwenyekiti wa Kikundi cha Wakulima wa mboga na matunda cha MAVUMO - AMCOS, Maliki Amili Shekidele, aliishukuru kampuni hiyo na serikali kwani wameanza kufaidika na mikopo; na wana uhakika wa maendeleo ya kiuchumi yatakayotokana na mazao yao.



Viongozi wa vikundi vya wakulima, ofisa kilimo Kata ya Malindi wilayani Lushoto, mkoani Tanga, na baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya MacLeans BeneCIBO walipotembelea shamba la mkulima wa mboga na matunda wa kijiji cha Mnadi. **PICHA: DEGE MASOLI**

# NEMC yatambua michango ya wadau katazo la mifuko plastiki

**Na Enock Charles**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEM), limeshukuru taasisi na mamlaka zote ambazo zimesimama imara na kufanikisha zoezi la kuondoa mifuko ya plastiki nchini.

Akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, ameishukuru kipekee Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutoka ngazi ya kata mpaka taifa na kueleza kazi ya wizari hiyo imezaa usimamizi mzuri na umekuwapo utekelezaji mzuri wa katazo hilo pasipo kuliletea taifa fedheha.

"Tunazishukuru taasisi zote na kwa kipekee kabisa ni wenzetu wa TAMISEMI kwa namna walivyolipokea katazo hili, wakalibeba na kulisimamia kikamilifu katika maeneo yao kuanzia ngazi za chini za kiongozi mpaka taifa," alisema.

Dk. Gwamaka alisema kuwa, licha ya mafanikio hayo bado zipo changamoto chache na kutaja moja kuwa ni kwamba kuna viwanda vinavyozalisha mifuko batili. Ameomba ushirikiano kutoka kwa wadau, hasa TAMISEMI, katika kusaka viwanda hivyo ili wamiliki wachukuliwe hatua za kisheria.

Zoezi la kusaka wamiliki wa viwanda hivyo limeanza jijini Dar es Salaam Alhamisi wiki hii.

Aidha, Mkurugenzi huyo amesema kuwa mazingira ni suala mtambuka hivyo ni vyema kila mtu akashiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha utekelezaji wa katazo hilo ili kuyafanya mazingira Tanzania yawe rafiki kwa kizazi cha leo na kesho. "Mazingira ni suala muhimu kwa kila Mtanzania, hivyo tunalojukumu la kuhakikisha watu wote wanaohujumu zoezi hili wanabainishwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria kwani viwanda bubu vipo huko mitaani ambako jamii kubwa inaishi," alisisitiza Dk. Gwamaka.

"Zoezi hili la kuvibaini viwanda vinavyoendelea kuzalisha mifuko ya plastiki linaweza kufanikiwa sana iwapo viongozi wa serikali za mitaa, kata, wilaya na mikoa watashirikiana vyema na maofisa wa NEMC ambao watakuwa wanapita huko mitaani," alisema Dk. Gwamaka na kuongeza.

# Mawakala Tigo wavuna mamilioni

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya mawakala 2,000 wa huduma ya Tigo Pesa, wamejishindia zawadi za fedha taslimu zaidi ya shilingi milioni 160 kwenye promosheni ya mwezi mmoja inayojulikana kama 'Wakala Cash In Promotion'.

Promosheni hiyo ya nchi nzima iliyozinduliwa Mei mwaka huu, ililenga kuwahimiza mawakala wa Tigo Pesa nchini kufanya miamala kwa wingi ili kuweza kujishindia zawadi za fedha taslimu.

Akiwakabidhi zawadi washindi wa promosheni hiyo, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, alisema kampuni ya Tigo inathamini juhudi kubwa zinazofanywa na mawakala na kuongeza kuwa promosheni hiyo ililenga kuwazawadia mawakala kutokana na kazi nzuri wanayoifanya.

"Kampeni hii siyo tu inaonyesha dhamira yetu ya kuwekeza kwenye biashara, lakini pia azima yetu ya kugawana tunachokipata kutokana na biashara tunayofanya pamoja na wadau wetu. Promosheni hii ni fursa nyingine ya kuwazawadia mawakala wetu fedha taslimu na bonasi ambazo tunawaamini zitawapa moyo wa kufanya kazi kwa bidii zaidi ili kuendelea kufikisha huduma jumuifu za kifedha kwa wananchi wengi zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Pesha, pamoja na washindi wengine, washindi wawili wakubwa kutoka kila kanda walipatikana ambao ni Suleiman Hussein na Vicky Ibrahim kutoka Kanda ya Pwani, Peter Myovela na Stivin Katoto kutoka kanda ya Kusini, Anton Masawe na Athuman Mbwana kutoka kanda ya Kaskazini pamoja na Harry Lwila na Joseph Kabeba kutoka Kanda ya Ziwa.

"Pamoja na washindi 2,000 ambao wamejinyakulia zawadi mbalimbali za fedha taslimu kutokana na juhudi zao, tumepata washindi wengine wawili wakubwa kutoka katika kila kanda ambao kwa jumla wao ni 8 ambao wameweza kujishindia shilingi milioni 12 zaidi kutokana na jitihada zao. Tunawapongeza sana mawakala wote ambao wamefanya vizuri na kujishindia zawadi na kwa wale ambao hawakuweza kushinda waongeze bidii ili waweze kuwa washindi katika promosheni zijazo," alisema.

Akipokea zawadi ya shilingi milioni 3.5, Suleiman Hussein ambaye ni wakala kutoka Kanda ya Pwani, alisema: "Napenda kuishukuru sana kampuni ya Tigo. Promosheni hii inaonyesha ni kwa kiasi gani sisi mawakala ni kiungo muhimu kwenye huduma nzima ya Tigo Pesa. Kuibuka mshindi kwenye promosheni hii ni rahisi sana kwa kuwa unahitajika kufanya kazi kwa bidii tu. Nawashauri mawakala wenzangu wafanye kazi kwa bidi kwani Tigo Pesa inalipa."

Vicky Ibrahim, wakala aliyejishindia shilingi milioni 2.5 alisema amefurahi kuwa mshindi wa zawadi hiyo na kuwataka wanawake kuwa mawakala wa Tigo Pesa na wale ambao tayari ni mawakala kuwekeza zaidi na kufanya kazi kwa bidii.

# Matukio ubakaji watoto yashika kasi

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), kimeungana na taasisi nyingine kusherehekea Siku ya Mtoto wa Afrika, huku takwimu zikionyesha matukio ya ubakaji yanashika kasi.

Aidha, Tamwa imeiomba serikali na wadau wengine wa masuala ya haki za watoto waendelee kupaza sauti zao ili kuhakikisha ukatili huu unapungua na ikiwezekana unamalizika kabisa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tamwa, Rose Reuben, matukio ya ubakaji wa watoto ni tishio kwa usalama wao, ukuaji wao kwa ujumla na maendeleo endelevu ya taifa.

Alisema takwimu zilizotolewa hivi karibuni na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), zinaonyesha kuwa katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo wa mwaka 2018 watoto 2,365 walibakwa, idadi ambayo ni sawa na watoto 394 kwa siku.

Aidha, alisema ripoti ya hali ya uhalifu kwa mwaka 2017 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya

Takwimu (NBS) inaonyesha katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2017, matukio ya uhalifu dhidi ya watoto yalikuwa 13,457.

Pia kwa mwaka 2016 matukio hayo yalikuwa 10,551, na kwamba kati ya hayo, matukio ya ubakaji yalikuwa 2,984.

"Mtoto ni taifa la kesho, endapo atafanyiwa ukatili leo, je, kesho taifa hili litaongozwa na nani? Tamwa tunasisitiza hatua kali za kisheria na mabadiliko mengine ya kisera ili kumlinda mtoto dhidi ya ukatili," alisema Reuben.

Aliwasihi wazazi, walezi kulipa uzito mkubwa suala la ulinzi wa mtoto ili kuepusha ubakaji .

Aidha, alisema ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia watoto (Unicef) inaonyesha kuwa wabakaji wengi ni ndugu wa karibu ambao wanaishi ndani ya familia.

"Kupinga unyanyasaji, ubakaji na ulawiti wa watoto ni jukumu la jamii nzima na wakati umefika sasa kila mmoja kwenye nafasi yake awalinde watoto kwa kuripoti vitendo vya unyanyasaji vilivyofichika kwenye jamii yetu," alisisitiza.

Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika hufanyika kila Juni 16, na kauli mbiu ya mbiu ya mwaka huu ni "Mtoto ni msingi wa taifa endelevu tumtunze, tumlinde na kumwendeleza".



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa (kulia), bungeni jijini Dodoma mwishoni mwa wiki baada ya Waziri wa Fedha, Dk. Philip Mpango (kushoto), kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/20. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali, wafanyabiashara watakiwa kuchangamkia fursa

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa uwezeshaji wa wafanyabiashara Afrika (AECF) umewaomba wajasiriamali na wafanyabiashara wa Tanzania kuchangamkia fursa za uwekezaji, ili kuongeza ajira kwa idadi ya watu na kusaidiana na serikali kukuza zaidi uchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa wadau wa uwekezaji kutoka katika mabara ya Amerika, Ulaya na Afrika jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa AECF Tanzania, Gerald David, alisema sekta binafsi ndiyo inatoa ajira nyingi , hivyo lazima kuongeza nguvu katika sekta hiyo kuhakikisha inatoa huduma kwa idadi kubwa ya watu mijini na vijijini na kuongeza zaidi ajira.

Alisema upo umuhimu kwa wawekezaji kupanua zaidi wigo wa uwekezaji husussan katika maeneo ya kilimo, nishati na maeneo mengine ambayo yanasaidia kutoa huduma za moja kwa moja kwa wananchi kuanzia wa hali ya chini.

"Tunaona kwamba nchi za Afrika zimekuwa zikitumia bidhaa nyingi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi hizo, wakati kuna uwezo mkubwa wa kuzalisha chakula cha kukidhi mahitaji yote, ilhali tuna vyanzo vingi ikiwamo nishati mbadala za kukidhi mahitaji na ambazo ni nzuri kwa kukidhi mazingira, tutumie fursa hizi hizi kunufaika wenyewe," alisema David na kuongeza:

"Sisi kama AECF ambao ni wadau muhimu katika sekta ya uwekezaji hususani katika nchi za bara la Afrika, tumeamua kushirikiana na serikali ya Tanzania kwa kuiunga mkono hasa kipindi hiki inapoimarisha na kujenga uchumi wake kupitia viwanda. Tunataka wajasiriamali na wafanyabiashara watumie fursa hii kuwekeza katika kilimo pamoja na rasilimali zote zilizopo Tanzania," alisema David.

Aliongeza: "Kama ni katika kilimo tuone." Alisema AECF imeanza kuwawezesha wakulima na wanaowekeza katika nishati mbadala na kwa Tanzania pekee imetoa Dola za Marekeni milioni 60 sawa na Shilingi bilioni 1.38 kwa ajili ya kuwezesha kampuni 71, na zaidi ya watu milioni 1.7 wamenufaika na msaada huo.

Mjasiriamali, Fahad Awadh ambaye ni mfanyabiashara wa korosho kutoka Zanzibar, alisema tatizo kubwa linalochangia watu wengi kuagiza bidhaa kutoka nje ya Tanzania ni kutokana wafanyabiashara wengi wa ndani kushindwa kuongeza thamani katika bidhaa zao ili kuziweka katika hali ya mvuto.

## Wadau wa kilimo wampa 5 JPM TADB mikoani

**Na Mwandisho Wetu**

WADAU wa kilimo wamepongeza pendekezo la Rais John Magufuli la kutaka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kuwa na matawi mikoani ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo na huduma nyingine za benki hiyo.

Rais alitoa pendekezo hilo alipokutana na wafanyabiashara kutoka nchi nzima Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Wadau wamesifu pendekezo la rais kwa kusema benki hiyo ikiwa karibu na wateja wake na kutoa mikopo kwa wakati, jambo hilo litachochea kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi hapa nchini. Wamesema TADB ipo katika nafasi nzuri ya kuchagiza maendeleo na ukuaji wa sekta ya kilimo jambo ambalo linahimizwa sana na Rais.

Akihojiwa juu ya maoni ya wadau wa benki yake, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, amesema benki inayafanyia kazi kimkakati maelekezo ya Rais na kufafanua kwamba tayari ofisi zimefunguliwa katika baadhi ya mikoa. Ameeleza kwamba tayari ofisi zimefunguliwa katika mji wa Kigoma na majiji ya Mwanza na Dodoma.

Ofisi ya Mwanza, ameeleza, ilifunguliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Machi 19, mwaka huu na inahudumia mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga, Simiyu, Geita na Kagera.

Maandalizi ya mwisho yanafanywa kufungua ofisi katika Jiji la Mbeya, ameeleza kiongozi huyo, na kufafanua kwamba ofisi hiyo itahudumia mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, na Ruvuma.

Ofisi ya Dodoma, amaeleza, imefunguliwa toka mwaka jana na ofisi ya Kigoma imekuwa ikihudumia wakulima kwa miezi tisa iliyopita.

"Tunafarijika wadau wanapoeleza uhitaji wa huduma zetu na kutambua kazi yetu. Agizo la Rais linaimarisha dhamira yetu ya kuwa karibu na wananchi na linatupa hamasa ya kufungua ofisi mpya za kongani ili kuhudumia wateja wetu," alisema Justine.

"Kama ulimsikiliza vizuri, Rais Magufuli ameonyesha kuguswa na utendaji kazi wa Benki ya Kilimo na ndiyo sababu anapenda ifungue matawi mikoani ili kusaidia serikali kuharakisha azima yake ya kujenga uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo 2025. Ujenzi wa viwanda msingi wake mkuu ni kilimo, mifugo na uvuvi," alisema Anangisye Mwakalindile, mkulima wa parachichi wa Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya. Mwakalindile alikumbusha pia kwamba wakati akiwa katika ziara mkoani Mbeya, Rais Magufuli aliwaasa wakulima kuchangamkia fursa ya mikopo inayotolewa na Benki ya Kilimo ili kukuza mitaji na kuinua kilimo nchini.

Samson Maduhu, mkulima wa pamba, Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza, alisema TADB ikiwa na matawi mikoani wakulima watanufaika na mikopo kwa kuongeza tija katika kilimo.

"Mimi nipo kwenye nafasi nzuri ya kuelezea umuhimu na faida ya kuwapo kwa benki hii kwani katika kipindi kifupi wakulima wengi wa pamba tumenufaika na huduma za benki hiyo kwa kupata pembejeo mbalimbali kwa urahisi na kwa wakati," alisema Maduhu.

Evodius Barongo, mfanyabiashara wa kahawa wa Wilaya ya Ngara, mkoani Kagera amliema wakazi wengi wa Kagera wameona umuhimu wa Benki ya Kilimo kupitia vyama vya ushirika. Benki imetoa mikopo ya zaidi ya bilioni 32 kwa ajili ya kukuza zao la kahawa.

Serikali inataka Tanzania ijenge uchumi wa kati wezeshi na unaotegemea viwanda ifikapo 2025. Katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja TADB imerejesha matumaini kwa wadau wa kilimo nchini kwa kuwapatia mikopo ambayo imesaidia kuinua hali ya wakulima na kukuza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi hapa nchini.

# Wafanyabiashara walia na viongozi wa h'shauri

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wadogo zaidi ya 17 waliopo soko kuu la mjini hapa, wameulalamikia uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, kwa kutowarejesha katika maeneo yao waliyokuwa wanafanyia biashara awali ambayo kwa sasa wanataka kuyagawa kwa wafanyabiashara wengine.

Wakizungumza na gazeti hili jana, baadhi ya wafanyabiashara hao, Nelson Alfayo, Gilbert Fransis, Joseph Mungaya, Juma Zuberi na Gasper Ngowi, walisema wameshangazwa na uamuzi wa uongozi wa Halmashauri ya Jiji kwa uamuzi huo kwa kuwa wao wamekuwa wakifanya biashara katika eneo hilo kwa zaidi ya miaka 40 sasa.

Walisema kuwa uongozi wa Jiji la Arusha uliwaamuru wapishe eneo hilo ili waweze kujenga mabanda ya kisasa ndani ya soko hilo kwa ahadi kuwa baada ya kukamilika watapewa kipaumbele kurejeshwa katika eneo hilo, jambo ambalo halijafanyika. Mmoja wa wafanyabiashara hao,

Nelson Alfayo, alisema kuwa uongozi wa jiji uliwaambia waandike barua ya kuomba kugawiwa maeneo hayo jambo ambalo walilifanya kwa kuandika barua hiyo Mei 13, mwaka huu, lakini cha kushangaza hadi leo wamekuwa wakipigwa danadana ikiwa ni pamoja na kupewa vitisho vya mara kwa mara.

"Baada ya kuandika barua tumekuwa tukifuatilia na kwa mara ya mwisho tuliambiwa turudi Mei 29 na tulifanikiwa kukutana na

Mkurugenzi wa Jiji, Dk. Ahmad Madeni, lakini tulishangazwa na kitendo chake cha kuamuru Mwenyekiti wetu Fredy Eliphace na baadhi ya wenzetu watatu kukamatwa na kufikishwa kituo cha polisi," alisema Alfayo.

Aliongeza kuwa wenzao walipopelekwa polisi walifunguliwa jalada la kufanya biashara bila leseni, jambo ambalo halikuwa na ukweli wowote

kwa kuwa walikuwa nazo pamoja na vitambulisho vya mjasiriamali na walilazimika kulala katika kituo kikuu cha polisi hadi siku iliyofuata walipotoka kwa dhamana.

Alisema kuwa kitendo cha kutishiwa maisha na wenzao kukamatwa kimekuwa kikiwapa hofu kubwa kuendelea kufuatilia majibu ya barua yao na kuziomba mamlaka za juu kulianglia suala hilo na kuhakikisha linapatiwa ufumbuzi.

Akizungumzia suala hilo Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha, Kalist Lazaro, alisema wafanyabiashara hao wanatakiwa kufuata taratibu stahiki za kuomba kupatiwa eneo la kufanyia biashara na baada ya kutuma maombi wanatakiwa wasubiri vikao husika kwa ajili ya kuwajadili.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. Ahmad Madeni, alinukuliwa akiwaambia wafanyabiashara hao kuwa endapo wanataka kuomba maeneo ya kufanyia biashara ndani ya jiji wanatakiwa kuomba mtu mmoja mmoja na sio kundi kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni sawa na fujo.

Naye Ofisa Biashara wa Jiji la Arusha, Godfrey Edward, aliliambia gazeti hili kuwa wafanyabiashara hao walifika katika ofisi za halmashauri hiyo kuomba wapatiwe maeneo hayo, lakini halmashauri imetenga maeneo hayo kuwapatia wafanyabiashara ambao walikuwa na migogoro ya vibanda vya biashara kwa muda mrefu katika maeneo ya biashara yanayomilikiwa na halmashauri ya jiji hilo.

# Zaidi ya 2,000 wanufaika na huduma za afya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya wananchi 2000, katika kata tano za Wilaya ya Arumeru, wamenufaika na huduma za afya, matibabu pamoja na kupewa dawa bila malipo kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na magonjwa mbalimbali.

Huduma hiyo ya matibabu ilitolewa na Kanisa la FPCT, kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Mission and Friend pamoja na Taasisi ya Kimataifa ya Afya ya International Medical Relief (IMR), kutoka nchini Marekani.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa utoaji wa huduma hiyo, kwa wagonjwa mbalimbali, Mkurugenzi wa Idara ya Afya katika kanisa hilo, Dk. Yahana Masonde, alisema mradi huo wa kutoa huduma ya matibabu ulianza mwaka 2016.

Alisema huduma hiyo imewalenga wananchi wa kipato cha chini kutokana na kutokuwa na uwezo wa kulipia gharama za matibabu.

Alitaja magonjwa waliyowapima watu na kutoa matibabu kuwa ni ya macho, kisukari, moyo, meno, presha, malaria, kifua, magonjwa ya zinaa, vidonda, mfumo wa uzazi kwa wanawake, shinikizo la damu, koho, masikio pua na magonjwa ya ngozi.

"Watu wenye uwezo wa kifedha ndio wamekuwa wakimudu gharama za matibabu, lakini maskini wasiokuwa na fedha wanapata shida sana maeneo ya vijiji ndio maana tumechukua jukumu la kutoa huduma hii bure," alisema Msonda.

Hata hiyo, alisema katika Wilaya ya Arumeru wametoa huduma kwenye Kata za Lengijave, Oljoro, Sokon II na Kata ya Bangata katika Kijiji cha Sasi.

Alisema huduma hiyo wanaitoa kila mwaka mara moja na malengo yao ni kuongeza huduma hiyo angalau itolewe mara mbili kwa mwaka, pia mwaka huu waliitoa huduma kwa siku tano kwenye maeneo mbalimbali ya kata za Wilaya ya Arumeru.

Akizungumza kwa niaba ya wanufaika wa huduma hiyo, Florence Gigion, alishukuru kutolewa kwa huduma za afya kwa wagonjwa, huku akisema kutokana na wingi wa watu walivyojitokeza bado kuna uhitaji wa mkubwa wa kupeleka huduma hiyo maeneo ya vijijini. Mkuu wa msafara wa Taasisi ya International Medical Relief, Ellison Fellers, alisema sababu ya kuja nchini ni kuwasaidia wanajamii wanaokabiliwa na magonjwa mbalimbali hususani sehemu za vijijini.

Aidha, alisema pia wanatoa ushauri kwa wananchi namna ya kujikinga na magonjwa mbalimbali.



Madaktari bingwa kutoka Taasisi ya International Medical Relief (IMR) ya nchini Marekani, wakitoa huduma ya matibabu ya meno kwa wananchi wa kijiji cha Sasi Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru jana. **PICHA:ALLAN ISACK**

# Watakaofanya biashara ya madini nje ya nchi kukiona

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema serikali itawachukulia hatua kali za kisheria wafanyabiashara wote wa madini watakaofanya biashara ya madini nje ya soko la madini la kimataifa la Arusha lililofunguliwa jana.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa soko la madini la kimataifa la Arusha, Waziri Biteko, alisema hatarajii kuona wafanyabiashara watakaofanya biashara nje ya soko hilo baada ya serikali kufungua soko la kisasa la kimataifa litakalowarahisishia shughuli zao za kibiashara.

Alisema endapo watatokea wafanyabiashara watakao kwenda kinyume na agizo la serikali watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Waziri Biteko alisema soko hilo, litakuwa la kwanza la kimataifa la madini tangu nchi kupata uhuru, hivyo litaiwekea nchi katika historia kwa wafanyabiashara wakubwa kutoka nje ya nchi kuja nchini kununua.

Alisema tangu serikali ilipoanza utaratibu wa kulinda rasilimali za nchi na kurekebisha sheria mbovu za madini, matokeo chanya yameanza kuonekana kwa maslahi ya Taifa la Tanzania.

Aliwataka wafanyabiashara kulitumia soko hilo, kuongeza kipato chao na kulipa kodi ya serikali.

"Tulipe kodi kwa uaminifu na kulipa kodi ndio heshima yako kwa kuwa huu ni wajibu wa raia yeyote katika taifa lolote duniani, pia tuwachukie watu wanaokwepa kodi na kutorosha madini maana tunataka kutoka katika taifa la watu wajanja wajanja na kuwa watu watakaofanya shughuli halali," alisema Biteko.

Hata hivyo, alisema kabla ya marekebisho ya sheria za madini ya mwaka 2010, sekta hiyo ilikuwa inapitwa na sekta ya uvuvi katika kuchangia pato la taifa kitu ambacho siyo sawa kwa kuwa madini yanathamani kubwa.

Alisema baada ya marekebisho ya sheria za madini kurekebishwa sekta hiyo, imechangia pato la nchi kutoka asilimia 3.5 mpaka asilimia 5.0.7 kwa mwaka.

Alisema mpango wa serikali hadi kufikia mwaka 2025, sekta ya madini iwe inachangia asilimia 10 kwenye pato la nchi.

Aidha, alisema awali kwa mwaka sekta hiyo, ilikuwa inaiingizia serikali Sh. milioni 196, lakini baada ya serikali kuweka usimamizi imara katika sekta hiyo inaiingizia serikali fedha kiasi cha Sh. bilioni 300 kwa mwaka.





## Hai yafafanua mil. 84/- za uwezeshaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WILAYA ya Hai imesema mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 84.3 ya uwezeshaji kiuchumi iliyotolewa kwa makundi maalum inalenga kuwaandaa kuchangia pato la taifa baadaye.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, amesema mikopo hiyo ni mahususi kwa ajili ya kuinua kipato cha kaya, lakini pia kuwaongezea wananchi uwezo wa kuchangia pato la taifa kwa kulipa kodi ili kuiwezesha serikali kutoa huduma bora kwao.

Sintoo alikuwa akikabidhi jana, hundi za mfano kwa vikundi 16 vya wanawake, vijana na walemavu. Mkurugenzi huyo alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Sintoo alisema kuwa mikopo hiyo ina thamani ya Sh. 84,349,528.

Kwa mujibu wa Sintoo, mgao huo unahusisha vikundi 16 vya wajasiriamali ambao kati yao vikundi vya wanawake ni 11, vijana vitatu na vikundi viwili vya watu wenye ulemavu.

Sintoo ameeleza zaidi: "Tunakabidhi mikopo hii kwa wajasiriamali kama sehemu ya halmashauri kuinua uchumi wa wananchi wake. Mnatakiwa kutumia fedha hizi kwenye miradi ya kiuchumi mnayoiendesha ili kujiongezea kipato na kuchangia pato la taifa."

Baada ya makabidhiano hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai (DAS), Upendo Wella akitoa nasaha zake katika hafla hiyo, amewasisitiza wanavikundi hao kuwekeza fedha hizo kwenye miradi yenye tija hasa ikizingatiwa elimu waliyopatiwa ya matumizi sahihi ya fedha za mikopo.

Halmashauri ya Wilaya ya Hai imetoa mikopo hiyo kutokana na asilimia 10 ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa awamu ya pili kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

# Wanafunzi waguswa kufutwa msamaha wa kodi taulo za kike

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SIKU chache baada ya serikali kupendekeza bungeni kufutwa kwa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye taulo za kike, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za Wilaya ya Moshi, wamedai bado changamoto ya kukosekana taulo za kujisitiri ni tatizo linalohitaji msukumo zaidi wa kiutekelezaji. Suala hilo lilijitokeza jana, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, yaliyofanyika katika Shule ya Msingi Mvuleni, Kata ya Mabogini, Moshi Vijijini.

Akiwasilisha maoni ya watoto wa kike, mwanafunzi wa darasa la sita wa Shule ya Msingi Mvuleni, Hafsa Bilal, alisema: "Changamoto ya mtoto wa kike kukosa taulo za kujisitiri pindi anapokuwa hedhi, bado ni tatizo na hali hiyo kwa ujumla inaathiri uhudhuriaji wake wa masomo darasani."

"Tunatoa wito kwa watu wazima, taasisi mbalimbali binafsi, serikali na idara zake inapaswa kujitolea kwa hali na mali kuhakikisha haki za mtoto hazivunjwi na pia mtatue changamoto nyingi zinazomkabili mtoto bila kijali jinsia yake."

Wiki iliyopita, Waziri wa Fedha, Dk. Philip Mpango, alipendekeza kufutwa kwa VAT kwa taulo za kike, wakati akiwasilisha bungeni, bajeti kuu ya serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Katika maadhimisho hayo, Mratibu wa mradi wa kuwawezesha watoto wa kike (GEP), unaotekelezwa na Shirika la Kwieco, Immaculate Mworia, alisema wamekuwa mstari wa mbele katika kulinda juhudi za nchi za kiafrika kutambua thamani, utu na umuhimu wa mtoto katika nyanja zote na bila kumbagua.

Alisema shirika hilo linatekeleza miradi mbalimbali ukiwamo wa Girls Empowerment Program ambao unahusisha shule tano za msingi na sekondari za Moshi Vijijini.

Akizungumza pia na wanafunzi hao, Ofisa Elimu Sayansikimu na Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Conjeta Kessy, alisema licha ya kuwapo changamoto hiyo ya taulo za kike, bado kuna tatizo kubwa la watoto kutishwa kutosema ukweli mahakamani kuhusiana na kesi za ukatili ili wasilete aibu kwenye familia na kuwafunga wazazi wao.

"Halmashauri ya Moshi inazo shule za sekondari 98 na shule za msingi 276, lakini wazazi tunachangia kwa asilimia 100 kuharibu ndoto za watoto wetu. Hatuzungumzi na watoto kuhusu matatizo yao hata katika elimu tu," alieleza ofisa elimu huyo.

Kutokana na maoni hayo, wakili maarufu katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini na Mkurugenzi wa Shirika hilo la Kwieco, Elizabeth Minde, ameshauri jamii kutenga walao siku moja kila wiki kuzungumza na watoto wao kuhusu masomo yao na kama wana matatizo ya afya.



Katibu Tawala (DAS) wa Wilaya ya Moshi, Angelina Marko, akihutubia mwishoni mwa wiki katika Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika (African Child Day) katika Manispaa ya Moshi yaliyoandaliwa na manispaa hiyo, kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali yanayojishughulisha na masuala ya haki za watoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahukumiwa miaka 30 jela kwa kubaka mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Siha, imempa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani, mkazi wa Kijiji cha Makiwaru wilayani humo, Goodluck Mungure, baada ya kumtia hatiani kwa kosa la ubakaji.

Mungure (25), alianza maisha mapya ya kutumikia adhabu yake mwishoni mwa wiki, baada ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya hiyo, Jasmine Abdul, kujiridhisha kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa kumbaka mwanafunzi wa darasa la sita mwenye umri wa miaka 13.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Jasmine alisema mahakama imejiridhisha kwamba ushahidi wa watu sita uliotolewa mahakamani hapo haukuacha shaka yoyote.

Alidai upande wa mashtaka uliijenga kesi hiyo kwa kupeleka mashahidi waliotoa ushahidi unaomtia hatiani mshtakiwa na kwamba adhabu pekee iliyopo kisheria ni kifungo cha miaka 30 gerezani.

Wakati hukumu hiyo inasomwa, mshtakiwa huyo hakuwapo mahakamani hapo, huku kukiwa na taarifa kwamba mshtakiwa aameruka dhamana yake na kukimbilia kusikojulikana.

Mungure anadaiwa kutenda kosa hilo la ubakaji ambalo ni kinyume na kifungu cha 130 (1), (2)(e) na kifungu cha 131 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, David Chisimba, kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Novemba 24 mwaka jana, majira ya saa 7:00 mchana katika kijiji cha Makiwaru.

Katika hati ya mashtaka, imedaiwa kuwa Mungure alimbaka mwanafunzi huyo, huku akitambua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Inadaiwa kuwa siku ya tukio mwanafunzi huyo alikuwa ametoka kanisani katika ibada ya Jumapili na mshtakiwa huyo alimkamata mkono kwa nguvu na kumwingiza katika nyumba yake na kutekeleza ukatili huo.

Zaidi ilidaiwa kuwa baada ya kitendo hicho, mwanafunzi huyo alikwenda kumsimulia rafiki yake kuwa amebakwa na rafiki yake kumshauri waende kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi Sanya Juu, jambo ambalo lilisababisha mshtakiwa kutiwa mbaroni.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mwendesha mashtaka huyo aliomba mahakama kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo, ili iwe fundisho kwa watu wenye tabia kama hiyo.

NIPASHE JUMATATU JUNI 17, 2019
Nipashe
Spotika



WAZAWA WENYE NAMBA KIKOSI LIGI KUU 2018/19 UK.18




# SAHANI MOJA...

Kiungo wa Colombia, Mateus Uribe, akila sahani moja na mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi (mbele) kwenye mechi ya kuwania kufuzu Copa America 2020 iliyopigwa jana na Wargentina kushuhudia timu yao ikilala nyumbani kwa mabao 2-0. HABARI UK. 29 **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Pedro ni mchezaji wa tano kuweza kufunga kwenye mchezo wa fainali ya Kombe la Europa/Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Uefa/ Europa League, baada ya Allan Simonsen, Dmitri Alenichev, Hernan Crespo na Steven Gerrard.





Trent Alexander

# MABEKI WA KULIA BORA ZAIDI ULAYA

**LONDON, England**

MABEKI wa pembeni wamekuwa ndio watengenezaji wa nafasi za kufunga mabao katika soka la kisasa. Chukua hata mfano wa mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, Liverpool. Mabeki wao wa pembeni, Andy Robertson na Trent Alexander-Arnold wametengeneza nafasi nyingi zaidi za pasi za mwisho.

Bayern wana nyota kama Joshua Kimmich, David Alaba na usajili wao mpya, Benjamin Pavard ambao wametawala winga zote. Wachezaji kama Jonny na Matt Doherty wamekuwa na kiwango cha kuvutia katika klabu yao ya Wolves kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

Mabeki wa kulia ndio wameonekana kuwa wa muhimu zaidi kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita. Beki anayecheza kwa ubora wake katika majukumu yake, kulinda lango lake kushambuliwa. Huwa pia anatambaa na mipira pembeni na kuitupia katikati kwa ajili ya kutengeneza mashambulizi kwa timu pinzani. Yote kwa yote hapa tunawaangalia mabeki wa kulia watatu ambao ndio bora zaidi kwa msimu huu barani Ulaya...

Kwanza, heshima kwa kuwataja mabeki wengine ni: Matt Doherty (Wolves), Noussair Mazraoui (Ajax), Łukasz Piszczek (Borussia Dortmund), Achraf Hakimi (Borussia Dortmund).

**3. AARON WAN-BISSAKA (CRYSTAL PALACE)**

Kama timu kama Arsenal, Manchester City na Manchester United zinakimbizana kuwania saini yako ukiwa kwenye umri wa miaka 21, inamaanisha kwamba umefanya kazi kubwa. Wan-Bissaka alilazimika kuwa chaguo la pili mbele ya Timothy Fosu-Mensah aliyekuwa akicheza kwa mkopo msimu uliopita, lakini baadaye akaanza kuaminiwa na kocha Roy Hodgson, ambaye amemfanya kuwa chaguo la kwanza la beki wa kulia wa Palace kwa msimu wote.

Si mabeki wengi wa kulia ni bora duniani kuliko yeye hasa linapokuja suala la mtu kwa mtu. Amekuwa na uwezo mkubwa wa kusukumiza mashambulizi mbele hasa kutokea pembeni, hasa baada ya kuhakikisha kwamba lango lake liko salama. Uwezo wake bado umeonyesha kuwa ana uwezo mkubwa mno wa kuwazuia mawinga wakali kuleta madhara langoni mwake. Katika orodha hii anashika nafasi ya tatu kama beki bora wa kulia barani Ulaya akiwa na wastani wa kukaba 3.7 kwa mchezaji mmoja mmoja na 2.4 kwa mchezo.

**2. JOSHUA KIMMICH (BAYERN MUNICH)**

Phillip Lahm ni jina kubwa kwenye mpira wa miguu, hasa kwa Bayern Munich. Shukrani kwa Bayern, walikuwa na mtu sahihi wa kurithi mikoba yake na huyo ni Joshua Kimmich ambaye anafananishwa mno na Lahm. Kwa miaka mingi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa nyota mwenye mafanikio makubwa kwa klabu yake na timu ya taifa.

Kwa msimu huu amecheza mechi 34 za Ligi Kuu akitoa pasi za mwisho 13, huku akifunga mara mbili na kuwa na mafanikio ya pasi zake kuwa sahihi kwa asilimia 90. Wakati ambao kikosi hicho cha Niko Kova kilishindwa kutawala kama ilivyotarajiwa, Kimmich aliendelea kuwa bora zaidi na nyota kwa klabu hiyo.

**1. TRENT ALEXANDER- ARNOLD (LIVERPOOL)**

Bila shaka. Kile ambacho Alexander-Arnold amefanikiwa mwaka huu ni ndoto ya kila mchezaji duniani. Hasa ikizingatiwa kwamba, ndio kwanza ana umri wa miaka 19, lakini amefanya mambo makubwa. Ni mmoja wa bidhaa muhimu zaidi ya kocha Jurgen Klopp msimu huu, akitengeneza pasi za mwisho 12 kwenye Ligi Kuu ya England, akivunja rekodi ya kuwa beki aliyetengeneza pasi nyingi zaidi kwa msimu mmoja.

Huku akiwa na stamina ya kukimbia wakati akiwa na mpira, amekuwa akigawa mipira kwa uhakika mkubwa kwa winga. Akiwa anatumia mguu wake wa kulia, pia alifunga bao matata kwenye mchezo dhidi ya Watford.

Wakati linapokuja suala la akili na uwezo mkubwa dimbani, huwezi kusahau kile alichokifanya kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona, na kuisaidia timu yake kufuzu kwa fainali ambayo walishinda taji hilo kwa mara ya sita katika historia yake. Na katika umri wake wa miaka 19, ana safari nzuri zaidi mbele yake.

**JE, WAJUA?**



Jasper Cillessen ni kipa wa tano Uholanzi kufikisha mechi 50 za kimataifa, baada ya Edwin Van Der Sar (mechi 130), Hans Van Breukelen (mechi 73), Maarten Stekelenburg (mechi 58) na Gejus Van Der Meulen (mechi 54).

# MICHEZO




Wachezaji wa Simba wakipongezana kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union ambayo imetengeneza takwimu na rekodi kwa kuzaa hat-trick mbili kwenye mechi moja msimu wa 2018/19

## NJE YA UWANJA

### Arsenal yaigomea Milan kwa Torreira


Arsenal imekataa kumuuza kiungo Lucas Torreira wakati huu akitakiwa na AC Milan, kwa mujibu wa Sky Italia.

Wakati Marco Giampaolo akijiandaa kuondoka Sampdoria kwenda kuinoa miamba hiyo ya San Siro, alikuwa tayari kumsajili kwa mara nyingine mchezaji wake huyo wa zamani aliyejiunga na Arsenal, majira ya joto yaliyopita kwa pauni milioni 26.

Lakini Milan inaonekana kama kutaka kuhamia kwa mbadala mwingine, ikiwa ni pamoja na kiungo wa Sassuolo, Stefano Sensi, kutokana na mipango ya Arsenal ya kuendelea kumbakisha nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay.

Torreira alicheza mechi 34 za Premier League katika nafasi ya kiungo mkabaji ya kikosi hicho cha Unai Emery msimu uliopita, huku akifunga mabao mawili, na alicheza mechi zingine 16 za kombe.

Torreira aliibukia katika timu ya Pescara, akiwa ametua Italia kama kinda, kabla ya kujiunga na Sampdoria kwa dau la zaidi ya pauni milioni moja mwaka 2016.



# REKODI, TAKWIMU LIGI KUU KATIKA NAMBA

Na Adam Fungamwango

**738-** Hii ni idadi ya mabao yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu msimu huu. Ni ongezeko la mabao 173 kwani msimu uliopita 2017/18, jumla ya mabao 600 yalifungwa kwenye Ligi msimu huo.

Hata hivyo, msimu huu kuna ongezeko la timu nne, zaidi kutoka 16 za msimu uliopita hadi 20.

**243-** Namba hii inasimama kama ni idadi ya wafungaji wote waliofunga mabao kwenye Ligi Kuu msimu uliomalizika. Idadi hii imeongezeka zaidi kwani msimu uliopita 2017/18 ilikuwa ni wachezaji 156.

**52-** Ni idadi ya penalti zilizotolewa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika 2018/19. Msimu uliopita kulikuwa na jumla ya penalti 38, hivyo msimu huu kumekuwa na ongezeko la penalti 12 zaidi.

**44-** Namba hii inasimama kama idadi ya penalti zilizofungwa au kuwekwa nyavuni na wachezaji mbalimbali za Ligi Kuu msimu uliomalizika. Penalti 32 zilifungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita kwa hivyo zimeongezeka penalti 12 msimu huu zilizotiwa kwenye kamba.

**17-** Hii ni idadi ya mabao yaliyofungwa kwenye raundi ya mwisho ya Ligi Kuu, jumla ya timu zote 20 zikishuka dimbani kwenye viwanja mbalimbali nchini kumalizia mechi zao, kila timu ikicheza mechi ya 38.

**15-** Haya ni mabao yaliyofungwa kwenye raundi ya ufunguzi wa Ligi Kuu msimu huu. Baada ya timu zote 20 kucheza mechi za kwanza kulikuwa na idadi hii ya mabao, ambayo yalikuwa ni pungufu ya mawili ya idadi ya mabao ya mechi za mwisho.

**10-** Hii ni idadi ya mabao ya kujifunga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu mzima. Mashabiki wa soka katika hili wanawakumbuka zaidi wachezaji wawili ambao ni Ally Ally wa KMC aliyejifunga mwenyewe kwenye mechi dhidi ya Yanga na timu yake kuchapwa mabao 2-1, mwingine ni Mohamed Hussein 'Tshabalala' aliyejifunga kwenye mechi ambayo timu yake ya Simba ilicheza dhidi ya Kagera Sugar na kuwa bao pekee kwenye mechi hiyo, Simba ikilala bao 1-0.

**9-** Ni rekodi ya idadi kubwa zaidi ya mabao yaliyofungwa kwenye mechi moja msimu huu. Hii ilikuwa ni mechi kati ya Simba dhidi ya Coastal Union. Mechi hiyo ilichezwa Mei 8, mwaka huu na Simba iliibugiza bila huruma Coastal Union mabao 8-1 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**8-** Hii ni namba inayosimama kwenye idadi ya penalti zilizokoshwa au kuota mbawa kwenye Ligi Kuu msimu huu uliomalizika. Msimu uliopita ni penalti sita tu ziliota mbawa na kuwa na ongezeko la penalti mbili. Lakini pia namba hii inasimama kama ni idadi ya wachezaji waliokosa penalti kwenye Ligi Kuu msimu uliomalizika. Ina maana kuwa wachezaji wote wamekosa penalti moja moja na hakuna aliyekosa mara mbili kwenye mechi moja, au tofauti.

**5-** Hat-trick tano zimefungwa msimu huu uliomalizika. Ni idadi ya hat-trick sawa na ya msimu uliopita iliyomalizika kukiwa na jumla ya hat-trick tano.

Namba hii pia inasimama kuwa ni idadi ya penalti zilizofungwa na straika wa Simba John Bocco ambaye ndiye anayeongoza kwa kufunga penalti nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu msimu huu.

**3-** Ni idadi ya wachezaji wa kigeni waliofunga mabao matatu kwenye mechi moja, maarufu kama 'hat-trick' msimu huu. Hawa ni Mganda Emmanuel Okwi na Mnyarwanda Meddie Kagere, wote wa Simba ambao kila mmoja alifunga kwenye mechi dhidi ya Coastal Union. Mwingine ni Alex Kitenge raia wa Burundi akiichezea timu ya Stand United alifanya hivyo kwenye mechi dhidi ya Yanga, lakini timu yake ikifungwa mabao 4-3.

**1-** Inasimama kwa straika Salum Aiyee ambaye ni Mtanzania pekee amefunga mabao mengi zaidi kwenye ligi msimu huu. Mchezaji huyo wa Mwadui amemaliza ligi akiwa amecheka na nyavu mara 18 nyuma ya kinara Mnyarwanda Kagere. Namba hii pia inasimama kwake ndiye mchezaji wa kwanza kufunga bao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika. Alifanya hivyo kwenye mechi ya ufunguzi Agosti 22, mwaka jana kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Kagera, alipoifungia timu yake bao dakika ya tisa tu ya mchezo, mechi iliyoisha kwa timu yake ya Mwadui kuchapwa mabao 2-1. Mabao yote ya mechi zote 10 za ufunguzi yalifungwa baada ya dakika hiyo kupita.

Pia namba hii inasimama kwa Aiyee kama mchezaji pekee wa Kibongo nchini kufunga 'hat-trick' msimu huu. Alifanya hivyo kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa Uwanja wa Mwadui Complex, timu yake ikishinda mabao 4-0.

## Extra Time

# NYOTA WA5 WENYE NAFASI KUBEBA BALLON D'OR 2019




**LONDON, England**

NYOTA wa Real Madrid, Luka Modric alivunja utawala wa muongo mmoja wa Ronaldo-Messi wa kutwaa tuzo ya Ballon d'Or mwaka jana. Raia huyo wa Croatia alimaliza utawala huo wa wawili hao kwenye soka baada ya kuiongoza Croatia kumaliza nafasi ya pili kwenye michuano ya Kombe la Dunia.

Ballon d'Or inabakia kuwa tuzo kubwa zaidi kwa mchezaji binafsi wa mpira wa miguu, anayotunukiwa mchezaji ambaye anatajwa kuwa ndiye bora zaidi duniani.

Wachezaji wengi wamekuwa na misimu ya kuvutia kama vile Kylian Mbappe, Sergio Aguero, Raheem Sterling, Lionel Messi, Mohamed Salah, Sadio Mane, Bernardo Silva, Cristiano Ronaldo, Virgil van Dijk, Eden Hazard na wengineo wengi.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wana nafasi kubwa ya kuitwaa Ballon d'Or mwaka huu, twende pamoja...

**5. SADIO MANE**

Sadio Mane alikuwa na msimu mzuri zaidi kwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kiatu cha Dhahabu kwa kumaliza kama mmoja wa wafungaji bora kwenye Ligi Kuu ya England.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Senegal alifunga mabao 22 kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu na kuitwaa kwa pamoja tuzo hiyo pamoja na mchezaji mwenzake, Mohamed Salah na Pierre-Emerick Aubameyang wa Arsenal.

Mchezaji huyo, Mane mwenye umri wa miaka 27, alikuwa mmoja ya nguzo muhimu kwa Liverpool wakati ikitwaa taji la sita la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati akifunga mabao manne na kutoa pasi ya mwisho moja katika mechi 13 alizoichezea huku pia akisababisha penalti iliyozamishwa kimyani na Salah katika mechi ya fainali dhidi ya Tottenham.

Kiwango chake dhidi ya Bayern Munich kitabakia kuwa kwenye kumbukumbu baada ya 'kumtesa' golikipa Manuel Neuer kabla ya kufunga bao.

Mane alikuwa akiwania tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Ligi Kuu ya England, PFA, lakini ikachukuliwa na mchezaji mwenzake, Virgil van Dijk na sasa itakuwa nafasi nyingine wakati huu akiongoza nchini yake kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika, (Afcon) 2019.

Senegal ipo kwenye nafasi nzuri ya kutwaa taji hilo na hilo linaweza kumsaidia mshambuliaji huyo wa Liverpool kuwa na nafasi ya kuitwaa tuzo hiyo mwaka huu.

**4. MOHAMED SALAH**

Mshambuliaji huyu wa Liverpool baada ya kuwa na msimu mzuri zaidi wa kwanza akiwa na 'Wekundu' hao, sasa umekuwa bora zaidi kwake. Mohamed Salah aliisaidia timu yake kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kufungwa na Real Madrid mwaka jana, na kumuacha akiondoka uwanjani na machozi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri msimu huu alifunga mabao 22 na kumfanya atwae kwa mara ya pili mfululizo tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora, akiitwaa sambamba na mchezaji wa Arsenal, Aubameyang na Mane ambao wote walifunga mabao 22.

Nyota huyo wa Liverpool alikuwa kwenye orodha ya wanaowania tuzo hiyo mwaka jana, lakini alishika nafasi ya sita nyuma ya Lionel Messi aliyeshika nafasi ya tano.

Mchango wa Salah kwenye kutwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya pia unaweza kuchangia yeye kuibeba tuzo hiyo. Mabao yake matano kwenye ligi hiyo yalikuwa muhimu kuisaidia timu yake na muhimu zaidi alilolifunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya pili kwenye fainali dhidi ya Tottenham ambapo 'alimtawanya' golikipa Hugo Lloris.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ataiongoza nchi yake kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 yanayofanyika katika ardhi ya nyumbani kwake na hivyo kama akilibeba taji hilo ana nafasi kubwa ya kutwaa Ballon d'Or.

**3. CRISTIANO RONALDO**

Cristiano Ronaldo alifanya maamuzi yake ya kuihama Real Madrid kwenda Juventus msimu uliopita.

Baada ya kuwa na mwanzo mgumu pale, Mreno huyo hatimaye akafunga mabao 21 katika mechi 31 alizowachezea Bianconeri hao kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A. mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alibeba taji la Ligi Kuu ya Italia, Scudetto, na akatwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka katika msimu wake wa kwanza nchini Italia.

Mfalme huyo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya alishindwa kuivusha Juve kwenye michuano hiyo. Ingawa 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kilimaliza kwenye hatua ya robo fainali, ilikuwa ngumu Ronaldo kulaumiwa. Kiwango cha Mreno huyo kwenye mchezo dhidi ya Atletico na dhidi ya Manchester United kilikuwa cha kuvutia. Dhidi ya Rojiblancos, kilipindua matokeo wakati akifunga mabao matatu 'hat-trick' na kuiwezesha Juve kutinga nane bora. Lakini licha ya kuonyesha kiwango cha juu, Juve iliondolewa na Ajax na mabao yake hayakutosha kuiokoa.

Nafasi ya Ronaldo kuitwaa tuzo hiyo sasa imeongezeka baada ya kutwaa Kombe la Ligi ya Mataifa ya Ulaya. Ureno walitwaa taji la ligi hiyo mpya kwa Mataifa ya Ulaya baada ya kuifunga Uholanzi bao 1-0.

**2. LIONEL MESSI**

Hii ni alama ya Barcelona. Lionel Messi kwenye orodha hii anashika nafasi ya pili kama inavyoonekana. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Argentina alikuwa katikati ya msimu bora zaidi kwake na hivyo kuwa kwenye nafasi kubwa zaidi ya kuibeba tuzo hiyo mwaka huu.

Messi alifurahia wakati bora zaidi katika msimu huu, akifunga mabao 36 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, katika mechi 29 alizoanza kwa miamba hao wa pale Catalunya na alitwaa tuzo ya mfungaji bora kwa ligi zote za Ulaya kwa mara ya tatu mfululizo.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 31, pia alimaliza akiwa mfungaji bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akifunga mabao 12. Kiwango chake dhidi ya Tottenham, Liverpool na Manchester United kilikuwa cha kuvutia zaidi.

Nyota huyu wa Barcelona nafasi ya kulitwaa taji la Ligi ya Mabingwa zilizimwa na Liverpool wakati walipofungwa pale kwenye dimba la Anfield mabao 4-0 na hivyo kutolewa hatua ya nusu fainali. Wakati huo huo, Barca wakifungwa na Valencia kwenye fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa Del Rey'].

Matumaini ya Messi kunyanyua tuzo ya Ballon d'Or kwa mara ya sita sasa yamebakia kwa kiwango atakachokionyesha kwenye michuano ya mataifa ya Amerika Kusini, Copa America. Argentina inapewa nafasi ya pili kuwa na nafasi kubwa ya kulibeba taji hilo nyuma ya Brazil, na kama Messi akilibeba, hakutakuwa na wa kumzuia kuitwaa tuzo hiyo.

**1. VIRGIL VAN DIJK**

Baada ya Fabio Cannavaro kuitwaa tuzo hiyo mwaka 2006, Virgil van Dijk anaweza kuwa beki wa kwanza kushinda Ballon d'Or. Mholanzi huyu ana ndoto baada ya kuwasaidia 'Wekundu' hao kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakimaliza kusubiria kwa kipindi cha miaka 14.

Van Dijk alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu ya England, PFA, mbele ya Mane, Raheem Sterling, Sergio Aguero na Bernardo Silva baada ya kuimarisha vizuri safu ya ulinzi ya Liverpool.

Ukuta wa chuma wa Liverpool uliwasimamisha washambuliaji kama Aguero, Sterling, Messi na wachezaji wengine wengi ambao walishindwa kabisa kuipita ngome yao.

Kiwango cha Mholanzi huyo kwa kipindi cha msimu huu kimemsaidia golikipa wa Wekundu hao, Alisson Becker kuwa imara zaidi. Kiwango chake dhidi ya Tottenham kwenye fainali dhidi ya Barcelona katika mchezo wa pili, ndicho kinaweza kuwa bora zaidi kwenye michuano hiyo.

Mholanzi huyo pia aliiongoza nchini yake kwenye fainali ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya, ambapo walipoteza dhidi ya Ureno walioshinda kwa bao 1-0.

## Nukuu

"Timu ya taifa itaendelea, ikiwa ama bila Cristiano. Nadhani timu ina uwezo mkubwa, kuna wachezaji vijana, wachezaji ambao kwa miaka ijayo watakomaa zaidi na kuwa bora. "Ninataka kuwa sehemu ya mradi huu kwa sababu ninajisikia vizuri na najisikia kuwa tayari kuisaidia timu ya taifa," Nahodha wa Ureno, **Cristiano Ronaldo** baada ya kuibebesha Kombe la Ligi ya Mataifa ya Ulaya.



"Nina furaha, nadhani ni usajili mkubwa, ni mmoja wa wachezaji wa kiwango cha juu duniani, ni vizuri kuimarisha kikosi kwa aina hiyo ya wachezaji ambao wanaweza kufafanua zama," Nahodha wa Real Madrid, **Sergio Ramos** akielezea furaha yake baada ya klabu hiyo kufanikisha usajili wa Eden Hazard kutoka Chelsea.




"Sikutaka kuwapeleka watoto wangu shule, kila mmoja angeweza kuniona nilikuwa baba mbaya. Kulikuwa na siku ambazo sikutaka kufanya lolote, ulikuwa wakati mgumu mno kwangu. Sikuona namna Liverpool wanaweza kututoa, kwa sababu Barcelona tulikuwa mbele na tulikuwa na kikosi bora kabisa na tulikuwa na nafasi kubwa zaidi," Mshambuliaji wa Barcelona, **Luis Suarez** akielezea alivyopata mshituko na maumivu makubwa mno baada ya kutolewa na Liverpool kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



# WAZAWA WENYE NAMBA KIKOSI LIGI KUU 2018/19




GADIEL MICHAEL

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tuliwaletea kikosi cha jumla cha wachezaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2018/19 uliyomalizika Mei 28, mwaka huu.

Kikosi hiki kiliwajumuisha wachezaji wa Kibongo na wa kigeni ambao walionekana kufanya vema kwenye Ligi Kuu msimu huu. Leo katika makala haya, tunawaletea wachezaji wazawa tu waliotamba kwenye Ligi Kuu msimu uliomalizika, na wiki ijayo tutamalizia kwa kutazama kikosi cha wachezaji wa kigeni tu.

Hiki ndicho kikosi bora kabisa cha wachezaji wa Kitanzania waliotikisa kwenye Ligi Kuu, nenda nacho...

**1. AISHI MANULA- SIMBA**

Alikuwapo kwenye kikosi bora cha jumla, lakini pia yumo kwenye kikosi cha wachezaji wa Kibongo.

Ukiwajumlisha makipa wa Kitanzania, Manula anawazidi kwa vitu vyote kitakwimu, ikiwapo kuwa na mechi nyingi ambazo hajaruhusu bao 'clean sheets' na pia kufungwa mabao machache kwenye Ligi Kuu.

**2. BONIFACE MAGANGA- SINGIDA UNITED**

Pia beki huyu anarejea tena kwenye kikosi cha Wabongo watupu waliofanya vema kwenye Ligi Kuu. Ni beki wa kupanda na kushuka ambaye pia ana uwezo mkubwa wa kufunga mabao, akiwa mmoja wa mabeki wanaoongoza kwa kufunga mara nyingi kwenye Ligi Kuu baada ya kupachika mabao matano msimu wa 2018/19.

**3. GADIEL MICHAEL- YANGA**

Ni beki aliyeonyesha uwezo wa hali ya juu akiwa na kikosi cha Yanga msimu huu. Ana uwezo wa kuzuia mashambulizi, lakini pia kuwasaidia mastraika kufanya mashambulizi kwenye eneo la adui.

Sifa yake kubwa ni kasi, pamoja na uwezo wa kurudi nyumba haraka. Kuna taarifa kuwa anawindwa na Klabu ya Simba na Azam FC.

**4. AGGREY MORIS- AZAM FC**

Kama alikuwapo kwenye kikosi cha jumla, huwezi kumtoa kwenye kikosi cha wazawa.

Ni beki aliyekamilika na aliyeumbwa kuwa beki. Ana nguvu, akili pamoja na maamuzi ya haraka yanayoshindwa kumpa straika yeyote uamuzi wa kumpita kirahisi.

Pamoja ya kwamba ana tatizo la hasira na wakati mwingine kucheza rafu zinazosababisha kuonywa kwa kadi nyekundu na kuiathiri timu yake, lakini huwezi kuondoa ukweli kuwa ni beki bora nchini na yupo kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars.

**5. ERASTO NYONI- SIMBA**

Ni beki ambaye hapa Bongo hana mjadala. Anakubalika na mashabiki wa timu zote. Ni mmoja wa mabeki wachache nchini wenye matumizi makubwa ya akili zaidi kuliko nguvu.

Huwezi kumuacha kwenye kikosi bora cha wachezaji wa Kitanzania. Ikumbukwe kuwa pia Simba imemuongeza mkataba haraka kwa kuhofia kuzidiwa kete kama ingemuacha kwenye michuano ya Afcon 2019 bila kumpa mkataba.

**6. MUDATHIR YAHAYA- AZAM FC**

Bado ni mchezaji mwenye uwezo mkubwa wa kusaidia mabeki wake kukabiliana na mastraika wasumbufu. Huyu ni kiungo mkabaji wa Azam, lakini pia ana uwezo wa kwenda mbele kusaidia mashambulizi.

Kwa msimu huu ameonekana yuko vizuri zaidi kuliko viungo wakabaji wengine wa Kibongo kwenye klabu zingine.

**7. AYOUB LYANGA- COASTAL UNION**

Ni yule yule Ayoub Lyanga aliyekuwa kwenye kikosi cha wachezaji bora wa msimu. Sasa yupo kwenye kikosi cha Wabongo watupu. Ni winga mwenye mabao 10, mwenye uwezo mkubwa wa kupiga chenga na kasi. Taarifa za usajili zinasema kuwa anawindwa na klabu kubwa tatu za Simba, Yanga na Azam FC. Na kwa jinsi alivyofanya vema msimu huu, sidhani kama msimu ujao ataichezea Coastal Union.

**8. IDD SULEIMAN 'NADO'- MBEYA CITY**

Ni mchezaji mwenye uwezo wa kucheza kama kiungo mchezeshaji, winga na pia straika. Hapa kwenye kikosi hiki tunamuweka kwenye nafasi ya kiungo mchezeshaji.

Amemaliza ligi akiwa na mabao saba, akiwa mhimili mkubwa wa kikosi cha Mbeya City, iliyomsajili kutoka kwenye michuano ya Ndondo Cup misimu miwili iliyopita, akiichezea Manzese United.

**9. JOHN BOCCO- SIMBA**

Ni straika mwenye sifa zote za kuitwa hivyo. Ana nguvu, uwezo wa kukaa na mpira miguuni kwa muda mrefu, lakini pia kutumbukiza mipira ndani ya nyavu na hasa ni hatari zaidi kwa mipira ya vichwa. Amemaliza ligi akiwa na mabao 16, lakini akiwa amefanya kazi kubwa sana kiasi cha kuipa timu yake ya Simba ubingwa wa Tanzania Bara.

**10. SALIM AIYEE- MWADUI FC**

Kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu ya Tanzania, imepata straika Mbongo hatari mwenye uwezo mkubwa wa kufumania nyavu, huyu si mwingine bali ni Salim Aiyee.

Amepachika mabao 18 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akikamata nafasi ya pili kwenye ufungaji bora nyuma ya mgeni Meddie Kagere aliyecheka na nyavu mara 23. Aiyee ndiye kinara wa mabao kwa Wabongo msimu huu.

Hata kwenye mechi za 'play off' mabao yake mawili ndiyo yaliyoirejesha Mwadui kwenye Ligi Kuu.

**11. RAMADHANI KAPERA- KAGERA SUGAR**

Ana uwezo wa kucheza kama straika au winga wa kushoto. Ni mchezaji mwenye uwezo mkubwa wa kukaa na mpira miguuni, lakini pia uwezo wa kunyumbulika na kupiga chenga za maudhi na kufunga pia. Haogopi mabeki, bali anapiga chenga huku akiwa anawafuata wapinzani, kitu ambacho si cha kawaida sana kwa wachezaji wengi. Ameingia kwenye kikosi bora cha wachezaji wa ndani msimu huu.

**NAJUA WAJUA**



URENO ni timu ya kwanza Ulaya kuweza kuwa mwenyeji na kushinda fainali ya michuano mikubwa tangu Ufaransa ilipoichapa Brazil 3-0 katika mechi ya fainali ya Kombe la Dunia mwaka 1998.

SOKA




# WALIOSHINDA, KUPOTEZA USAJILI WA HAZARD REAL

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid ilitangaza kumsajili mshambuliaji wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28, Eden Hazard kutoka Chelsea Ijumaa iliyopita. Klabu hiyo ilipata huduma ya Hazard kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni zaidi ya euro milioni 100 na amesaini mkataba wa miaka mitano na 'Los Blancos' hao. Mbelgiji huyo alikuwa usajili wa kwanza wa Los Blancos tangu James Rodriguez, ambaye alitua hapo mwaka 2014.

Baada ya kuwasili kutoka Lille mwaka 2012, Hazard ameonyesha kiwango cha juu kwenye Ligi Kuu ya England. Hazard anachukuliwa kama mmoja wa washambuliaji aliyekamilika duniani mwenye uwezo wa kuiangamiza safu yoyote ya ulinzi anavyotaka.

Mbelgiji huyo anashika nafasi ya tisa kwa wafungaji bora wa Klabu ya Chelsea akifunga mabao 110, huku mabao 85 akifunga kwenye Ligi Kuu ya England. Hazard ametoa pasi za mwisho 54 kwa Blues hao kwenye Ligi Kuu na ametengeneza nafasi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu kuliko mchezaji yeyote wa Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ameshinda mara tatu taji la Ligi Kuu na pia ametwaa lile la Ligi ya Europa kwa kipindi chake alichokaa kwa Blues hao. Hivi karibuni, Hazard amefunga mabao 21 na pasi za mwisho 17 kwenye mashindano yote, na kuisaidia kushinda taji la Ligi ya Europa msimu huu uliomalizika.

Kwa upande mwingine, Real Madrid walikuwa na msimu mbaya zaidi katika siku za hivi karibuni baada ya kuondoka kwa Cristiano Ronaldo. Walikuwa wanahitaji mshambuliaji wa daraja la juu na Hazard ndiye alikuwa akifiti kwenye nafasi hiyo.

Pamoja na yote, hapa tunaangalia nani ni mshindi na aliyepoteza kwa usajili huu wa Hazard, tiririka nayo...

**4. MSHINDI: KARIM BENZEMA**

Licha ya Los Blancos kuwa na msimu mgumu wa 2018/19, Benzema alisimama kuwa ndiye mchezaji wao bora. Mshambuliaji huyu raia wa Ufaransa alimaliza La Liga akiwa kama mfungaji bora namba mbili akifunga mabao 21 sawa na Luis Suarez wa Barcelona. Katika mashindano yote, amefunga mabao 30 na kutoa pasi za mwisho 11 na ameonyesha kuwa na mchango mkubwa zaidi kwa klabu yake msimu huu uliomalizika.

Hakuna shaka kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ndiye aliyeonekana kuwa mbele baada ya kukosekana kwa Ronaldo. Washambuliaji kama Gareth Bale, Marco Asensio na Mariano hawakuwa kwenye ubora wa kuvutia. Kwa ushirikiano wa mbali na Vinicius Jr, Benzema aliachwa kuwa ndiye tegemeo pekee kwenye ushambuliaji.

Sasa kwa kujumuishwa kwa mchezaji kama Hazard, Benzema atakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kulishwa mipira mbele ya goli. Na pengine sasa wanakuwa na upatina mzuri zaidi wa Benzema kama alivyoupata wakati wa uwapo wa Ronaldo.

**3. ALIYEPOTEZA: MAURIZIO SARRI/CHELSEA**

Tayari Maurizio Sarri amepewa ruhusu ya kuondoka Chelsea na kama angebaki angekuwa amepoteza mno kwa kuondoka kwa Eden Hazard aliyetua Real Madrid. Pamoja na kwamba, Blues walipata kiasi cha euro milioni 100 kwa kumuuza, lakini wamepoteza bidhaa muhimu zaidi.

Mafanikio ya msimu wa kwanza wa Maurizio Sarri katika klabu hiyo ulibebwa kwa kiasi kikubwa na Hazard. Kwani peke yake tu alihusika katika mabao 31. Chini ya Sarri, Blues hao walifunga mabao 63 kwa kipindi chote na Hazard alihusika katika nusu ya mabao hayo.

Ni wazi kwamba fedha haziwezi kuwa mrithi wa Hazard. Zaidi ni kwamba pengo lake ni kubwa hasa ikizingatiwa kwamba Chelsea imepigwa marufuku ya kufanya usajili msimu huu baada ya kukiuka sheria ya haki sawa ya matumizi ya fedha. Licha ya kukata rufani kwa Mahakama ya Usuluhishi ya Masuala ya Michezo (CAS), lakini wamegonga mwamba.

**2. MSHINDI: ZINEDINE ZIDANE**

Wakati Zinedine Zidane aliporudi kuchukua nafasi ya kuwanoa tena Los Blancos kwa mara ya pili, timu hiyo ilihitaji kujiimarisha zaidi.

Real Madrid walikuwa wanasumbuka kwenye safu ya ushambuliaji na walishindwa kushindana na wapinzani wao Barcelona, Ajax na klabu nyingine kwenye La Liga na Ulaya. Hata baada ya Zidane kurudi, alishindwa kuifanya Madrid kurudi kwenye

**UBORA WAKE, KWANI WALIPOTEZA MECHI 12.**

Hakukuwa na shaka kwamba miamba hao wa Hispania walikuwa wanahitaji kukiimarisha kikosi chao na Zidane aliweka wazi kwamba atakifumua kikosi chake haraka. Zidane aliahidiwa kuwa utafanyika usajili wa nguvu kama akirudi Santiago Bernabeu na atarudisha mfumo wa kusajili wachezaji wenye majina makubwa, Galactico, na wamefanya hivyo kwa Hazard.

Zidane ambaye aliwarithi watangulizi wake, Julen Lopetegui na Santiago Solari amepata nafasi nzuri zaidi ya kuwa na Hazard kwenye kikosi chake. Kuwasili kwa Hazard kutaimarisha zaidi safu ya ushambuliaji ya Real Madrid kama ambavyo alivyokuwa kule Chelsea. Zaidi ni kwamba Zidane mara kadhaa amezungumzia kuhusu kuvutiwa na nahodha huyo wa timu ya Taifa ya Ubelgiji.


**1. ALIYEPOTEZA: GARETH BALE**

Gareth Bale alitarajiwa kwamba angeweza kufiti kwenye viatu vya Ronaldo baada ya kuondoka kwake kipindi cha majira ya joto kilichopita. Raia huyo wa Wales alifurahia kipindi chake cha mchezaji hapo Santiago Bernabeu, lakini alikumbwa na majeraha ya mara kwa mara. Baada ya kufunga bao lake 'tamu' kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool msimu uliopita, Los Blancos walimtarajia kuwa ndiye atakayeongoza safu yao ya ushambuliaji.

Hata hivyo, kushindwa kwa Bale kuongoza mashambulizi, kukaifanya klabu hiyo kuwa na wakati mgumu zaidi. Majeruhi yakamfanya Bale kumaliza msimu akiwa na mabao 14 na kutoa pasi za mwisho sita katika mashindano yote. Kutokana na kiwango kushuka, Bale anaonekana wazi kwamba hayupo kwenye mipango ya kikosi cha Zidane.

Na taarifa zaidi zinaeleza kwamba, Bale hayupo kwenye mipango ya Zidane kwa msimu unaokuja. Hata kama atabaki, ni wazi kwamba amepoteza nafasi yake katika kikosi cha kwanza. Na kwa ujio wa mchezaji kama Hazard ambaye yupo daraja la juu, nafasi ya Bale kwenye kikosi cha kwanza pale Real Madrid haitakuwapo tena.

NDANI YA 18



USHINDI wa mabao 13-0 Timu ya Taifa ya Wanawake ya Marekani iliyoupata kwenye fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Thailand, ndicho kipigo kikubwa zaidi kuwahi kutolewa katika historia ya michuano hiyo ya dunia kwa upande wa wanawake.

Nipashe
Spotika



...Wachezaji wengi wamekuwa na misimu ya kuvutia kama vile Kylian Mbappe, Sergio Aguero, Raheem Sterling, Lionel Messi, Mohamed Salah, Sadio Mane, Bernardo Silva, Cristiano Ronaldo, Virgil van Dijk, Eden Hazard na wengineo
Uk. 16-17

# MAKIPA WA5 WAKUVAA GLOVU ZA DE GEA UTD

**MANCHESTER, England**

INAONESHA ni wazi kwamba kipindi hiki cha majira ya joto pale Old Trafford kutakuwa na usajili mkubwa chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer.

Ulikuwa msimu mbaya kwa Manchester United ikiwa imeanza msimu chini ya kocha Jose Mourinho ambaye alikuwa na matokeo ya kukatisha tamaa na hasa baada ya maombi yake ya kumleta beki wa kati kushindikana. Hivyo United haikuwa na matokeo ya kuvutia kwa kipindi cha pili cha msimu.

Matokeo yalikuwa mabaya zaidi chini ya Mourinho, na baada ya kipigo cha mabao 3-1 nyumbani dhidi ya Liverpool, alifukuzwa. Nafasi yake ikachukuliwa na Ole Gunnar Solskjaer ambaye awali alikuwa kocha wa muda hadi akiacha kazi pale katika klabu ya Molde na kujiunga kwenye dimba la Old Trafford.

Solskjaer alianza vizuri, na akapewa mkataba wa kudumu kuwa kocha, baada ya kuwa na kiwango kizuri kwa kuifunga PSG kwenye hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mambo yakabadilika kuelekea mwishoni mwa msimu, wakati walipotolewa na Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa, na walimaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England baada ya kuwa na kipindi kirefu cha matokeo mabaya.

Kwa upande mwingine United baada ya kumalizika kwa msimu ni David de Gea, ambaye alikuwa anachukuliwa kama golikipa bora duniani. Alifanya makosa mengi katika wiki ya mwisho ya msimu, na alifanya makosa zaidi kwenye mchezo dhidi ya Manchester City, Barcelona na Chelsea.


Kwa sababu ya hiyo, na ukweli ni kwamba mwaka mmoja umebakia kwenye mkataba wake na United, kuna uvumi kwamba De Gea anaweza kuondoka Manchester kipindi hiki cha majira ya joto, huku PSG wakipewa nafasi kubwa kwa yeye kwenda kujiunga nao.

Hiii inamaanisha kwamba United wanatakiwa kusajili kipa mpya kipindi hiki, huku Solskjaer akitaka kutafuta golikipa ambaye atakuwa msaada kwa kikosi chake. Hapa tunawaangalia magolikipa watano wanaoweza kumrithi De Gea kipindi hiki cha majira ya joto, twende sasa....

**1. Keylor Navas (Real Madrid)**

Baada ya miaka mitano pale Bernabeu, Navas anaonekana anataka kuondoka Real Madrid. Licha ya kurudishwa kwenye kikosi cha kwanza kuelekea mwishoni mwa msimu baada ya Zinedine Zidane kurudishwa kuwa kocha wa Real, Navas anaonekana kwamba hahitajiki zaidi na alishaambiwa kwamba anaweza kutafuta klabu nyingine.

Katika umri wake wa miaka 32, Navas anaweza kuwa ubora wake unakaribia mwisho, lakini amekuwa na mafanikio makubwa kwa kipindi chote alichokaa hapo Real Madrid. Ameshinda mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, na alitajwa kuwa golikipa bora wa msimu wa michuano hiyo msimu wa 2017/18. Kwa Navas, United wanaweza kuwa wanasajili mtu mwenye uzoefu wa kiwango cha juu katika soka la Ulaya, na ubora wa kiwango cha juu. Anaweza pia kupatikana kwa bei nafuu, hivyo kama 'Mashetani Wekundu' hao wanamhitaji, anaweza kuwa msaada mkubwa kwao.



**2. Gianluigi Donnarumma (AC Milan)**

Kama United inatafuta mrithi wa muda mrefu wa De Gea, hivyo wanatakiwa kumuangalia Donnarumma. Muitaliano huyu ndiye kwanza ana umri wa miaka 20, lakini tayari ameshajithibitishia kuwa ni golikipa wa kiwango cha juu. Amekuwa golikipa namba moja wa Milan tangu akiwa na umri wa miaka 16, na tayari amecheza mechi 142 za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa jina lake, akicheza mechi 46 bila kuruhusu bao.

Ingawa namba hiyo inaweza kuwa siyo ya kuvutia kwa baadhi ya magolikipa ambao United wanawawania, kwani anacheza katika moja ya kikosi cha ovyo zaidi cha Milan kilichowahi kushuhudia katika miongo ya hivi karibuni. United inaweza kuchua tahadhari ya kusajili mtu ambaye hana uzoefu wa Ligi Kuu ya England ambayo ni ya kutumia nguvu zaidi kuliko ile ya Serie A. Anaweza asiwe wa bei rahisi, lakini Milan kwa kuwa inahitaji fedha, wanaweza kumuuza kwa bei ya kawaida.

**3. Jasper Cillessen (Barcelona)**

Golikipa mwingine ambaye anaweza kuwa rahisi zaidi kwa United kwa kipindi hiki cha majira ya joto ni yule wa Barcelona, Jasper Cillessen. Mholanzi huyu alijiunga na miamba hao wa Catalunya mwaka 2016, lakini kwa sababu ya Marc-Andre ter Stegen kuwa kwenye kiwango cha juu zaidi, nafasi yake imekuwa ngumu pale katika dimba la Nou Camp.

Katika kipindi cha miaka mitatu nchini Hispania, amecheza mechi tano tu za Ligi Kuu ya La Liga, huku 24 akicheza kwenye Kombe la Mfalme ['Copa Del Rey']. Na matokeo yake sasa anaweza kuondoka kipindi cha majira ya joto, hasa ikizingatiwa kwamba anataka kupata nafasi kwenye kikosi cha Taifa cha Uholanzi.

Anaweza akaonekana hayupo kwenye daraja la juu kwa United kati ya wale inaowahitaji, lakini kwa kushindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, itakuwa ngumu kuwashawishi wachezaji wakubwa msimu ujao. Cillessen anaweza kuwa tu kwa kipindi kifupi, lakini kumsajili moja kwa moja itaonekana kama biashara kichaa.

**4. Andre Onana (Ajax)**

Inaonekana amekuwa kwenye kiwango cha juu pale Ajax msimu huu baada ya kuiwezesha kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Frenkie de Jong tayari ameshachukuliwa na Barcelona, na Matthijs de Ligt anaweza kumfuata hivi karibuni, huku pia kumekuwa na ofa kwa David Neres, Hakim Ziyech na Donny van de Beek. Mtu mwingine ambaye anaonekana kwamba ataondoka hapo katika Jiji la Amsterdam ni Andre Onana, ambaye alikuwa na msimu bora zaidi katika goli la Ajax.

Katika umri wake wa miaka 23, golikipa huyu wa kimataifa wa Cameroon ambaye alitua hapo akitokea akademi ya Barcelona, alisajiliwa na Ajax mwaka 2015, na amecheza mechi 98 kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie. Amecheza mechi 32 bila goli lake kutikiswa, na ameisaidia timu yake kushinda taji la Eredivisie kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2014. Anaweza asiwe chaguo la United, lakini ameshajithibitisha yeye mwenyewe kwamba ni golikipa bora pale Ajax. Anaweza asipatikane kwa bei rahisi, kwani klabu hiyo imeshajitanabaisha kuwa ipo vizuri kwenye suala la mazungumzo ya kumuuza mchezaji.

**5. Jan Oblak (Atletico Madrid)**

Kama United inataka kumsajili golikipa bora kwa soko la sasa, Oblak anaweza kuwa mtu sahihi kwao. Raia huyo wa Slovenia ameonyesha ubora wake pale Atletico wakati alipojithibitishia kuwa ni mmoja kati ya makipa bora duniani. Rekodi yake tangu atue kwa miamba hao wa Hispania ni ya kuvutia. Tangu kuanza kwa msimu wa 2015/16, amecheza mechi 142 za La Liga, huku akicheza mechi 81 bila nyavu zake kutikiswa na ameruhusu mabao 82 tu.

Kwa United, unaweza kuwa usajili bora zaidi. Kwa kuwa safu yao ya ulinzi imekuwa haina ubora mzuri, hivyo wanahitaji mtu ambaye ana uwezo mkubwa pale golini na Oblak anaweza kulifanya hilo. Anaweza asiwe rahisi, na anaweza kuipiku rekodi ya golikipa wa Chelsea, Kepa Arizzabalaga wakati aliposajiliwa kwa pauni milioni 72 kipindi kilichopita. Hata hivyo, kama United watamuuza De Gea, wanajua kwamba watahitaji golikipa wa daraja la juu kumrithi, na Oblak pengine anaweza kuwafaa.

## USILOLIJUA



NAFASI ya tatu England iliyomaliza kwenye michuano ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya, ni mara ya kwanza kwao kumaliza katika nafasi ya juu kama hiyo kwenye mashindano makubwa ya kimataifa tangu ilipofanya hivyo kwenye Euro 1968.



# HABARI MBEYA

## Mafundi wasiopitia Veta watahadharishwa

**Na Nebart Msokwa** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imewatahadharisha mafundi wa fani mbalimbali wa mitaani ambao wanafanya kazi hiyo bila kupitia kwenye Chuo cha Ufundi Stadi (Veta).

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipokuwa anazungumza na wafanyakazi wa Chuo cha Veta cha Mkoa wa Mbeya.

Alisema serikali inakusudia kufanya msako mkali wa kuwasaka mafundi wa mitaani wanaotoa huduma.

Alisema mafundi hao wa mitaani wanatakiwa wakapate mafunzo kutoka kwenye chuo hicho ama vyuo vingine vinavyotambuliwa na serikali ili kuwaepusha wananchi na madhara wanayoweza kuyapata kutokana na huduma hafifu za mafundi hao.

Alisema wananchi wanapata madhara mbalimbali wanapohudumiwa na mafundi wasiokuwa na ujuzi wa kutosha ikiwamo kuharibu mali zao na baadhi kuharibu hata vifaa vyenye umuhimu.

"Kumekuwa na tabia ya watu kufanya shughuli za kiufundi kwa uzoefu, sasa tutafanya operesheni, tutakagua vyeti vya mafundi na yeyote ambaye ataonekana hana cheti tutampa muda aje asome hapa, lakini pia hata kwa wenye vyeti vya sehemu zingine ni lazima wapate mafunzo ya muda mfupi kwenye chuo hiki ili kuwa na usalama zaidi," alisema Chalamila.

Mkuu wa Chuo hicho, Hassan Kalima, alisema chuo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa uzio wa chuo hali inayofanya kutokuwapo kwa usalama wa kutosha.

Changamoto zingine alizozitaja Mkuu huyo wa chuo ni pamoja na ufinyu wa maktaba kwa madai kuwa iliyopo ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 30 pekee, hivyo akaiomba serikali kusaidia kupanua maktaba ili kuwawezesha wanafunzi wengi zaidi kujisomea.

"Changamoto nyingine inayotukabili ni uchache wa magari ya kufundishia wanafunzi, yapo machache sana na hivyo hutuchukua muda mwingi kuwafundisha wanafunzi wetu masuala ya udereva," alisema Kalima.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wa chuo, mmoja wa walimu wa chuo hicho, Julius Mkena, alimuomba Mkuu wa Mkoa kuwawekea mazingira mazuri wafanyakazi wa chuo hicho kufanya kazi zao wanapokwenda kuhudumia wananchi.

Alisema wakati mwingine wanapata ugumu wa kuihudumia jamii kutokana na uelewa mdogo wa jamii hiyo, hivyo akamuomba Mkuu wa Mkoa kuwasaidia kuwapa kinga ili wapate ushirikiano.



Wafanyakazi wa kampuni ya ujenzi ya Mac, wakifunika bomba la maji kwa zege kabla ya kuanza upanuzi wa barabara ya Mwenge-Morocco katika eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mataifa kuhudhuria kongamano la uwekezaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya watu 600 wakiwamo wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali duniani wanatarajiwa kuhudhuria kongamano la kuhamasisha uwekezaji kwenye kilimo cha matunda na mboga katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Kongamano hilo ambalo limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Sagcot na Shirikisho la wakulima wa mboga na matunda Tanzania (Taha), linatarajiwa kuanza leo jijini Mbeya na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, anatarajiwa kuhudhuria.

Akizungumza na wandishi wa habari juzi ofisini kwake kuhusu maandalizi ya kongamano hilo, Meneja wa TIC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Pendo Gondwe, alisema kongamano hilo litawahusisha pia wadau mbalimbali wa kilimo nchini.

Alisema mpaka sasa wawekezaji kutoka katika mataifa saba duniani wameshathibitisha kushiriki kwenye kongamano hilo na kuwataka wakulima wa Tanzania kuchangamkia fursa hiyo, ili wajifunze teknolojia mbalimbali zitakazokuwa zinafundishwa.

Aliyataja baadhi ya mataifa ambayo wawekezaji hao watatoka kuwa ni pamoja na Italia, India, Afrika Kusini, Ubelgiji na Malawi na kwamba baadhi ya wawekezaji walionyesha nia ya kuwekeza kwenye sekta ya kilimo cha mboga na matunda ni wazawa.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunafikia malengo kwenye uwekezaji wa Horticulture (kilimo cha mboga, maua na matunda) katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na tumeandaa kongamano hili kwa kushirikiana na wadau mbalimbali," alisema Pendo.

Alisisitiza kuwa kwa sasa mapato yatokanayo na uuzaji wa mboga na matunda nje ya nchi yameongezeka kutoka Dola milioni 64 mwaka 2015 mpaka Dola milioni 764 mwaka 2017.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inaongeza uwekezaji kwenye sekta ya kilimo hicho ili kuongeza mapato zaidi kwa wananchi na kwa taifa. Meneja wa Sagcot, Kongani ya Mbarali, Tulleh Mloge, aliwataka wananchi kuhudhuria kongamano hilo kwa kuwa litakuwa na umuhimu mkubwa kwao na kwa taifa.

Alisema wao wanafanya kazi na wadau mbalimbali wa maendeleo hasa wanaohusika kwenye sekta ya kilimo wakiwamo wakulima wa maparachichi, viazi, nyanya, alizeti na kusisitiza kuwa kongamano hilo ni muhimu.

Mlonge alisema uzalishaji wa mazao ya matunda na mboga nchini umeongezeka kutokana na juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kwenye uhimizaji wa kilimo pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji.

"Kilimo cha mazao ya mboga na matunda kinachukua muda mfupi mkulima kuanza kuvuna matunda yake, hivyo hii ni fursa kubwa sana kwa wananchi hasa vijana kwenye uwekezaji huu na haya yote yatafundishwa kwenye kongamano letu," alisema Mlonge.

Aliwataka pia wakulima wa mazao hayo kuzingatia mahitaji ya soko kabla ya kuanza kuzalisha kwa madai kuwa kuna baadhi ya mazao yakilimwa bila kuzingatia mahitaji ya soko mkulima anaweza akaingia hasara.

## Jaji amwaga machozi akiwaaga watumishi wenzake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ALIYEKUWA Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, Robert Makaramba, amemwaga machozi ya furaha wakati akiwaaga waliokuwa watumishi wenzake wa mahakama hiyo waliojitokeza kumuaga katika viwanja vya mahakama hiyo.

Jaji Makaramba aliagwa kitaaluma mwishoni mwa wiki jijini Mbeya na kuwaachia ujumbe mzito watumishi wa mahakama wanaobaki kwenye utumishi na alipomaliza kutoa ujumbe huo ndipo alitoa machozi.

Aliwataka majaji na mahakimu kuwa wabunifu na kutumia vizuri sheria na kanuni wakati wanapofanya maamuzi kwenye mashauri wanayoendesha ili kutenda haki kwa pande zote za mashauri hayo.

Vilevile aliwataka kutumia busara katika kufanya maamuzi, huku akiwasisitiza kutumia maamuzi ya mashauri mengine yaliyowahi kufanywa kwenye kesi zingine ili wapate mwanga wa namna ya kufanya maamuzi.


"Kazi ya ujaji sio ya kujipatia fedha bali ni ya kutenda haki na ndio maana huwezi kusikia majaji wanasema wanataka kuandamana wanadai mishahara, kwahiyo ujumbe mwingine ninao waachia ni kwamba wawe wabunifu wasitumie sheria kavu kavu," alisema Jaji Makaramba. Hata hivyo, alieleza moja ya kesi ambayo aliwahi kufanya maamuzi ya kisheria, lakini yakataka kumsababishia matatizo kwa kutelekezewa mtoto na mmoja wa wanawake waliokuwa wanadai haki mahakamani hapo.

Kwa upande wake Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Tanzania, Dk. Eliezer Fereshi, alisema kwa sasa mahakama hiyo imeanza mikakati ya ndani ya kuwajengea uwezo majaji na mahakimu wa mahakama zote nchini ili waamue kesi kwa weledi na ufanisi wakizingatia sheria. Alisema watendaji hao wa ma

hakama watakuwa wanajengewa uwezo huo kwenye maeneo yao ya kazi badala ya kuwapeleka mbali ili kupunguza gharama za uendeshaji wa zoezi hilo.

"Tunataka watendaji wetu wa mahakama za chini wapewe mafunzo huku huku bila kuwa na ulazima wa kwenda kupatia mbali na eneo lao la kazi, lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha watendaji hawa wanafanya maamuzi yenye weledi," alisema Dk. Fereshi. Akizungumza kwa niaba ya mawakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, Wakili wa Serikali kutoka katika Ofisi ya Mashtaka ya Taifa, Basilius Namkambe, aliziomba idara zinazowaandaa mawakili nchini kuboresha mitaala yao ya elimu ili wazalishe mawakili bora.

Alisema endapo idara hizo zitaboresha mitaala hiyo zitakuwa na uwezo wa kuzalisha mawakili wenye ubora watakaotumika ndani na nje ya nchi.





## Sera ya viwanda kupitiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ameagiza kuanza kupitiwa Sera ya Maendeleo ya Viwanda endelevu ya mwaka 2003 ambayo itasaidia kupata sera mahsusi ya kufikia uchumi wa kati.

Bashungwa alitoa kauli hiyo jana jijini hapa katika kikao kazi cha siku mbili cha wizara hiyo, pamoja na taasisi zilizo chini yake, ambacho kililenga kupitia sera, kanuni mbalimbali ili ziweze kukidhi kiu ya Watanzania kufikia uchumi wa viwanda na kipato cha kati.

Alisema kuna haja ya kupitia sera ambazo zinasimamia utekelezaji wa kuwapeleka Watanzania kwenye uchumi wa viwanda haraka iwezekanavyo.

"Tumeona sera hizi ni za mwaka 2003 kwa mfano kuna sera ya masoko kwenye kilimo katika kufungamanisha kilimo na viwanda lazima tuwe na sera ambayo ita 'reflect' uzito wa jambo hilo," alisema.

Alieleza katika mwaka wa fedha unaoanza Julai mwaka huu, mapitio hayo ya sera lazima yakamilishwe haraka, ili yatoe nafasi ya kuangalia sheria ambazo zinatumika kwenye viwanda na biashara nchini.

"Ili mwaka wa fedha 2019/20 unapoisha tuwe tumekamilisha mapitio ya sera na sheria na utengenezaji wa kanuni zake na tunapoanza mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano tuwe na nyaraka ikiwamo sera inayosimamia azma ya kuwa na uchumi unaofungamanisha kilimo na viwanda," alisema.

Alizitaka taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kubadili mitizamo yake katika utoaji wa huduma kwa wateja, huku akisisitiza kuhakikisha kunakuwapo na ushirikiano kati ya Wizara ya Kilimo na Viwanda.

"Tuwe na mipango ambayo sio ya kushtukiza kwenye mazao ya kimkakati kama vile pamba, korosho, chai na kahawa lazima tuwe na business model (mfano wa biashara) ya kila mazao, naamini tukishirikiana tutaweza kufanikisha azma ya serikali ya ku add value (kuongeza thamani)," alisema.

Alisema kama kuna taasisi inadhibiti ihakikishe haizidishi ili kutokuwa kikwazo kwa kuwa jukumu lao ni kusaidia wadau kufikia azma hiyo.

"Changamoto niliyoona kulikuwa hakuna uratibu wa pamoja wa taasisi zilizo chini ya wizara na pia kufungamanisha kilimo na viwanda," alisema.

# Matumizi ya Hifadhi Ngorongoro kupitiwa upya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Kurekebisha Sheria, imependekeza hatua stahiki kuchukuliwa mapema ili kunusuru Hifadhi ya Ngorongoro kwa kuangalia upya mfumo wa matumizi mseto wa ardhi.

Hatua hiyo, imetokana na tume kubaini upungufu wa aina mbalimbali ikiwamo wa kisheria ambao umeathiri eneo hilo.

Sheria ya Uhifadhi ya eneo hilo ya mwaka 1959 ilitungwa na kuweka mpango jumuishi wa matumizi ya ardhi ambao uliwezesha wanyamapori, mifugo na binadamu kuishi ndani ya hifadhi hiyo.

Mwenyekiti wa tume hiyo, Jaji mstaafu January Msoffe, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akiwasilisha ripoti ya mapitio ya sheria zinazosimamia mfumo wa Sheria ya Hifadhi hiyo kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga.

Alisema Novemba mwaka jana walipokea barua kutoka kwa Mhifadhi Mkuu akiomba tume hiyo kupitia mfumo wa sheria hiyo.

Baada ya utafiti, Jaji Msoffe, alisema tume hiyo imebaini upungufu wa kisheria na kiutendaji kuathiri eneo hilo.

Alisema kuna ongezeko kubwa la watu, mifugo na wanyamapori na mwaka 1959 kulikuwa na watu 8,000, lakini kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi mwaka 2017 kuna zaidi ya watu 93,000.

"Ongezeko kubwa la watu na wanyamapori linasababisha kupungua kwa malisho ya wanyamapori na mifugo, uharibifu wa mazingira, misitu, mmomonyoko wa udongo na kukosekana kwa maji," alisema.

Jaji huyo alisema ongezeko la watu ndani ya hifadhi limesababisha kukua kwa vijiji na kuhatarisha uhifadhi na utalii.

"Hali kadhalika, wananchi waliomo ndani ya hifadhi hawaruhusiwi kufanya shughuli nyingine za kiuchumi kama kilimo na biashara na hivyo kusababisha umaskini mkubwa kwa wananchi," alisema.

Hata hivyo, alisema tume imegundua kuwa kutokana na zuio la shughuli za uchumi kwa wananchi ndani ya hifadhi, serikali kupitia mamlaka ya hifadhi hiyo inawahudumia wananchi chakula, afya na matibabu ya mifugo yao kiasi cha Sh. bilioni nane kinatumika kwa mwaka.

Aidha, alisema tume imebaini ongezeko la mifugo na mapito ya wanyama yameathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na ujenzi wa nyumba na uharibifu wa uoto wa asili kwa njia hizo.

Alisema taarifa zinaonyesha kwamba kumekuwapo na ongezeko la matukio ya ujangili kwenye hifadhi hiyo na kupungua kwa idadi ya wanyamapori adimu kama vile faru, mbwa mwitu na simba.

Mapendekezo

Mwenyekiti huyo alisema kutokana na hali hiyo, Tume inapendekeza hatua stahiki mapema kunusuru hali hiyo na kuhakikisha hifadhi hiyo inakuwa endelevu.

Akizungumza mara baada ya kupokea ripoti hiyo, Waziri Mahiga alisema serikali itazingatia mapendekezo ya tume hiyo.

"Tangu zamani nilikuwa nashindwa nikasema tusubiri siku moja italeta mgongano, nafasi ya Ngorongoro ni ndogo, tutalishughulikia suala hili," alisema.




Meneja Biashara na Mkakati wa Mauzo wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Kanda ya Kati, Baraka Siwa (kushoto), akimkabidhi zawadi ya hundi ya Sh. 500,000, mmoja wa washindi wa shindano la Tuzo Pointi, Markfason Haule, mkazi wa Kitinku Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, jana, katika Ofisi za Vodacom Kanda ya Kati zilizopo eneo la Kilimani jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunge wapewa somo utekelezaji wa bajeti

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE wameelezwa kuwa Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2019/20 itafanikiwa kutekelezwa iwapo mafungu yote ya fedha yatazingatia kikamilifu maelekezo yaliyopo kwenye mwongozo wa mpango wa bajeti.

Hayo yalielezwa jana na mtoa mada kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Muga Matitu, wakati akiwasilisha mada kwenye semina ya kamati mbalimbali za kudumu za Bunge, kuhusu mwongozo wa maandalizi ya mipango bajeti, mwaka 2019/20-2021/22.

Alisema muundo wa mwongozo umeweka wazi maelekezo yanayopaswa kufuatwa na kuanzia ngazi ya chini, ili kila mmoja aweze kutimiza majukumu yake.

Matitu alisema uchambuzi wa bajeti ni lazima uangalie nguzo tatu ambazo ni ujenzi wa viwanda, maendeleo ya watu na ufanisi katika utekelezaji na kwamba kama nguzo hizo zitatekelezwa uchumi utaua na maendeleo ya watu yataonekana.

Alisema vipaumbele vya mpango wa pili wa maendeleo wa taifa na bajeti kuu vimegawanyika kwenye maeneo manne ya kimkakati yanayolenga kukuza uchumi wa viwanda na kuboresha maisha ya Watanzania.


"Ni vyema kama tumedhamiria kutekeleza bajeti na mpango wa maendeleo ni lazima mafungu yote ya fedha yaliyotengwa yatumike kama yalivyopangwa na ile tabia ya maofisa masuuli ya kuhamisha fedha yasipewe kipaumbele kwa sababu yatakwamisha malengo ya serikali," alisema Mtitu.

Kuhusu vipaumbele vya mpango wa miaka mitano, Mtitu alisema viko vitano ambavyo ni miundombinu, kilimo, viwanda, rasilimali watu, utalii, biashara na huduma za fedha.

Kuhusu miundombinu, Mtitu alisema itawezesha kuondoa vikwazo katika uchumi kwa kuhakikisha nishati, bandari, reli, barabara na viwanja vya ndege, maji na mawasiliano vinakuwa vya uhakika.

Aidha, kwenye kilimo alisema mpango umelenga kuwezesha kuinua tija na kuwanufaisha wananchi wengi wa vijijini na maeneo ya mpango ni mazao ya uzalishaji na utaminishaji, uvuvi, misitu na mifugo.

Aliwashauri wabunge kuhakikisha wanapitia vipengele vyote kwenye mpango na bajeti na kuchambua kwa kina ili kuja na mapendekezo ya jinsi ya kuiwezesha bajeti hiyo itekelezeke kwa manufaa ya Watanzania.





Wataalamu wa afya wakiwafanyia uchunguzi wa kinywa wanafunzi wa Shule ya Kibuteni Mkoa wa Kusini Unguja, ikiwa ni Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, uchunguzi huo uliandaliwa na Jumuiya ya Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto Zanzibar (Biwo). **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Vyakula vya sukari vinaathiri meno watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto Zanzibar (BIWO) kwa kushirikiana na madaktari kutoka Wizara ya Afya imefanya uchunguzi wa afya ya kinywa kwa wanafunzi wa shule ya msingi na maandalizi ya Kibuteni, Mkoa wa Kusini Unguja.

Wanafunzi 140 wamefanyiwa uchunguzi huo na asilimia kubwa ya watoto wamegundulika kuwa meno yao yameoza.

Akizungumza baada ya uchunguzi huo, Ofisa Tabibu wa Afya ya Kinywa na Meno kutoka Hospitali ya Mpendae, Makame Shaibu, alisema sababu ya watoto hao kuoza meno ni ulaji wa vyakula vya sukari.

Aidha, alisema pia kukosekana kwa usafi wa meno kunasababisha meno kuoza au kutoboka.

Alisema wengi wa wanafunzi hao meno yao yapo katika hali mbaya na yanahitaji kung'olewa.

Aliwataka wazazi kuhakikisha watoto wanawasafisha meno tangu siku wanapoanza kuota meno badala ya kuwasubiri hadi kufika miaka mitano.

Aliitaka jamii kuacha kung'oa meno wakati tiba mbadala zipo kwa sababu kung'oa jino ni ulemavu.

Naye mlezi wa jumuiya ya BIWO, Shara Ahmed Ame, alisema wameamua kufanya uchunguzi wa afya ya kinywa kwa watoto hao kwa sababu wanahitaji kupewa haki zao ikiwamo afya.

Aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawahimiza watoto kusafisha meno yao mara mbili kwa wiki ili kuwalinda na magonjwa nyemelezi ya kinywa na meno.

# Vitendo vya udhalilishaji vyaongezeka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya Tanzania kusaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda yenye lengo la kuwalinda watoto dhidi ya udhalilishaji, bado vitendo hivyo Zanzibar vinaongezeka siku hadi siku na kurudisha nyuma makuzi ya watoto.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, Mkurugenzi wa Miradi ya SOS Zanzibar, Asha Salim Ali, alisema licha ya serikali kuwa na sheria mbalimbali, sera na mipango ya kuwalinda watoto dhidi ya aina zote za udhalilishaji, bado vitendo hivyo vinaendelea kutokea ikiwamo kubakwa na kulawitiwa.

Alisema vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa watoto vinaripotiwa katika maeneo mbalimbali na kurudisha nyuma maendeleo ya watoto na kuminya uhuru.

Hata hivyo, Asha alisema licha ya Zanzibar kutekeleza mpango wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, lakini bado inakabiliwa na kiwango cha juu cha udhalilishaji ikiwamo utelekezaji wa familia, ndoa za utotoni, ukatili wa kingono, na wa kimwili pamoja na watoto kubakwa na kulawitiwa.

Alieleza kuwa ushirikishwaji wa watoto ni moja kati ya haki zao za msingi, hivyo matumaini yake ni kuwa maadhimisho hayo yatawapa watoto fursa ya kucheza na kufurahi na kujifunza mambo mengi muhimu.

Kwa upande wake, Meneja Mradi wa huduma za simu kwa mtoto Zanzibar, Fatma Ahmada, alisema lengo kuu la maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika ni kuwakumbusha viongozi wa serikali na jamii kuwa maendeleo ya taifa hayawezi kupiga hatua bila ya kuwasaidia watoto katika kupata mahitaji yao muhimu.

Alisema bado kuna kundi kubwa la watoto wanaohitaji msaada ikiwamo maskini na wenye mahitaji maalum.

Siku ya Mtoto wa Afrika huadhimishwa kila mwaka Juni 16, Zanzibar itaadhimishwa katika kijiji cha SOS na taasisi za kutetea haki za wanawake na watoto, kwa umoja wao wameungana kuadhimisha siku hiyo na miongoni mwa taasisi hizo ni SOS, Tamwa, Zafela, Save the Children na Action Aid.

# 'Elimu chanzo cha maendeleo, ukuaji uchumi'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema elimu ni chanzo cha kila taifa kuwa na maendeleo endelevu ya kijamii na ukuaji wa uchumi wake.

Akizungumza wakati wa mahafali ya 17 ya Chuo cha Kiislam Mazizini Unguja, alisema elimu ni nuru na ndio maana hata umma uliopita uletewa mitume ili kuelimisha jamii zao katika nyanja mbalimbali na kuwa na maendeleo ya uhakika.

Simai aliwataka wahitimu wa chuo hicho kuihudumia jamii kwa kuhakikisha walimu wanaowasomesha wanapata upeo wa kufikiria, kujiamini na kuwa wataalamu wa kupeleka mbele maendeleo ya taifa lao.

Aidha, aliwataka wahitimu kuwa kigezo chema shuleni wanakofundisha kwa kuwa na tabia njema mbele ya watoto watakaowafundisha ili nao wawe vijana bora wa kulitumikia taifa lao.

Aidha, aliwasisitiza wahitimu kutotosheka na elimu waliyoipata na badala yake kuzitumia vyema fursa za kielimu zinazotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kujiendeleza zaidi katika masomo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imeazimia kukiboresha chuo hicho ili kibaki katika hadhi yake.

Naye Mkuu wa Chuo cha Kiislam Mazizini, Dk. Muhidini Ahmad, aliwasihi wahitimu hao kuwa mabalozi wazuri katika jamii zao na watendaji kazi wenye bidii wanapokuwa katika sehemu zao za kazi.

Mapema akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Said Suleiman Mohamed, alisema wapo tayari kuitumia nchi yao kwa lengo la kuleta maendeleo ya elimu kwa watoto, ili taifa liwe na wasomi bora.

Jumla ya walimu 283 wamehitimu katika fani za sayansi, sanaa ya msingi, dini na Kiarabu, kwa ngazi ya cheti na diploma.

## Serikali yaitunuku Exim utoaji damu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Tanzania ikiungana na mataifa mengine ulimwenguni katika kuadhimisha Siku ya Wachangiaji Damu Duniani, Benki ya Exim Tanzania imekabidhiwa tuzo maalum kutoka serikalini ikiwa ni utambuzi wa mchango wa benki hiyo katika kufanikisha suala zima la upatikanaji wa damu salama hapa nchini.

Benki hiyo imekabidhiwa tuzo hiyo na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika maadhimisho hayo yaliyofanyika kitaifa jijini Mwanza, viwanja vya Furahisha mwishoni mwa wiki iliyopita yakiwa na kauli mbiu 'Damu Salama Kwa Wote'.

Akiipongeza benki hiyo kwa ushiriki wake mkubwa kwenye jitihada za upatikanaji wa damu salama nchini, Waziri Ummy ambaye alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, pia aliihimiza benki hiyo kuendelea kuwa balozi imara wa damu salama hapa nchini, sambamba na kuhamasisha taasisi nyingine na watu binafsi kuungana na benki hiyo katika kufanikisha mpango huo muhimu.

"Serikali imetenga Sh. bilioni tano katika mwaka wa fedha 2019/20 zitakazotumika kujenga vituo vidogo vya uchangiaji damu salama katika mikoa 12 nchini." Alisema Ummy ambae pia alizindua mashine mpya 'full automation' za kupima maambukizi katika damu na za kupima makundi ya damu ambazo zimesimikwa kwenye vituo vya kanda sita ikiwamo Dar es Salaam, Mwanza, Tabora, Kilimanjaro, Mtwara na Mbeya.

"Tunataka kumfikia kila Mtanzania mwenye mahitaji ya damu salama popote alipo tuhakikishe anapata damu salama bila kikwazo chochote. WHO inakadiria idadi ya watu 1000 zipatikane chupa 10 za damu, Watanzania tunakadiriwa kuwa milioni 55, tunapaswa kupata asilimia moja ya idadi hiyo, hivyo chupa 550,000 zinahitajika kila mwaka kutosheleza mahitaji," alisema.

Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu, alisema: "Tumepokea tuzo na heshima hii kutoka serikalini kwa mikono miwili kwa kuwa ni sehemu ya matokeo chanya ya mkakati wa benki ya Exim ya uwajibikaji kwa jamii unaofahamika kama 'Exim Cares'. Hivyo tuzo na heshima hii ni kama chachu ya sisi kuendelea kujitoa zaidi katika kufanikisha mpango wa damu salama hapa nchini."

# Kigwangalla kuchangisha fedha za kutokomeza VVU

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangalla, amesema anatarajia kuandaa utaratibu wa makundi ya watu mbalimbali wakiwamo viongozi mashuhuri na wasanii kupanda Mlima Kilimanjaro, ili kuchangisha fedha za kuendeleza mapambano dhidi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi.

Dk. Kigwangalla alitoa kauli hiyo jana mkoani Kilimanjaro, wakati akizindua zoezi la upandaji Mlima Kilimanjaro lililoshirikisha zaidi ya watu 80 kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kuchangisha fedha za mapambano dhidi ya Ukimwi kwa kupitia kampeni ya 'Geita Gold Mining Kilimanjaro Challenge 2019'.

Kampeni hiyo ambayo iliyoratibiwa na Mgodi wa dhahabu ya Geita (GGM) kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) pia imelenga kutunisha mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi (ATF).

Alisema Wizara ya Maliasili na Utalii itaanda utaratibu wa kuhamasisha makundi ya watu mbalimbali ikiwamo wasanii na watu mashuhuri duniani kupanda Mlima Kilimanjaro ili kuchangisha fedha za mapambano dhidi ya Ukimwi kwani mapambano ya virusi hivyo ni ya watu wote na sio ya serikali pekee.

"Takwimu za maambukizi mapya hususan katika kundi la vijana yanatisha na kwamba zinahitajika jitihada za makusudi kutoka katika kundi hilo kudhibiti ugonjwa huo.

"Hali ya maambukizi mapya ya VVU yanatisha ni lazima sisi vijana tuwe mstari wa mbele kupambana na hali hii, kwa mwaka nimepanga kupanda mlima huu na watu mashuhuri ikiwamo wanasiasa na wasanii ili kuchangisha fedha kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa huu."

"Lakini pia nimefurahi kuona kuwa miongoni mwa wanufaika wa kampeni hii ni wapagazi takribani 150 waliopatiwa mafunzo ya kujilinda na VVU na masuala mbalimbali kuhusu udhibiti wa Ukimwi. Kundi hilo pia limepatiwa mafunzo ya ujasiriamali kwa lengo la kuwasaidia wawe na kipato endelevu," alisema.

Mkurugenzi wa Tacaids, Dk. Leonard Maboko, alisema kila siku watu zaidi ya 200 huambukizwa VVU ambapo kati yao asilimia 80 ni vijana kuanzia miaka 15-24.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM), Richard Jordinson, alisema kampeni hiyo imewezesha ukusanyaji wa zaidi ya Sh. bilioni 13 tangu ilipoanzishwa miaka 17 iliyopita. Alisema kampeni ya mwaka huu zaidi ya watu 80 wameshiriki, ambapo kati yao 32 watapanda mlima, 28 watauzunguka kwa kutumia baiskeli na watu 17 kutoka nchi mbalimbali wameshiriki kampeni hiyo ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

"Upandaji huo utachukua siku saba, ambapo wameanza kupanda Juni 15 na kushuka Juni 22 mwaka huu," alisema.

Alisema tangu kuanzishwa kwa kampeni hiyo miaka 17 iliyopita zaidi ya taasisi binafsi na mashirika 50 yanayotoa misaada na elimu ya Ukimwi nchini yamenufaika na kampeni hiyo.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla (kulia), akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM), Richard Jordinson, katika hafla ya uzinduzi wa zoezi la kupanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kukusanya fedha za kutomomeza maambukizi ya VVU nchini. **MPIGAPICHA WETU**

# Katazo uchimbaji mchanga mtoni

**Na Frank Monyo**

OFISA wa Maji Bonde la Wami/Ruvu, Simon Ngonyani, amepiga marufuku uchimbaji wa mchanga katika Mto Mbezi mkoani Dar es Salaam, kwa kuwa unaathiri kingo za mto na kusababisha uharibifu katika makazi ya watu.

Aidha, amekunusha taarifa zinazodai kuwa Bonde la Wami/Ruvu wameruhusu watu kuchimba mchanga katika eneo hilo.

Kauli hiyo aliitoa baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika machimbo hayo yaliopo Kawe na kukamata gari moja lililokuwa mtoni likipakia mchanga.

Wakati akizungumza na waandishi wa habari pamoja na wananchi wa mtaa wa Mji Mpya, Ngonyani, alisema kumekuwa na uharibifu mkubwa unaoendelea kwenye mto huo unaotokana na watu kujichukulia sheria na kuchimba mchanga na kuathiri kingo za mto na kuchimba hadi kwenye kuta za nyumba zilizopo karibu na mto huo.

"Nimepewa maelekezo kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni kufuatilia suala hili, kabla sijaja hapa nilikaa kikao naye, hata yeye anasema hafurahishwi na kinachoendelea hapa na hataki kuona watu wakiendela kuchimba mchanga," alisema Ngonyani. Alisema kwenye Sheria ya Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009 No 11, mwenye mamlaka ya kutoa vibali kwa mtu yeyote kuingia mtoni ni Bonde la Wami/Ruvu na sio halmashauri labda sheria ibadilike baadaye.

"Watu wengi wanaofanya shughuli za uchimbaji mchanga hapa walikuwa wanadai Mkuu wa Wilaya kawaruhusu kuchimba, jambo ambalo sio la kweli kwani hata yeye anachukizwa na uharibifu huu unaoendelea hapa na ameniagiza kupiga marufuku zoezi hili," alisema Ngonyani.

Baada ya kutolewa tamko hilo, baadhi ya wakazi wa eneo hilo ambao wana jipatia kipato kwa shughuli za uchimbaji mchanga, walidai uchimbaji mchanga katika mto huo ni sahihi kwa kuwa unazuia nyumba zao kusombwa na maji. Mjumbe wa nyumba kumi katika mtaa wa Kwamani, Mwatano Ally, alisema awali hali ilikuwa mbaya kwani mvua zikinyesha maji yalikuwa yakisambaa kwenye makazi ya watu, lakini baada ya watu kuchimba mchanga hali hiyo haikujirudia tena.

"Mvua zilizonyesha hivi karibuni hazikuleta madhara kwani maji yalikuwa yanapita bila kuingia kwenye makazi ya watu, hivyo serikali ituangalie kwani vijana wetu wanapata kipato hapa na kusaidia kuacha tabia za ukabaji," alisema. Naye Mwanaisha Shaban, alisema kwa sasa wanaona afadhari kwani mvua zinaponyesha maji hayawaletei madhara.

## HABARI KIMATAIFA



Askari wa NATO wakifanya mazoezi ya kijeshi katika Bahari ya Baltiki, wakiongozwa na kikosi namba mbili cha Jeshi la Majini la Marekani. **PICHA: AFP**.

# Polisi wafariki dunia baada ya gari lao kukanyaga bomu

**NAIROBI, Kenya**

MAOFISA wanane wa polisi katika Jimbo la Wajir nchini Kenya, wamefariki baada ya gari waliyokuwa wakisafiria kukanyaga bomu lililotegwa ardhini. Askari hao walikuwa karibu na mpaka wa Somalia.

Inspekta Mkuu wa Polisi nchini humo, Hilary Mutyambai, amethibitisha kutokea kwa mlipuko huo na kusema kuwa waliotekeleza wanatafutwa.

Wakati wa shambulizi hilo, maofisa 11 wa polisi walikuwa ndani ya gari hilo wakipiga doria katika eneo hilo ambalo limekuwa likikumbwa na vitisho vya usalama kutoka kwa kundi la Al Shabab.

Hata hivyo, kundi la Al Shabab halijajitokeza kudai kuhusika na shambulizi hilo.

Juni mwaka 2018, maofisa wengine wanane waliuawa baada ya kutokea kwa shambulizi lingine kama hilo katika kaunti hiyo. Jimbo la Wajir, Mandera na Garissa yameendelea kushambuliwa na kundi la Al Shabab, huku maofisa wa usalama wakishambuliwa zaidi.

Kenya imeendelea kupata vitisho kutoka kwa kundi la kigaidi la Al Shabab nchini Somalia, baada ya kutuma jeshi lake nchini humo mwaka 2011 kwenda kupambana na kundi hilo.

Tangu mwaka 2007, kundi la Al Shabab limekuwa likiisumbua serikali ya Mogadishu na Umoja wa Afrika (AU) uliamua kutuma kikosi chake cha wanajeshi 20,000 kukabiliana na kundi hilo la kigaidi. **RFI**

# Omar al Bashir kufikishwa mahakamani muda wowote

**KHARTOUM,** Sudan

MWENDESHA Mashtaka Mkuu nchini Sudan, Al Waleed Sayyed Ahmed amesema kiongozi aliyeondolewa madarakani, Omar al-Bashir atafikishwa mahakamani wiki ijayo.

Al Waleed Sayyed Ahmed aliwaambia waandishi wa habari kwamba Bashir anakabiliwa na mashtaka ya rushwa na kumiliki fedha za kigeni kinyume cha sheria.

Hali hiyo inatokea baada ya kupita muda wa miezi miwili tangu jeshi nchini humo lilipomwondoa Bashir madarakani kufuatia maandamano makubwa ya kitaifa yaliyopinga utawala wake.

Siku ya Alhamisi, ofisa mmoja alinukuliwa na Shirika la Habari la Sudan (SUNA), akisema Bashir anakabiliwa pia na mashtaka ya kuamuru hali ya dharura nchini Sudan.

Aprili mwaka huu, Mkuu wa Jeshi la Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan alisema fedha zaidi ya dola milioni 113 zilikamatwa kutoka kwenye makazi ya al-Bashir.

Jenerali Burhan alisema Jeshi la Polisi na wanajeshi na mawakala wa usalama walipata kiasi cha Euro milioni saba, Dola za Kimarekani 350,000 na Pauni za Sudan milioni moja.

Omar al Bashir alipotangaza hali ya dharura mnamo Februari 22 katika jitihada za kuyazima maandamano yaliyoanza kushamiri Desemba mwaka jana alipitisha amri kwamba ni kinyume cha sheria kwa mtu kuwa na fedha za kigeni zaidi ya dola 5,000.

Mwezi uliopita, Mwendesha Mashtaka Mkuu, Ahmed aliamuru Bashir ahojiwe kuhusu tuhuma za utakatishaji fedha na kufadhili ugaidi.

Mei mwaka huu, mwendesha mashtaka huyo alisema Bashir atashtakiwa kwa mauaji ya waandamanaji waliokuwa wanaipinga serikali yake jambo lililosababisha kuondolewa kwake madarakani.

Ahmed alisema watuhumiwa wengine waliotumikia chini ya utawala wa Bashir bado wanachunguzwa. Ingawa hakuwataja majina, lakini alisema tuhuma dhidi yao ni kuhusu umiliki wa ardhi.

Maandamano dhidi ya utawala wa Bashir yalianza Desemba 9, mwaka jana baada ya serikali yake kupandisha bei ya mkate.

Omar al Bashir aliondolewa madarakani na jeshi Aprili, 11 baada ya maelfu ya waandamanaji wakiongozwa na muungano wa vyama vya watu stadi kupiga kambi mbele ya makao makuu ya jeshi, katikati ya Mji Mkuu wa Khartoum kuanzia Aprili 6.

Kwa sasa Omar Bashir anazuiwa kwenye gereza la Kober.

**DW**

# Boris Johnson aongoza mbio kumrithi May

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI wa zamani wa Mambo ya Nje nchini Uingereza, Boris Johnson, ameongoza duru ya kwanza ya mchujo wa wagombea wanaowania kuchukua uongozi wa chama cha Conservative kilicho madarakani nchini humo.

Johnson, mmojawapo wa vinara wa kampeni ya kuiondoa Uingereza katika Umoja wa Ulaya (EU) amewaacha mbali wagombea wengine tisa, akipata kura 114 kati ya 313 zilizopigwa na wabunge wa chama chake cha Conservative.

Aliyeshika nafasi ya pili ni Jeremy Hunt ambaye ni Waziri wa sasa wa Mambo ya Nje, ambaye amepata kura 43, naye Waziri wa Mazingira, Michael Gove ameshika nafasi ya tatu akiwa amepata kura 37.

Wengine waliofanikiwa kuingia katika duru ya pili ya mchujo ni Waziri wa Mambo ya Ndani, Sajid Javid, aliyekuwa waziri ahusikaye na mchakato wa Brexit, Dominic Raab, Waziri wa Afya Matt Hancock, Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa, Rory Stewart.

Mawaziri Jeremy Hunt na Michael Gove wamegawana sawa kura za wabunge wenye msimamo mwepesi kuhusu mchakato wa Uingereza kuondoka ndani ya EU.

Hunt na Gove wanapendelea nchi yao kupata makubaliano na EU kabla ya kuondoka, tofauti na Johnson ambaye anataka Uingereza ifungashe virago vyake ifikapo mwishoni mwa Oktoba, bila kujali kama itakuwa imefikia mwafaka na EU au la.

Sajid Javid alisema Uingereza kuondoka ndani ya Umoja wa Ulaya sio kigezo pekee cha Brexit.

"Tunapaswa kufahamu kwamba hatutatimiza matakwa ya waliopiga kura kuunga mkono Brexit, kwa kuondoka ndani ya Umoja wa Ulaya tu. Kura ya kuondoka huko haikuukosoa tu umoja huo, bali pia mfumo wa uongozi wa Uingereza, ambao wanaamini hauendi sawa na dunia ambayo haina mustakabali mwema kwao," alisema Javid.

Wakati wagombea hao wakisalia, wenzao watatu wameng'olewa katika kinyang'anyiro hicho cha uongozi wa chama cha Conservative, ulioachwa na Waziri Mkuu wa sasa, Theresa May alipojiuzulu mwanzoni mwa Juni.

Wagombea hao ni Mark Harper, Esther McVey na Andrea Leadsom ambao hawakuweza kupata kura 17, kiwango cha chini kinachohitajika ili mgombea aingie katika duru inayofuata.

**DW**

# Anayewatuhumu polisi adai hana uwezo kwenda Mwanza

**Na Romana Mallya**

SIKU tatu baada ya Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kumtaka mkazi wa jijini Dar es Salaam, Nixon Moshi, aende mkoani humo baada ya kuwatuhumu askari watatu kumpora Sh. 1,188,000, amedai mwongozo wa nani atakaye gharamia nauli na malazi yake.

Moshi aliliambia Nipashe jana kuwa yupo tayari kwenda Mwanza kuitikia wito huo wa Jeshi la Polisi, lakini kwa sasa hana nauli wala fedha za kujikimu atakapokuwa mkoani humo.

Ijumaa iliyopita, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Jumanne Muliro, alimtaka Moshi kwenda mkoani Mwanza kwa sababu jalada la kesi ndiko lililofunguliwa.

Akizungumzia wito huo wa kamanda, Moshi alisema yupo tayari kwenda ingawa kwa sasa hana fedha.

"Nipo tayari kwenda Mwanza, lakini kwa sasa sina fedha ya nauli na ya kujikimu wakati wote nitakaokuwa Mwanza, ninaomba Jeshi la Polisi linisaidie mwongozo kwa sababu linashikilia fedha zangu, je, litanisaidia kuniwezesha kufika Mwanza na fedha za kujikimu," alihoji.

Hata hivyo, Moshi alisema mwishoni mwa wiki iliyopita alipeleka barua ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) na kupokelewa na msaidizi wake ambaye alimpa wiki moja ndipo awasiliane naye kujua nini hatima ya fedha zake.

Aidha, Moshi aliandika barua ya wazi kwa IGP, Simon Sirro, akiomba ichapishwe gazetini ili aweze kumsaidia arudishiwe fedha zake anazodai walichukua askari hao.

Alipotafutwa Kamanda Muliro kuhusu madai hayo, alimtaka Moshi aende Mwanza kwa sababu

jalada la kesi limefunguliwa mkoani humo na kwamba tayari Mkuu wa Upelelezi Mkoa Mwanza (RCO) ameshapewa maelekezo.



Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim Tanzania, Stanley Kafu (kulia), akipokea tuzo maalum kutoka kwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ikiwa ni utambuzi wa mchango wa benki hiyo kwa uhamasishaji na uchangiaji wa damu salama hapa nchini. Habari Uk. 24. **MPIGAPICHA WETU**

# Ongezeko la watu, mifugo tishio

**Na Salome Kitomari,** ARUSHA

ONGEZEKO la watu na mifugo kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), limekuwa tishio kwa binadamu, mifugo na wanyamapori.

Tangu mwaka 1959 watu waliokuwa wanaishi kwenye eneo la Serengeti waliondolewa na kupelekwa Ngorongoro ambako kumeruhusiwa wanyama wafugwao, wanyamapori na binadamu kuishi pamoja.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi wanaoishi ndani ya hifadhi katika eneo la Seneto, maarufu kama Masai Boma, walisema ongezeko hilo ni tishio kwa pande zote.

Viongozi hao waliongea na waandishi wa habari 10 wa Tanzania na Thailand, walio kwenye programu maalum ya kuandika habari za ujangili na uhifadhi, iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

Viongozi wa eneo hilo Mwenyekiti wa Vijana, Tunai Kasyaro na Mwenyekiti wa Boma, Bahati Miando, walisema mwaka jana maelfu ya mifugo ilikufa kutokana na ukame.

"Mtu alikuwa na ng'ombe 400 walikufa wote kutokana na ukame, raha ya Masai ni kuona mifugo mingi na inapokufa anabaki kuwa maskini, inatuumiza sana kichwa," alisema Miando.

Alisema eneo hilo lenye maboma saba lina watu 120 na kwamba wanajitahidi kuzuia wageni ili kupunguza ongezeko la watu kutokana na eneo kuwa ni lile lile.

Viongozi hao walisema kwa sasa wanafikiria uwezekano wa kupunguza mifugo na kufuga michache yenye tija, kwa kuwa wanaona hasara ya mifugo mingi ambayo inakosa sehemu za malisho.

"Masai na mifugo ni pete na kidole, ni raha sana sisi kuwa na mifugo, lakini mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la watu ni tishio kwetu kwa kuwa sasa ardhi haitoshi nasi tunaongezeka, huku ukame ukishika kasi," alisema Kasyaro.

Aidha, alisema pia wanatamani kuishi kwenye nyumba nzuri na kuondokana na wanazoishi sasa ambazo nyakati za mvua maji huingia ndani na maisha kuwa magumu zaidi.

Walisema kwa sasa wanauza mifugo ili wanunue chakula kingine kwa kuwa nyakati za kutegemea nyama na maziwa zimebadilika na sasa wanakula vyakula vingine.

Aliishukuru NCAA kwa kuwapa elimu, kujenga shule za msingi na sekondari zikiwamo za bweni ambazo zimewezesha watoto wao kupata elimu.

Hivi karibuni, Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Freddy Manonga, alisema kiwango cha watoto wasiojua kusoma na kuandika ni asilimia 64 na kwamba hadi sasa haijulikani sababu ni nini kwa kuwa kuna shule zenye miundombinu mizuri.

Alisema idadi ya mifugo inayokufa kutokana na ukame, magonjwa ya kimeta na kichaa cha mbwa inaongezeka, huku binadamu wanaoliwa na wanyama au kupata magonjwa ya wanyama na mifugo kupata magonjwa ya wanyamapori inaongezeka.

"Mamlaka inapata fedha nyingi sana kutokana na utalii, lakini hazifanani na maisha ya watu wa eneo husika. Tunapata wastani wa Sh. bilioni 120 kwa mwaka na watalii 600,000, lakini bado watu wetu ni maskini sana, tunawapa fedha kupitia baraza lao, lakini bado maisha yao ni yale yale," alibainisha.

# Dk.Tulia awaonya wanafunzi mapenzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewataka wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwendakulima kutojihusisha na vitendo vya mapenzi na wanafunzi wenzao.

Aidha, amewaonya walimu pia kutojihusisha na vitendo hivyo na wanafunzi kwa kuwa wazazi wamewaamini na kuwakabidhi watoto wao kipindi chote watakachokuwapo shuleni.

Dk. Tulia aliyasema hayo jana wakati akikabidhi gari aina ya Noah yenye thamani ya Sh. milioni 18 iliyotolewa na Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Shinyanga, Lucy Mayenga, katika hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama na kuhudhuriwa na wajumbe wa Baraza la Wanawake (UWT).

Aliwataka wanafunzi kuhakikisha wanakuwa na nidhamu shuleni ili waweze kufanya vizuri kwenye masomo yao na kuwataka kuwa na bidii na nidhamu shuleni kwa kuwa ndiyo silaha pekee ya mafanikio katika kufanya vema kwenye mitihani ya mwisho.

"Kipindi cha nyuma wasomi walikuwa ni wachache hali iliyopelekea viongozi kuwa wengi tofauti na sasa, ila kwasasa hauwezi kuwa kiongozi au kushika wadhifa wowote serikalini kama hauna elimu na ili uweze kuwa na elimu ni lazima uwe na bidii katika masomo na nidhamu shuleni," alisema.

Naye Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Mayenga alikabidhi gari hilo kama moja ya kuboresha miundombinu ya elimu na kusaidia kupunguza changamoto ya usafiri kwa wanafunzi na walimu.

Pia alikabidhi mifuko ya saruji 360 katika vituo vya afya, kituo Ukune Halmashauri ya Ushetu kilipata mifuko ya saruji 100, Wendele, mifuko 100, Isaka mifuko 100, huku mifuko 50 ikipelekwa Sekondari ya Mwendakulima kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule hiyo.

Aidha, Mayenga alitoa mifuko 10 kwa ajili ya kujenga uzio wa nyumba ya chama, mashuka 100 Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, kikundi cha kinamama cha Ushetu, viti 100 vya plastiki na kadi 1000 za Chama Cha Mapinduzi kwa jumuiya hiyo, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 39.5.

Mayenga alisema mifuko hiyo ya saruji iliyoelekezwa kwenye vituo vya afya itasaidia katika ukamilishaji wa ujenzi na kuwapunguzia adha wajawazito kutembea umbali mrefu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**


## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI ,** Mtu wa IT diploma anahitajika na Mesenger form six. Mawasiliano: 0715 885533


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI


## CHETI KIMEPOTEA



115275802

**JUVENTUS BAITU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0152/0557** kilichotolewa na SHINYANGA SEKONDARI mwaka 1995. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CD/IR/RB/3393/2019.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA ILEMELA**

**SHAURI LA NDOA NO 03 OF 2018**

**NGONZI SEFOLOZA BYAMUNGU.....MDAI**

**DHIDI YA**

**ROMULUZI EMMANUEL MSUNGA......MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**MJIBU MAOMBI POPOTE PALE ULIPO**

KWA KUWA, mdai ameleta madai yake ya kesi ya ndoa na yameelekezwa katika mahakama ya wilaya ilemela mkoa wa Mwanza,shauri limepangwa hukumu tarehe 18.06.2019 saa mbili na nusu asubuhib mbele ya mheshimiwa KALEGEYA RM

HIVYO BASI unatakiwa kufika mahakamani wewe mwenyewe au wakili wako au mtu ambaye anaruhusiwa kisheria na kutakiwa kuja kusikiliza hukumu upatapo taarifa hii kupita tangazo hili

ANGALIA kama hautahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, mahakama itatoa uamuzi upande mmoja.

**IMETOLEWA NA MAHAKAMA YA WILAYA YA ILEMELA**
**TAREHE 03/06/2019**
**HAKIMU**
**MH,KALEGEYA, RM**

---

**JAMURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MWANZA**

**SHAURI LA MADAI YA ARIDHI NA.29 YA MWAKA 2018**

**BENEDICTOR SAMWELI MUGOSI...........................MDAI**

**DHIDI YA**

**1 OLIPA STANSLAUS SAMWEL**
**2. STANSLAUS SAMWELI................................WADAIWA**
**3. MLIMI SYLIVESTER SAMWEL**
**4 MUGOSI SYLIVESTER SAMWEL**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA,**
**1. OLIPA STANSLAUS SAMWEL**
**2. STANSLAUS SAMWELI**
**3. MLIMI SYLIVESTER SAMWEL**
**4 MUGOSI SYLIVESTER SAMWEL**

**POPOTE MLIPO**
mdai katika shauri tajwa hapo juu amefungua shauri katika mahakama hii na shauri hilo limepangwa kusililizwa tarehe 18/o6/2019
mnatakiwa kufika mahakamani siku hiyo .pia mnatakiwa kujibu kiapo kinzani kabla ya tarehe tajwa.
kumbuka kuwa msipofika ninyi au wawakilishi wenu shauri hili litatolewa uamuzi upande mmoja.

---

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**PASTORY .B. KUGENDA** MKAZI WA NGOKOLO MANISPAA YA SHINYANGA.
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFA YAKE YA KIWANJA **NAMBA 196 KITALU "NN" (HD)** NDALA AMBAYO ILIPOTEA TANGU MWAKA 2017 MAENEO YA SHINYANGA.
KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA **PASTORY .B. KUGENDA KWA SIMU NAMBA 0765951152. RB NAMBA SHY/RB/2019.**

215278002

---

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR MARA AT MUSOMA**

**MISC. APPLICATION NO. 461 OF 2019**

**ATHUMAN ALLY NYABANGE ............. APPLICANT**

**VERSUS**

**JOHN PETRO LUSAYA**
**(Administrator of the late......................... RESPONDENT**
**Suzana Peter Lusaya**

**SUMMOUNS/ NOTICE**
**TO,**
**JOHN PETRO LUSAYA**
**(Administrator of the late**
**Suzana Peter Lusaya**

The above mentioned applicant has instituted a suit in this Tribunal, against you, particulars of which ara mentiond in a copy of the Application which is obtainable from the registry of this Tribunal, **YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL** in person(s)for mention on 02nd July 2019 at 08:00 am in the fore noon.

**TAKE NOTISE THAT;**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence.


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0766 721 072

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Bayern kumnasa Bale kwa mkopo



**MUNICH,** Ujerumani

HUKU Real Madrid ikiangalia namna ya kumuondoa Gareth Bale kipindi hiki cha majira ya joto, Bayern Munich inaweza kutoa ofa ya kumsajili kwa mkopo kwa ajili ya msimu ujao, kwa mujibu wa Gazeti la The Sun.

Manchester United tayari imekataa kumsajili raia huyo wa Wales, hivyo mabingwa hao wa Ujerumani wapo tayari kumchukua na kumlipa mshahara wake.

Bale anachukua mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki baada ya makato ya kodi, na Bayern wapo tayari kumbeba kwa ajili ya kwenda kuziba nafasi ya Arjen Robben na Franck Ribery, ambao wameondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Bosi wa Real Madrid, Zinedine Zidane, hakuficha kuonyesha wazi kwamba hana mipango na Gareth Bale, licha ya kuwa ndiye mchezaji aliyefunga mabao muhimu zaidi kwa timu hiyo kwa miaka ya hivi karibuni.

Hata hivyo, Bale mwenyewe ameshabainisha wazi kwamba hana mpango wa kuondoka klabuni hapo kuelekea msimu mpya, ingawa Zidane ameshabainisha hayupo kwenye mipango yake.

Real inataka kumuuza Bale kipindi hiki cha majira ya joto kwa ajili ya kupata fedha za kuimarisha kikosi chao, huku tayari wameshamsajili kwa gharama kubwa Eden Hazard, Luka Jovic na Ferland Mendy.

Na sasa wanaangalia uwezekano wa kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kumsajili nyota wa Manchester United, Paul Pogba.

# PSG yazipiku Barca, United kwa De Ligt



**PARIS,** Ufaransa

BEKI anayewindwa zaidi Ulaya kwa sasa, Matthijs de Ligt anajiandaa kujiunga na Paris Saint-Germain na hivyo kuwaacha kwenye mataa Barcelona na Manchester baada ya miamba hao wa Ufaransa kutoa ofa nene ya mshahara wa pauni milioni 17 kwa mwaka, kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail.

De Ligt mwenye umri wa miaka 19, amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa kubwa Ulaya baada ya kuwa na wakati mzuri pale Ajax ambayo ilitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na sasa PSG wamefanikiwa kushawishi kwa kumpa mshahara mkubwa.

Mchezaji huyo pia ametajwa kuvutiwa zaidi na Ligi ya Ufaransa ili ajiimarishe zaidi kabla ya kugeugia Ligi ya Hispania, La Liga, au ile ya England.

Hii inamaana kwamba, mbio za Barcelona na Man United kumwania mchezaji huyo sasa zinaelekea ukingoni kwani wameshindwa kushindana na matajiri hao wa jijini Paris.

Ingawa bado haijatwaa ada ya mchezaji huyo ya kutua hapo PSG, lakini Gazeti la Daily Mail limeripoti kwamba, tayari klabu hizo mbili zimeshafikia makubaliano juu ya nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi.

# NYOTA UFARANSA AJIPELEKA ARSENAL



**LYON,** Ufaransa

MCHEZAJI wa timu ya Taifa ya Vijana ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 20, Alexis Claude-Maurice anataka kusajiliwa na Arsenal, lakini klabu kubwa 10 zinamwania mshambuliaji huyo wa Lorient, kwa mujibu wa Sky Sports.

Chanzo kimoja kimenukuliwa na Sky Sports kikieleza kwamba Claude-Maurice amezitaja klabu za Borussia Monchengladbach, RB Leipzig, Lyon, Lille, Monaco, Marseille, Sevilla, Brighton, Newcastle United na West Ham kwamba zote zinamtaka.

Ingawa bado taarifa hazijatihibitishwa, lakini inadaiwa kwamba, Arsenal juzi Jumamosi tayari ilishatoa ofa ya pauni milioni 14 kwa ajili ya kumsajili Claude-Maurice.

Mmiliki wa Lorient ameripotiwa akisema kwamba ndio kwanza amerudi kutoka likizo na yupo tayari kumuuza Claude-Maurice kwa kiasi kikubwa cha fedha.

West Ham ilitoa ofa yake ya kumsajili mshambuliaji huyo mwezi uliopita, lakini ilikataliwa.

Lakini Claude-Maurice mwenyewe ameripotiwa kwamba anataka kujiunga na Arsenal kwani ndiyo timu anayoipenda.

# MESSI: TUMEFUNGWA LAKINI BADO TUNA NAFASI



**SAO PAULO,** Brazil

NAFASI ya Lionel Messi kubeba taji la kimataifa imeanza kuwa ngumu kwake baada ya timu yake ya Taifa ya Argentina kukubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Colombia kwenye mchezo wake wa kwanza wa michuano ya Copa America, juzi Jumamosi usiku.

Argentina ilishindwa kabisa kupenya ngome ya Colombia katika kindi cha kwanza na 'wahuni' hao wa jiji la Bogota wakapata bao la kwanza katika dakika ya 71 likifungwa na Roger Martinez.

Wakati Argentina ikitafuta namna ya kusawazisha bao hilo, mambo yalikwenda mrama zaidi wakati Duvan Zapata alipofunga bao la pili na kufanya matokeo kuwa 2-0.

Mara baada ya mchezo huo, Messi aliwaambia waandishi wa habari kwamba hawakuanza mchezo huo kama walivyotaka wao.

"Hii si kama tulivyotaka sisi kuanza," alisema Messi ambaye alionekana kuwa na huzuni kubwa.

"Kwa uhakika kuna vitu vinatutia hofu, tulitaka kuanza vizuri na sio kufanya makosa."

Aliongeza, "Tunatakiwa kuendelea kunyanyua vichwa vyetu juu na kufikiria kuhusu mchezo ujao, kwa sababu huu ni mwanzo tu na bado kuna mechi nyingi za kucheza zimebaki za Copa," alisema.

Licha ya uwapo wa Messi, Sergio Aguero na Angel Di Maria mbele, lakini Argentina haikuweza kabisa kupenya ngome ya Colombia.

Colombia sasa inaongoza kundi hilo B kwa pointi tatu, huku Qatar ambayo ni mwalika na Paraguay zilicheza jana Jumapili.



## Madrid yamsajili 'Messi' wa Japan

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imetangaza kumsajili kiungo wa FC Tokyo, Takefusa Kubo.

Kubo, ambaye amekuwa akitajwa kama 'Messi wa Japan', alikuwa pia akiwaniwa na Barcelona, alianza kuichezea timu ya wakubwa ya Japan mapema mwezi huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, yupo na timu yake ya Japan kwenye michuano ya Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, kama timu mwalika katika michuano hiyo inayofanyika nchini Brazil.

Katika taarifa yake, Madrid ilisema Kubo ataichezea kwanza timu yao ya vijana pale Castilla msimu ujao, kabla ya kumpandisha kwenye timu ya wakubwa.

"Real Madrid itakuwa na mmoja wa wachezaji wenye vipaji vya ukweli duniani, kwani ni kiungo mshambuliaji ambaye ana akili ya mpira na mwenye nguvu na mbinu bora za soka," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Gazeti la Marca limeripoti kwamba Madrid italipa euro milioni mbili kwa Klabu ya FC Tokyo na imempa mkataba wa miaka mitano mchezaji huyo wenye thamani ya euro milioni moja.

Kubo atafanya mazoezi na kikosi cha kwanza cha Zinedine Zidane wakati akiendelea kucheza pale Castilla, kama ilivyokuwa kwa wachezaji waliosajili hivi karibuni, Martin Odegaard na Vinicius Junior.

## Kipigo Liverpool nusu kinitoe uhai - Suarez

**SAO PAULO,** Brazil

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Luis Suarez, amesema alipatwa na mshtuko na maumivu makubwa mno baada ya kutolewa na Liverpool kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Amesema maamuzi yale yalikuwa sawa sawa na wakati alipotolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumng'ata mwenzake kwenye Kombe la Dunia mwaka 2014 nchini Brazil.

Barca walionekana kama vile tayari wametinga fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi Ulaya ngazi ya klabu, wakati walipopata ushindi wa 3-0 kwenye mchezo wa kwanza, lakini mchezo wa marudiano wakajikuta wakichezea kichapo cha 4-0 katika dimba la Anfield ambako Suarez aliwahi kucheza.

Na Liverpool ikashinda kombe hilo kwa kuifunga Tottenham Hotspur mabao 2-0 kwenye fainali.

"Siku chache baadaye, tulivyorudi Barcelona, ulikuwa wakati mbaya zaidi katika maisha yangu ya soka kama ilivyokuwa kwenye Kombe la Dunia mwaka 2014. Nilitaka kuondoka duniani," alisema mshambuliaji huyo wa Uruguay katika mahojiano na Fox Sports, akikumbukia namna alivyomng'ata meno beki wa Italia, Giorgio Chiellini na kujikuta akifungiwa kucheza soka kwa miezi minne.



"Sikutaka kuwapeleka watoto wangu shule, kila mmoja angeweza kuniona nilikuwa baba mbaya. Kulikuwa na siku ambazo sikutaka kufanya lolote, ulikuwa wakati mgumu mno kwangu."

Aidha, Suarez amesema hakuwahi kufikiria kama historia hiyo ingejirudia pale kwenye dimba la Anfield wakati walipofungwa na Liverpool.

"Sikuoana namna Liverpool wanaweza kututoa, kwa sababu Barcelona tulikuwa mbele na tulikuwa na kikosi bora kabisa na tulikuwa na nafasi kubwa zaidi.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA AZIITA JUVE, REAL MADRID MEZANI

●●● Kuna mambo mengi yanaongelewa na mawazo mengi pia, nadhani kwangu ni muda muafaka kupata changamoto nyingine...

**TOKYO,** Japan

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba ameziita Juventus na Real Madrid baada ya jana kueleza kwamba atafungua milango ya kuondoka kwa miamba hiyo Premier League, kufuatia kuwaambia waandishi wa habari jijini Tokyo, Japan kuwa 'unaweza kuwa muda mwafaka kwake kupata changamoto mpya kwingineko'.

Mfaransa huyo amekuwa akihusishwa na kujiunga na Real Madrid ili kufanya kazi na kocha Zinedine Zidane, ama kurudi klabu yake ya zamani ya Juventus.

Wakati wa Pogba hapo Manchester United umejumuishwa na matatizo yakiwamo kutofautiana na kocha wa zamani, Jose Mourinho, huku akilaumiwa kutocheza kwa kiwango, na sasa amedai kuhitaji kuondoka.

**"Kama ulivyosema, kuna mambo mengi yanaongelewa na mawazo mengi pia," Pogba, 26, aliwaambia wanahabari jijini Tokyo.**

"Kwangu mimi nimekuwa Manchester kwa kipindi cha miaka mitatu na imekuwa ikifanya vizuri; baadhi ya nyakati nzuri na nyakati nyingine mbaya, kama ilivyo kwa kila mtu. Kama kila sehemu yoyote.

"Baada ya msimu huu na kila kitu kitakachotokea msimu huu, na msimu wangu kuwa mzuri pia... nadhani kwangu mimi unaweza kuwa muda mwafaka kupata changamoto nyingine kwingineko.

"Ninawaza kuhusu hili: Kupata changamoto mpya kwingineko."

Pogba, ambaye alitua Old Trafford akitokea Juventus kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya pauni milioni 89 Agosti mwaka 2016, ameshuhudiwa timbwili lake na Mourinho, likifanya nafasi ya kocha huyo kurithiwa na Ole Gunnar Solskjaer.

Kiungo huyo alitofautiana na Mourinho mwanzoni mwa msimu uliomalizika, lakini kiwango chake kikawa kimeimarika chini ya Solskjaer.

Hata hivyo, kwa ujumla mshindi huyo wa Kombe la Dunia katika kiwango chake ameshuhudiwa akifunga mabao 24 kwenye mechi 92, alizoichezea United na akiwa ametangazwa kuwamo katika kikosi bora cha msimu cha Premier League.

Aidha, Sportsmail liliripoti wiki iliyopita kuwa kocha wa Madrid, Zidane bado hajanyoosha mikono juu katika mpango wake wa kuipata saini ya Pogba, hata baada ya kuwa ametumia pauni 344 majira haya ya joto.

Pogba pia anataka kutua Bernabeu majira haya ya joto licha ya United kutokuwa tayari kumuuza, kwa mujibu wa taarifa kutoka Hispania. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, mkataba wake wa sasa hapo Old Trafford unamalizika majira ya joto mwaka 2021.

Ukurasa wa mbele wa Gazeti la Tuttosport, jana ulisomeka: 'Pogba-De Ligt Juve Blitz'.

Mabingwa hao wa Serie A, pia wanataka kuharakisha mchakato wa mazungumzo na kiungo huyo wa United na pia wanataka kuona kama wanaweza kuendelea na mpango wa kufanikisha kuipata saini ya beki wa Ajax, Matthijs de Ligt, kwa mujibu wa gazeti hilo la Italia.

## KWA UFUPI

### SALAH AZIKATALIA REAL, JUVE
MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah, 27, amekataa kuondoka katika klabu hiyo kwa pauni milioni 150 ili kwenda kujiunga na Real Madrid ama Juventus. (Mirror)

### SOLSKJAER KUMKOSA GRIEZMANN
KIKOSI cha Ole Gunnar Solskjaer, kinajiandaa kumkosa mshambuliaji wa Atletico Madrid, Mfaransa Antoine Griezmann, 28, kutokana na Barcelona kujiandaa kutoa ofa ya pauni milioni 150. (Mirror)

### RASHFORD KUZUIWA REAL, BARCA
STRAIKA wa England, Marcus Rashford, 21, atapewa ofa ya mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki ili kubaki Old Trafford na kuzizuia Real Madrid na Barcelona kumpata. (Sun)

### JESUS APUUZIA KUSEPA CITY
MSHAMBULIAJI wa Brazil, Gabriel Jesus, 22, amesema ni "nje ya swali" kwamba yeye na straika Muargentina Sergio Aguero, 31, wataondoka Manchester City majira haya ya joto. (Mail)

### MAGUIRE ATOA SIRI KUONDOKA
BEKI wa Leicester na England, Harry Maguire, 26, alikubaliana na aliyekuwa mmiliki wa klabu hiyo, marehemu Vichai Srivaddhanaprabha kwamba ataondoka majira haya ya joto. (Mirror)

### MCCARTHY KUMRITHI MIGNOLET LIVER
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, 52, yupo tayari kuziba pengo la kipa namba mbili, Simon Mignolet, 31, ambaye anatarajiwa kuondoka majira haya ya joto, kwa kumsajili mlinda mlago wa Southampton, Alex McCarthy, 29, ili kumsaidia Alisson. (Mirror)

### ARSENAL KUMRUDIA CLAUDE-MAURICE
Arsenal itatoa ofa ya tatu kwa mshambuliaji wa Lorient, Mfaransa Alexis Claude-Maurice baada ya kukubaliana malipo binafsi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (Metro)

### TRIPPIER AGEUKA LULU JUVE
Juventus ipo tayari kumfuata beki wa pembeni wa Tottenham na England, Kieran Trippier, 25, ikiwa na dau la pauni milioni 45. (Times)

### BENTEKE ANOGEWA PALACE
MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ubelgiji, Christian Benteke, 28, anataka kubaki Crystal Palace licha ya kuhusishwa na kutimkia China. (Standard)

### KESSIE CHAMBO KWA TORREIRA
AC Milan inaweza kumtoa ofa Kiungo Muivory Coast Franck Kessie, 22, kwa Arsenal ili kumpata kiungo wa kimataifa wa Uruguay, Lucas Torreira, 23. (Gazzetta dello Sport - in Italian)

### BAKAYOKO AFUNGUKA PSG
KIUNGO wa Chelsea na Ufaransa, Tiemoue Bakayoko, 24, amesema anataka siku moja kuichezea Paris St-Germain. (L'Equipe - in French)

### STURRIDGE KUMPELEKA KLOPP SOKONI
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amekuwa akielezwa kuhakikisha anatafuta mbadala wa wachezaji wawili wanaoondoka; beki Mhispania Alberto Moreno, 26, na straika Daniel Sturridge, 29. (Star)

### RICHARLISON AMVUTA NERES EVERTON
MSHAMBULIAJI wa Everton, Richarlison, 22, amemwambia mchezaji mweza wa Brazil na straika wa Ajax, David Neres, 22, ajiunge naye Goodison Park. (Liverpool Echo)

HABARI MICHEZO

# MAYANGA MBIONI KUJIUNGA NA KMC

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Salum Mayanga, anatarajiwa kutua katika kikosi cha KMC FC kurithi mikoba iliyoachwa na Mrundi Etienne Ndayiragije, ambaye tayari ametangazwa kujiunga na Azam FC, zote za jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Mayanga msimu uliomalizika alikuwa akifundisha Mbao FC ya jijini Mwanza ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa zilizopatikana jana jijini zinaeleza kuwa uongozi wa KMC umeanza mazungumzo na Mayanga baada ya kushindwa kufikia makubaliano na Selemani Matola, ambaye jana alisaini mkataba rasmi wa kuitumikia Polisi Tanzania.

"Tayari ameshaanza mazungumzo na mambo yakienda vema, Mayanga atakuwa kocha mpya wa KMC, tunaamini tutamaliza majadiliano vizuri," alisema kiongozi mmoja wa KMC.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa wameanza kwanza kuboresha benchi la ufundi, ili kumpa nafasi kocha huyo mpya aweze kusajili wachezaji anaowataka na anaoamini watamsaidia katika msimu ujao.

Timu nyingine ambazo Mayanga amewahi kufanya nazo kazi hapa nchini ni Mtibwa Sugar ya Manungu, Turiani mkoani Morogoro na Tanzania Prisons ya jijini Mbeya.

Klabu zote zinazotarajiwa kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao zimeshaanza kuboresha vikosi pamoja na mabenchi ya ufundi kwa lengo la kujiandaa kuonyesha ushindani katika ligi hiyo na mashindano mengine watakayoshiriki.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, akiwasalimia kwa kuwapungia mikono wanachama wa Yanga, mashabiki na wadau mbalimbali wa michezo waliojitokeza kuichangia klabu hiyo katika tamasha la "Kubwa Kuliko" lililofanyika Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam juzi, ambapo jumla ya Sh. milioni 920 ahadi na taslimu zilipatikana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Wanamichezo wanawake waitwa darasani

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

WADAU wa michezo wanawake wametakiwa kujitokeza kushiriki katika kozi mbalimbali za kufundisha mpira wa miguu, ili kushiriki kikamilifu kwenye maendeleo ya michezo hapa nchini.

Ushauri huo ulitolewa na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza wakati akiwakabidhi vyeti wahitimu waliomaliza kozi mbalimbali katika Chuo cha Michezo cha Malya kilichoko jijini hapa.

Shonza alisema wanawake hawatakiwi kukaa nyuma na badala yake kujitokeza kushiriki katika kozi hizo kama wanavyojiandikisha kwenye mafunzo mbalimbali kwenye chuo hicho na vingine ndani na nje ya nchi.

Waziri huyo aliongeza kwamba anaamini katika mahafali yajayo, idadi ya wanawake itaongezeka, kwa sababu anajua wana uwezo mkubwa wa kuyafikisha kwa wachezaji chipukizi, kuanzia kwenye ngazi ya familia.

"Nawashauri wanawake wajitokeze zaidi kushiriki kozi hizi za ukocha, hii itawasaidia nao kushiriki kuwaandaa wachezaji na pia kupambana kwenye kazi hiyo kama zilivyo taaluma nyingine," alisema waziri huyo.

Naye Mkuu wa Chuo hicho cha Michezo Mallya, Richard Mganga, alisema ni faraja kwake kuona chuo hicho kimeendelea kuwa faraja ya kuwaandaa makocha wa michezo mbalimbali.

# Dodoma kufua makocha wake

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Soka Mkoa wa Dodoma (Dorefa), kimetangaza kuendesha kozi maalumu ya ukocha wa mchezo huo itakayofanyika kuanzia Alhamisi jijini humo, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Dorefa, Mussa Kissoyi, alisema kozi hiyo itakuwa ni ya ngazi ya kati na gharama zake kwa kila mtu ni Sh. 150,000.

Kissoyi alisema anaamini kozi hiyo itasaidia kuwapa nafasi makocha wao wanaohitaji kuboresha viwango vyao kujiandikisha na hatimaye kupata sifa za kufundisha timu za madaraja mbalimbali hapa nchini.

"Tunapenda kuwatangazia wadau wetu kuwa Dorefa kwa kushirikiana na Chama cha Makocha jijini hapa kitaendesha kozi ya ngazi ya kati itakayofanyika Juni 20 katika Shule ya Msingi Uhuru. Ada ya ushiriki ni Sh. 150,000 ambayo italipwa na kila mshiriki," alisema Kissoyi.

Kiongozi huyo alimtaja mkufunzi anayetambuliwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), George Komba, wa jijini hapa ndiye atakayeongoza mafunzo hayo.

"Hii si kozi ya kwanza, tumekuwa tukiendesha mafunzo mara kwa mara kutokana na mahitaji tunayokuwa nayo, kwa sababu tunahitaji kuona Dodoma inazalisha makocha wanaotambulika rasmi na watakaotumika kuibua vipaji vipya," aliongeza.

Bado Dodoma inaendelea kupambana kuhakikisha inaipandisha timu yake ya Dodoma FC Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini kwenye Ligi Kuu ya Wanawake inawakilishwa na Baobao Queens.

# ZFF yatangaza nyota Afcon 1980 wa kuishuhudia Taifa Stars

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WACHEZAJI wawili wa zamani waliowahi kuchezea timu ya Taifa ya Tanzania iliyoshiriki Afcon mwaka 1980 wameteuliwa kwenda nchini Misri kuangalia michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Juni 21, mwaka huu.

Wachezaji hao ni Othman Abdallah Foumen na Seif Nassor Bausi ambao wamepata udhamini wa asilimia 100 kutoka kwa Taasisi ya Mimi na Wewe Foundation.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi fedha zilizotolewa na taasisi hiyo, Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu alisema hatua hiyo ni kudhihirisha kwa vitendo dhamira ya uongozi mpya ya kuwatambuwa wachezaji hao wa zamani.

Alisema wachezaji hao wametoa mchango mkubwa katika soka la Zanzibar ambao kwa kiasi kikubwa unapaswa kuenziwa.

"Itakumbukwa katika moja ya kampeni yangu wakati naomba ridhaa ya kuchaguliwa kuwa Rais nilisema moja ya vipaumbele vyangu ni kuwatambua wachezaji wa zamani na kutunza kumbukumbu zao ambapo kupitia hadhara hii leo tumeanza kwa kushirikiana na kamati yangu," alisema.

Alieleza ZFF imekuja na wazo la kuwaenzi wachezaji hao wa zamani, ambapo kwa kuanzia watawapeleka wachezaji hao wawili ambao watakaa Misri kwa muda wa siku 10.

Hata hivyo, alisema wakati wakipata udhamini huo wa siku 10, watashuhudia mechi za hatua ya makundi ya Taifa Stars na kama itasonga mbele wataomba udhamini mwingine ili kuendelea kubakia hadi mwisho wa mshindano hayo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Mimi na Wewe Foundation, Ayoub Mohammed Mahmoud, ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, alisema suala la ushirikishwaji wa wachezaji wa zamani katika suala la michezo ni kuonyesha umoja na ushirikiano uliopo baina ya viongozi hao na wanamichezo wa zamani.

"Umoja na ushirikiano ndio dhana nzima ya kuonyesha kwamba Zanzibar inaendelea kimichezo na hakuna anayeachwa nyuma," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi wa shirikisho hilo kuwaona wachezaji hao kama ni moja ya familia katika michezo ikiwa katika kuendeleza michezo ili lengo la rais wa nchi liweze kufikiwa.

# Michezo

Jumatatu Juni 17, 2019

Nipashe


Pogba aziita Juve, Real Madrid mezani



HABARI UK. 30

HUFURUKUTI...



Kipa wa Colombia, David Ospina, akiwahi kutoka kuokoa hatari dhidi ya mshambuliaji wa Argentina, Sergio Aguero kwenye mechi ya Kundi B ya michuano ya Copa Amerika iliyopigwa nchini Brazil usiku wa kuamkia jana. Colombia ilishinda 2-0. HABARI UK. 29. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA SASA YA HISTORIA

## Mwakalebela aeleza 'Kubwa Kuliko' ilivyoleta matumaini, mamilioni yamiminika usajili mastaa...

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Yanga umesema klabu yao itaandika historia ya kufanya vema katika kila mashindano watakayoshiriki msimu ujao kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika harambee yao maarufu "Kubwa Kuliko" iliyofanyika juzi kwenye Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, walikuwa wageni walioalikwa katika harambee hiyo ambayo ilikusanya ahadi na fedha taslimu kiasi cha Sh. milioni 920.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema baada ya kufanikiwa kupata fedha hizo, wanaamini wataanza msimu mpya kwa kishindo na watatimiza malengo yote waliyojiwekea.

Mwakalebela alisema wamejipanga kurejesha heshima na hadhi ya Yanga ambayo wanachama wake wameikosa kwa kipindi cha misimu miwili mfululizo.

Alisema mafanikio yaliyoonekana katika harambee yao, umoja na ushirikiano kutoka kwa makundi yote ya wanachama, ni vitu vinavyowapa nguvu viongozi kwamba hakuna kitakachokwama.

"Tumejipanga kuweka historia, si katika Ligi Kuu Tanzania Bara tu, kila mashindano tutakayoweka mguu, Yanga ile mliyokuwa mnaijua ndiyo itarudi, kila kitu kitakwenda vizuri, tutashindana na tutashinda," alisema Mwakalebela.

Aliongeza kuwa kutokana na fedha walizopata, kikosi chao kitaendelea kujiimarisha kwa kusajili wachezaji wenye uzoefu na kuwalipa malimbikizo ya mishahara baadhi ya nyota wao wa zamani ambao wanadai.

"Tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa, malengo yametimia, tunasema asanteni Wanayanga wote, hii ni timu yetu, lazima tushiriki kuisaidia kwa kila hali, sisi ni mashahidi, tukutane uwanjani," Mwakalebela alisema.

Waziri Mkuu, Majaliwa katika hotuba yake hapo juzi alisema kama hakuna Yanga imara, basi hakutakuwa na ushindani kwenye Ligi Kuu na mashindano mengine ya nje ambayo timu za hapa nchini zitashiriki.

"Naomba nimalizie, bila Yanga imara, huwezi kuwa na Simba imara, na bila Simba imara, huwezi kuwa na Yanga imara," Waziri Mkuu huyo ambaye pia ana taaluma ya ukocha wa mpira wa miguu mwenye leseni inayotambuliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf) alihitimisha.

Naye Rais Kikwete aliwataka viongozi wa Yanga kuhakikisha wanawekeza katika soka la vijana ili baadaye kuisaidia Timu ya Taifa (Taifa Stars), badala ya sasa kuwalipa fedha nyingi makocha ambao wanawaimarisha wachezaji wengi wa kigeni wanaokwenda kuzichezea nchi zao, inapofika suala la utaifa.

Rais Kikwete aliwataka pia mashabiki wa Yanga kuacha kuwa wanyonge wanapokwenda viwanjani na badala yake kujitokeza kwa wingi na kuishangilia timu yao kama wanavyofanya watani zao, Simba.

## Moris hatihati kuikosa Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

HALI ya beki wa kati wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Aggrey Moris, kuweza kuitumikia timu yake katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, ambazo zitaanza Ijumaa nchini Misri, iko mashakani, imefahamika.

Taifa Stars inayofundishwa na Mnigeria Emmanuel Amunike, itaanza kutupa karata yake ya kwanza katika fainali hizo Jumapili dhidi ya wenzao wa Senegal.

Moris, beki mkongwe wa mabingwa wa Kombe la FA Tanzania, Azam FC aliumia mguu katika mechi ya kirafiki dhidi ya wenyeji Misri, na jana hakuwa sehemu ya kikosi kilichoshuka dimbani kuivaa Zimbabwe.

Akizungumza na Nipashe kutoka jijini Cairo jana, Meneja wa Stars, Danny Msangi, alisema tayari beki huyo ameshafanyiwa vipimo vya MRI na hatima yake kuelekea mashindano hayo ilitarajiwa kujulikana jana jioni.

Msangi alisema kwa sasa kocha Amunike anaendelea na maandalizi yake kwa sababu anafahamu kila nafasi ina wachezaji zaidi ya mmoja.

"Ni mgonjwa na ameshafanyiwa vipimo, leo (jana) jioni ndio tutajua nini nafasi yake," Msangi alisema kwa kifupi.

Amunike alitarajiwa kutumia wachezaji tofauti na wale walioivaa Misri, katika mchezo mwingine wa kirafiki dhidi ya Zimbabwe uliotarajiwa kufanyika jana usiku.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002